
# Kiswahili

## Shule za sekondari

### Kitabu cha Mwanafunzi

Kidato cha Kwanza




Taasisi ya Elimu Tanzania

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Kiswahili

## Shule za Sekondari

## Kitabu cha Mwanafunzi

## Kidato cha Kwanza



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 524

Jina la Chapisho: Kiswahili Shule za Sekondari Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Kwanza

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978-9987-09-267-3

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 10 Juni, 2021 kuwa Kitabu cha Kiada kwa ajili ya Mwanafunzi wa Kidato cha Kwanza katika ngazi ya Elimu ya Sekondari nchini Tanzania kulingana na Muhtasari wa mwaka 2005.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

Taasisi ya Elimu Tanzania

© Taasisi ya Elimu Tanzania 2021

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kimechapishwa 2021

ISBN: 978 – 9987 – 09 – 267 – 3

Taasisi ya Elimu Tanzania,
S. L. P. 35094,
Dar es Salaam,
Tanzania.

FOR ONLINE USE ONLY

Simu: +255 735 041 168

+255 735 041 170

Baruapepe: director.general@tie.go.tz

Tovuti: www.tie.go.tz

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kukitoa kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

# Yaliyomo

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Orodha ya vielelezo** ..................... v

**Vifupisho** ..................... vi

**Shukurani** ..................... vii

**Dibaji** ..................... viii

**Sura ya Kwanza: Lugha na mawasiliano** ..................... **1**
Dhana ya lugha ..................... 1
Dhana ya mawasiliano ..................... 3
Dhana ya lugha ya Kiswahili ..................... 4
Umuhimu wa kujifunza Kiswahili ..................... 5
Matamshi na lafudhi ya Kiswahili ..................... 8
Zoezi la marudio la 1 ..................... 17

**Sura ya Pili: Aina za maneno** ..................... **19**
Dhana ya aina za maneno ..................... 19
Nomino ..................... 23
Viwakilishi ..................... 24
Vivumishi ..................... 25
Vitenzi ..................... 26
Vielezi ..................... 27
Viunganishi ..................... 28
Vihusishi ..................... 28
Vihisishi ..................... 29
Matumizi ya kamusi ..................... 33
Zoezi la marudio la 2 ..................... 38

**Sura ya Tatu: Fasihi kwa ujumla** ..................... **42**
Fasihi na dhima zake ..................... 42
Aina za fasihi ..................... 44
Tanzu za fasihi simulizi na vipera vyake ..................... 46
Usimulizi wa hadithi ..................... 62
Uhakiki wa kazi za fasihi simulizi ..................... 64
Zoezi la marudio la 3 ..................... 75

FOR ONLINE USE ONLY

**Sura ya Nne: Uandishi wa insha na barua ..................................................... 77**
Kuandika insha za wasifu za kisanaa na zisizo za kisanaa ............................... 77
Kuandika barua ya kirafiki........................................................................... 84
Zoezi la marudio la 4 .................................................................................... 89

**Sura ya Tano: Ufahamu................................................................................. 90**
Dhana ya ufahamu ........................................................................................ 90
Ufahamu wa kuona ........................................................................................ 92
Ufahamu wa kusikiliza .................................................................................. 94
Ufahamu wa kusoma...................................................................................... 97
Kusoma kwa burudani .................................................................................. 104
Ufupisho...................................................................................................... 106
Zoezi la marudio la 5 ................................................................................... 110

**Faharasa..................................................................................................... 114**
**Bibliografia ................................................................................................ 118**

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE
FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 4 05/09/2021 15:40

# Orodha ya Vielelezo

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

1.1: Mfumo wa mawasiliano....................................................................3

1.2: Herufi na matamshi yake ....................................................................14

2.1: Mti unaoonesha aina za maneno....................................................................32

2.2: Mfano wa ufafanuzi wa maneno katika kamusi ......................................35

2.3: Sehemu ya utangulizi wa kamusi....................................................................36

2.4: Sehemu ya mwisho wa kamusi....................................................................37

3.1: Matawi ya sanaa....................................................................43

3.2: Tanzu za fasihi simulizi na vipera vyake ..........................................61

4.1: Anwani ya mwandikiwa mbele ya bahasha ..........................................86

4.2: Anwani ya mwandishi nyuma ya bahasha ..........................................87

FOR ONLINE USE ONLY

# Vifupisho

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| | |
|---|---|
| ATM | Automated Teller Machine |
| BAKITA | Baraza la Kiswahili la Taifa |
| CKD | Chuo Kikuu cha Dar es Salaam |
| DUCE | Dar es Salaam University College of Education |
| DUP | Dar es Salaam University Press |
| E | Kielezi |
| EMS | Express Mail Service |
| Hs | Kihisishi |
| H | Kihusishi |
| N | Nomino |
| NECTA | National Examinations Council of Tanzania |
| n.k. | na kadhalika |
| OUP | Oxford University Press |
| SADC | Southern Africa Development Community |
| SAUT | Saint Augustine University of Tanzania |
| S.L.P. | Sanduku la Posta |
| T | Kitenzi kikuu |
| t | Kitenzi kishirikishi |
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| Ts | Kitenzi kisaidizi |
| U | Kiunganishi |
| UDOM | University of Dodoma |
| V | Kivumishi |
| W | Kiwakilishi |

FOR ONLINE USE ONLY

# Shukurani

FOR ONLINE USE ONLY

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini mchango wa washiriki waliofanikisha uandishi wa kitabu hiki. Pia, TET inatoa shukurani kwa taasisi zote za umma na binafsi zilizoshiriki kwa namna moja ama nyingine katika kufanikisha uandishi wa kitabu hiki. Taasisi hizo ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (CKD), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam - Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (CKD - DUCE), Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Chuo Kishiriki cha Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino (SAUT, Mbeya), Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA), na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA). Pia, TET inatoa shukurani kwa Vyuo vya Ualimu, Shule za Sekondari, na Ofisi za Uthibiti Ubora wa Shule.

Vilevile, TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu wafuatao:

**Waandishi**: Bw. Jivitius C. Sabatho, Bi. Monica W. Manyanga, na Bi. Razia Y. Shemlugu (TET).

**Wahariri**: Prof. David P. B. Massamba (CKD), Dkt. Adventina Y. Buberwa (CKD), Dkt. Faraja J. Mwendamseke (CKD - DUCE), Bw. Saul S. Bichwa (CKD - DUCE), Dkt. Azimio L. Sote (SAUT - MBEYA), Bi. Neema J. Luhwago (UDOM), na Richard P. Mtambi (BAKITA).

**Msanifu**: Bw. Kuyonza K. Kuyonza

**Mpiga picha**: Bw. Chrisant Ignas

**Wachoraji**: Bi. Rehema H. Maganga na Alama Art and Media Production Co. Ltd.

**Mratibu**: Bw. Jivitius C. Sabatho.

Pia, TET inatoa shukurani kwa walimu na wanafunzi wa shule za sekondari walioshiriki katika hatua ya ujaribishaji wa muswada wa kitabu hiki. Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha zoezi la uandishi na uchapaji wa kitabu hiki.

..................................

**Dkt. Aneth A. Komba**
**Mkurugenzi Mkuu**
**Taasisi ya Elimu Tanzania**

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 7 05/09/2021 15:40

# Dibaji

FOR ONLINE USE ONLY

Kitabu hiki ni cha Kwanza katika mfululizo wa vitabu vinne vya Somo la Kiswahili kuanzia Kidato cha Kwanza hadi cha Nne, kilichoandaliwa mahususi kwako mwanafunzi wa Kidato cha Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kitabu hiki kimeandaliwa kulingana na Muhtasari wa Somo la Kiswahili wa mwaka 2005 uliotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Kitabu kimegawanywa katika sura tano: Lugha na mawasiliano, Aina za maneno, Fasihi kwa ujumla, Uandishi wa insha na barua, na Ufahamu. Maudhui ya kitabu hiki yamewasilishwa kwa njia ya matini, kazi za kufanya, vielelezo, pamoja na picha ambazo zote zinachochea ujenzi wa umahiri unaokusudiwa kwa kila sura. Vilevile, katika kila sura kuna mazoezi yenye lengo la kupima na kujenga uelewa pamoja na ujuzi katika somo hili. Hivyo basi, unapaswa kufanya mazoezi na kazi zote zilizopo kwenye kitabu hiki pamoja na kazi nyingine utakazopewa na mwalimu.

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 8 05/09/2021 15:40

# Sura ya Kwanza

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Lugha na mawasiliano

### Utangulizi

*Lugha ni chombo kikuu cha mawasiliano ya binadamu. Katika sura hii, utajifunza dhana na umuhimu wa lugha ya Kiswahili. Vilevile, utajifunza namna ya kuwasiliana kwa kutumia lugha fasaha na kutofautisha lugha fasaha na isiyo fasaha katika mazungumzo na maandishi. Utasoma matini za Kiswahili kwa kuzingatia matamshi, lafudhi, mkazo, na kiimbo sahihi. Pia, utafanya uchanganuzi wa vipengele vya sarufi ya Kiswahili kwa kuzingatia ufasaha wa lugha. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kuwasiliana kwa Kiswahili fasaha katika miktadha mbalimbali.*

### Dhana ya lugha

**Kazi ya 1.1**

*Soma shairi lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Nataka nena na wewe, upate kunielewa,
Wengi washikwa kiwewe, kwa kushindwa nielewa,
Yapaswa unielewe, nimekwishakubaliwa,
Sauti zangu nasibu, hakuna wa kukanusha.

Huwezi kuwazuia, waliokubaliana,
Mimi wananitumia, wapate kuelewana,
Kanuni wazingatia, ili kuwasiliana,
Sauti zangu nasibu, hakuna wa kukanusha.

Mfumo wangu makini, sauti kupangilia,
Maneno kuyatumia, yenye mpango sawia,
Sentensi kuzitumia, mawazo kupangilia,
Sauti zangu nasibu, hakuna wa kukanusha.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 1 05/09/2021 15:40

## Maswali

1. Mwandishi anazungumzia nini katika shairi ulilosoma?
2. Ni nani waliokubaliana kuwasiliana kwa kutumia hicho alichokizungumzia mwandishi katika ubeti wa pili wa shairi?
3. Ni mambo gani matatu yaliyojumuishwa na mwandishi katika mfumo wa jambo alilozungumzia?
4. Unafikiri kwa nini mstari wa mwisho wa kila ubeti umerudiwarudiwa na mwandishi katika shairi hilo?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Kazi ya 1.2

*Maneno yafuatayo yameandikwa kwa kuchanganya herufi. Chunguza maneno hayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

1. luagh
2. anomasiwali
3. unabidam
4. ribaha

## Maswali

1. Je, maneno hayo yana makosa gani?
2. Kuna changamoto gani katika kusoma maneno hayo?
3. Nini kifanyike ili maneno hayo yaweze kusomeka vizuri na kuleta maana?
4. Andika maneno hayo kwa usahihi.
5. Kutokana na uelewa ulioupata, lugha hufasiliwaje?

**Zingatia**

Lugha ni mfumo wa sauti za nasibu ambazo zimebuniwa na kukubaliwa na jamii ya watu ili zitumike katika mawasiliano baina yao. Mfumo huo hujumuisha sauti, silabi, neno, na sentensi. Ili watu au jamii iweze kuwasiliana, sharti lugha inayotumika iwe inaeleweka vizuri kwa kuwa lugha ni chombo cha mawasiliano. Unapowasiliana kwa kutumia lugha ya Kiswahili ni muhimu kuzingatia kiimbo, mkazo, matamshi na lafudhi sahihi.

FOR ONLINE USE ONLY




KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 2 05/09/2021 15:40

## Dhana ya mawasiliano

### Kazi ya 1.3

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Chunguza kielelezo cha mfumo wa mawasiliano, kisha jibu maswali yanayofuata.*




**Kielelezo namba 1.1**: *Mfumo wa mawasiliano*

## Maswali

1. Kwa kutumia kielelezo cha mfumo wa mawasiliano, bainisha njia kuu mbili za mawasiliano unazoweza kutumia unapowasiliana kwa kutumia lugha.
2. Njia ulizozibainisha katika swali la 1 zinaweza kutumia vifaa gani vya mawasiliano kati ya vifaa vilivyobainishwa katika kipengele cha 3 katika kielelezo ulichopewa?
3. Bainisha vifaa vingine vya mawasiliano unavyoweza kutumia katika kuwasiliana.
4. Kwa kutumia kielelezo ulichopewa, eleza jinsi mchakato wa mawasiliano unavyofanyika.
5. Unafikiri ni mambo gani yanaweza kukwamisha mawasiliano unapotumia lugha?

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 3 05/09/2021 15:40

**Zingatia**

Mawasiliano ni upashanaji habari au taarifa kwa njia mbalimbali. Mawasiliano hukamilika iwapo tu taarifa inayotolewa inaleta maana iliyokusudiwa. Binadamu huwasiliana kwa kutumia lugha. Dhima kuu ya lugha ni kupashana habari. Katika mawasiliano lugha inaweza kuleta athari ama chanya au hasi. Lugha inaweza kumtambulisha mtumiaji wa lugha inayohusika, utamaduni wake na kubainisha hisia alizonazo. Pia, kwa kutumia lugha, mtu au jamii hupata maarifa kuhusu mambo mbalimbali. Maarifa hayo hupatikana ama kupitia lugha ya mazungumzo au lugha ya maandishi. Pamoja na hayo, lugha ikitumika vibaya, inaweza kukwamisha mawasiliano au kuleta mgongano kwa watumiaji wake. Ili mawasiliano yafanyike kwa ufanisi ni lazima pawe na mtoa ujumbe, ujumbe wenyewe, midia ambayo hubeba ujumbe, na mpokeaji wa ujumbe unaohusika. Aidha, ili mawasiliano yaweze kukamilika, sharti mpokeaji wa ujumbe atoe mrejesho kwa mtoa ujumbe.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Dhana ya lugha ya Kiswahili

### Kazi ya 1.4

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Kiswahili ni lugha ya Kibantu inayozungumzwa kama lugha mama au lugha ya pili katika ukanda wa pwani ya Mashariki mwa Afrika. Pia, huzungumzwa kama lugha ya pili maeneo mengine ya Afrika Mashariki. "Kibantu" ni jina jumuishi linalotumika kutaja lugha zote zinazotumia maneno yanayoishia na –tu (au –ntu, -nt$^{h}$u, -nu, n.k) kurejelea mtu au watu. Kwa hiyo, hakuna lugha maalumu ijulikanayo kama Kibantu. Watu wanaozungumza Kiswahili kama lugha mama hujulikana kama Waswahili. Hata hivyo, jina hili linarejelea lugha yao tu na siyo kabila kwani hakuna kabila la Kiswahili wala Waswahili. Kiswahili kinatumika Tanzania na Kenya kama lugha ya Taifa.

Nchini Tanzania, Kiswahili hutumika pia kama lugha ya kufundishia elimu ya msingi na vyuo vya ualimu elimu ya msingi. Aidha, lugha hii hufundishwa kama somo kuanzia ngazi ya sekondari hadi elimu ya juu. Kwa upande wa Kenya na Uganda, Kiswahili ni lugha ya pili sanjari na Kiingereza. Nchini Kongo (Kinshasa), Kiswahili ni mojawapo ya lugha nne za utawala, lugha kuu ikiwa Kifaransa.

Pamoja na kwamba Kiswahili ni lugha ya Kibantu, baadhi ya maneno katika lugha hii yamekopwa kutoka katika lugha mbalimbali kama vile, Kiarabu,

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 4 05/09/2021 15:40

Kireno na Kiingereza. Inasemekana kwamba kuna lahaja kuu 15 za Kiswahili zinazotumika ingawa tafiti bado zinaendelea. Kwa upande wa Afrika Mashariki, lahaja zinazojulikana sana ni Kiunguja (kinachozungumzwa katika Kisiwa cha Unguja) ambacho ndicho kilisanifishwa na kuwa Kiswahili Sanifu; Kipemba (kinachozungumzwa katika Kisiwa cha Pemba); Kitumbatu (kinachozungumzwa katika Kisiwa cha Tumbatu); Kimvita (kinachozungumzwa Mombasa); na Kiamu (kinachozungumzwa katika Kisiwa cha Lamu huko Kenya). Pamoja na lahaja zote hizo, Kiswahili Sanifu ndicho hufundishwa shuleni.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maswali

1. Kwa nini Kiswahili kinazungumzwa kama lugha ya pili katika ukanda wa pwani ya Mashariki mwa Afrika?
2. Unaelewa nini kuhusu lugha mama?
3. Mwandishi ana maana gani anaposema, "... hakuna lugha maalumu inayojulikana kama Kibantu?"
4. Ni nchi zipi zinatumia Kiswahili kama lugha ya taifa?
5. Je, ungepewa nafasi ya kupendekeza kuwa Kiswahili kitumike au kisitumike kama lugha ya kufundishia masomo ya ngazi ya sekondari hadi elimu ya juu ungependekeza nini na kwa sababu gani?

### Kazi ya 1.5

Chunguza maneno ya Kiswahili, kisha andika maneno kumi (10) ambayo yamekopwa kutoka katika lugha mbalimbali.

## Umuhimu wa kujifunza Kiswahili

### Kazi ya 1.6

*Soma sehemu ya mahojiano baina ya **Mwandishi wa habari** na **Mwalimu**, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Mwandishi**: Baadhi ya watu hawaoni umuhimu wa kujifunza Kiswahili. Wewe una maoni gani?

**Mwalimu**: Kwa kweli, hayo ni mawazo potofu. Tuelewe kuwa lugha ya Kiswahili nchini Tanzania hutumika kufundishia masomo yote katika shule za msingi na vyuo vya ualimu elimu ya msingi vinavyotumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia. Hii inawasaidia wanafunzi wengi kuelewa masomo hayo kwa urahisi kwa kuwa wanafundishwa kwa lugha wanayoifahamu zaidi.

FOR ONLINE USE ONLY

Pia, Kiswahili hufundishwa kama somo katika elimu ya sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Mwandishi**: Sawa. Je, kuna mahali kwingine ambako Kiswahili kinafundishwa?

**Mwalimu**: Ndiyo. Kiswahili kinafundishwa katika shule na vyuo vikuu vya nchi zingine za Afrika, na hata katika baadhi ya vyuo vikuu vya nchi mbalimbali za nje ya Afrika kama vile, Marekani, Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, China, Japani, na kadhalika.

**Mwandishi**: Mbali na umuhimu huo, kuna umuhimu mwingine?

**Mwalimu**: Ndiyo. Lugha ya Kiswahili inatumika kuwaunganisha Watanzania wote. Tanzania inakadiriwa kuwa na watu zaidi ya milioni hamsini wenye makabila tofauti lakini wanaunganishwa na lugha ya Kiswahili kwa mawasiliano. Aidha, Kiswahili kinachangia katika kukuza uchumi, amani, na utulivu nchini na katika nchi jirani. Isitoshe, wakati wa kupigania uhuru, lugha ya Kiswahili ilitumika kama chombo muhimu cha umoja wa kimawasiliano.

**Mwandishi**: Kwa kweli, unanikumbusha mbali mwalimu. Naomba uendelee kunieleza zaidi.

**Mwalimu**: Lugha ya Kiswahili ni lugha rasmi. Inatumika katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na kiserikali kama vile katika mahakama, bunge na elimu. Vilevile, Kiswahili kama lugha ya taifa hutumika kama utambulisho wa taifa. Kwa hiyo, Kiswahili kina nafasi kubwa katika nyanja zote za maendeleo ya taifa.

**Mwandishi**: Kiswahili kina hadhi gani kimataifa?

**Mwalimu**: Kiswahili kimepata hadhi ya kutumika kimataifa. Hii ndiyo lugha pekee ya Kiafrika ambayo imesambaa zaidi kuliko lugha zingine. Hivyo, imefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika kuleta umoja barani Afrika. Ikumbukwe kwamba, Kiswahili ndiyo lugha pekee ya Kiafrika iliyopendekezwa kutumika pia katika vikao vya Umoja wa Afrika sanjari na lugha zingine. Aidha, Kiswahili kinatumika kama lugha rasmi katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

FOR ONLINE USE ONLY

**Mwandishi**: Ni fursa zipi ambazo Watanzania wanafaidika nazo kutokana na kupanda hadhi kwa lugha ya Kiswahili?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Mwalimu**: Kiswahili hutoa fursa za ajira. Kwa mfano, baadhi ya Watanzania wenye taaluma ya kufundisha Kiswahili hujipatia fedha kutokana na kufundisha Kiswahili. Vilevile, kutokana na umuhimu wa Kiswahili kutumika nje ya nchi, baadhi ya nchi kama vile Afrika Kusini zimekuwa zikihitaji wataalamu wa Kiswahili kwenda kukifundisha katika nchi hizo.

**Mwandishi**: Sasa turudi kwa wanafunzi. Je, wanafunzi wanapojifunza somo la Kiswahili katika elimu ya sekondari wanapata manufaa gani?

**Mwalimu**: Mwanafunzi akijifunza kikamilifu somo la Kiswahili katika elimu ya sekondari, ataweza kuwasiliana kwa Kiswahili fasaha katika nyanja mbalimbali za maisha, na kukithamini Kiswahili kama sehemu muhimu ya utamaduni wa Mtanzania. Vilevile, husaidia kujenga tabia ya udadisi na ubunifu katika masuala ya lugha na fasihi ya Kiswahili, kuelewa, kuthamini na kutumia kazi za fasihi katika maisha. Aidha, ataweza kutumia lugha hii katika miktadha mbalimbali; kukuza na kukieneza Kiswahili ili kiweze kutumika katika mawasiliano kitaifa na kimataifa, na kujenga uwezo wa kujisomea maandiko mbalimbali ya Kiswahili. Pia, atapata msingi bora na imara wa kujifunza na kujiendeleza katika taaluma za Kiswahili na kukitumia kupata maarifa, mwelekeo, na stadi za kijamii, kitamaduni, kiteknolojia, na kitaaluma.

**Mwandishi**: Mwalimu, ninakupa nafasi ya kumalizia suala hili la umuhimu kama una lolote la kuongezea ili tuingie kwenye kipengele kingine.

**Mwalimu**: Ndugu mwandishi, ninapenda kumalizia kwa kueleza kwamba lugha ya Kiswahili, kama zilivyo lugha zingine, inaweza kutumika kutolea maarifa na ujuzi wa taaluma mbalimbali kama vile habari na mawasiliano, historia, na sayansi na teknolojia.

**Mwandishi**: Asante sana mwalimu kwa maelezo yako ya kina kuhusu umuhimu wa kujifunza Kiswahili.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 7 05/09/2021 15:40

**Mwalimu:** Asante na karibu tena.

**Mwandishi:** Shukurani.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maswali

1. Kuna faida gani ya kutumia Kiswahili kufundishia masomo yote ya elimu ya msingi?
2. Fafanua, kwa kutoa mifano, umuhimu wa kujifunza Kiswahili.
3. Mwanafunzi akijifunza kikamilifu somo la Kiswahili katika elimu ya sekondari atapata faida gani?
4. Kwa nini mwandishi alimshukuru mwalimu?
5. Eleza faida na changamoto za kutumia Kiswahili kama lugha ya kujifunzia na kufundishia masomo yote katika ngazi ya sekondari.

### Matamshi na lafudhi ya Kiswahili

**Kazi ya 1.7**

*Soma kisa kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Zukwe ni kijana aliyeishi katika Kijiji cha Misike kilichoko katika Wilaya ya Nduna mkoani Shobo. Kijana huyo alipenda sana kushiriki mazungumzo na vijana wenzake yaliyokuwa yakifanyika kijiweni wakati wa jioni baada ya kazi. Kijiwe hicho kiliitwa Bunguabongo kwa sababu vijana wengi waliopendelea kwenda mahali pale walikuwa wakiibua mazungumzo yaliyokuza fikra na kuwafanya wapate mwelekeo sahihi wa maisha.

Siku moja Zukwe baada ya shughuli zake za ufugaji, alitembelea kijiweni kama ilivyokuwa ada yake. Alikwenda mahali pale kwa ajili ya kubadilishana mawazo na wenzake. Alipofika, aliwakuta vijana wenzake wakijadiliana kuhusu suala la ajira kwa vijana. Kwa kuwa Zukwe alikuwa anapenda sana mijadala, alisogea karibu na kuanza kusikiliza kwa makini ili aweze kuchangia mada.
Mazungumzo yao yalikuwa hivi:

**Tongoa**: Mimi ninaona ajira ziko za aina nyingi tu ila baadhi ya vijana wenzetu hawapendi kujituma; au unasemaje Benjo?

**Benjo**: Kweli bwana! Kwa mfano, mimi nimeamua kufuga kuku. Wakati ninaanza shughuli hii, vijana wengi mlinidhihaki. Sasa ninaona mnanimezea mate kwa jinsi ninavyopata pesa kutokana na kuuza mayai, kuku, na mbolea inayotokana na kuku. Zukwe, si ndiyo?

FOR ONLINE USE ONLY

**Zukwe**: Haswaaa! Mimi pia nilikuwa kama wewe. *Ntoto* wa ndugu yangu alinicheka sana na *kunizarau* nilipoanza kufuga mbuzi. Alisema nimekosa kazi ya kufanya. Benjo, fikiria *ntoto* kama yule ananicheka mimi. Ni *zarau* sana; ingawa sasa ninawauzia mbuzi wa nyama wafanyabiashara wa hapa kijijini na mjini.

**Shehena**: Mmmh! Zukwe, umesema *ntoto*! Ni nani huyo? Nani anaitwa *ntoto* hapa kijijini? Pia, umesema *zarau.* Mimi sikuelewi bwana.

**Chachu**: Shehena vipi? *Ntoto* si jina la mtu wa hapa kijijini bwana. Zukwe anamaanisha *mtoto* wa ndugu yake. Eti jamani .... si ndivyo? (*Wote wanacheka*).

**Funko**: Ndivyo ilivyo Chachu. Sasa tuendelee na mazungumzo yetu. Mimi ninafikiri ajira ni tatizo. Hata wenzetu waliosoma *wanakwendaga* mjini wanapata kazi lakini siku hizi wengi wanabaki hapahapa kijijini. Pia, hapa kijijini *ninawaonapo* watu wengi wanakaa tu. Ndugu zangu ajira hakuna kabisa.

**Ajala**: Funko! *Wanakwendaga* ... *ninawaonapo* ...! Sema vizuri bwana. Mimi ninakubaliana na Benjo na Zukwe. Kazi za kufanya zipo nyingi. Vijana wengi tunapenda kazi za ofisini hata kama hatuna ujuzi nazo. Mtu anaweza kuajiriwa au kujiajiri kama walivyofanya wenzetu Zukwe na Benjo. Si lazima kufuga kuku kwani unaweza kujishughulisha na kilimo au biashara. Shughuli zote hizi zinaweza kutuletea maendeleo. Tufanye kazi bwana! Bila kufanya kazi maisha ni magumu kweli.

**Shaburi**: Kwa *kweri* nimejifunza jambo hapa. *Kurara badara* ya kutafuta kazi ya kufanya kunasababisha maisha kuwa magumu. Ama *kweri erimu* haina mwisho. Mazungumzo haya yamenifungua macho kabisa. Kumbe! Ninaweza kufuga, *kurima* au kufanya biashara nikapata kipato *badara* ya *kuenderea* kuwategemea wazazi wangu. Nadhani ningekuwa *mbari* kama ningeanzisha *kirimo* cha mbogamboga. Nani yuko tayari, tuanzishe *kirimo* cha mbogamboga.

**Egeli**: Haaaa! Shaburi, unauliza au unaeleza? Umesahau tulivyofundishwa shule ya msingi? Kwenye swali sharti uweke kiulizo bwana.

**Shaburi**: Tatizo *rako* wewe ni mikwara tu. Kwani *hujanierewa*?

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 9 05/09/2021 15:40

**Egeli**: Sema vizuri ueleweke. Mbogamboga zinalipa kweli? Sidhani. Fanya biashara ya duka Shaburi.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Shaburi**: Tatizo *rako Egeri* hufikirii *mbari* na hupendi *kujishughurisha* kama mimi. Mbogamboga *zitaturipa* sana, hasa *tukirima* wenyewe. Hapa kijijini maduka ni mengi tu. Tufikirie *shughuri* tofauti na hiyo; au mnasemaje jamani?

**Zukwe, Tongoa na Benjo**: Kweli bwana.

**Zukwe**: Mimi ninaweza kushirikiana na mtu yeyote anayetaka kufuga mbuzi wa nyama. Tunaweza kuwa na mradi mkubwa tukasambaza nyama katika masoko mbalimbali na kujipatia fedha. Jamani, naona Dageta hafurahishwi na mazungumzo yetu. Vipi Dageta una neno?

**Dageta**: *Nimekasirika* kwa sababu nimepata ujumbe wa simu wenye *taharifa* mbaya kutoka kwa mjomba kwamba bibi aliyemzaa mama amelazwa hospitalini.

**Zukwe**: Dageta, pole sana. Ina maana umekasirika kwa sababu hiyo? Kwa nini ukasirike kama bibi yako amelazwa?

**Dageta**: Du! Nimepitiwa jamani. Mnajua bibi amenilea tangu nikiwa mdogo. Sijakasirika bwana.

**Chachu**: Kwa hiyo, Dageta "amehuzunika." Sidhani kama unaweza kukasirika kwa sababu ya ugonjwa. Dageta, pole sana rafiki yangu.

**Dageta**: Asanteni.

**Zukwe**: Mazungumzo yetu yalikuwa matamu kweli lakini giza limeingia. Kila lenye mwanzo halikosi kuwa na mwisho. Kikubwa hapa ni kufanya kazi kwa bidii ndugu zangu. Tumsindikize rafiki yetu Dageta kwenda hospitalini. Mnaonaje?

**Wote**: Sawa. *(Wakaondoka na kwenda hospitalini.)*

Wakiwa njiani kuelekea hospitalini, Zukwe aliendelea kutafakari maarifa aliyoyapata kupitia mazungumzo yao. Alidhamiria kuboresha biashara yake ya mbuzi wa nyama na kuongeza mradi wa kilimo cha mbogamboga ili kujiongezea kipato. Kutokana na mazungumzo yale, Zukwe alipata hamasa ya kufanya kazi kwa bidii zaidi.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 10 05/09/2021 15:40

## Maswali

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

1. Kwa kuzingatia kisa ulichosoma, kuwasiliana ni kufanya nini?
2. Katika kisa ulichosoma, lugha ina dhima gani?
3. Bainisha sentensi ambazo zimetumia lugha isiyo fasaha katika kisa ulichosoma.
4. Unafikiri kwa nini lugha hiyo siyo fasaha?
5. Andika kwa ufasaha sentensi ulizozibainisha katika swali la 3.
6. Kwa kuzingatia mjadala wa Zukwe na wenzake, wewe una maoni gani kuhusu mazungumzo yao?
7. Kipi kinafaa kuwa kichwa cha habari cha kisa ulichosoma?

## Zoezi la 1.1

1. Kwa kuzingatia lafudhi na matamshi sahihi, bainisha maneno yenye makosa katika sentensi zifuatazo:
   (a) Hata wenzetu waliosoma wanakwendaga mjini.
   (b) Nimepata ujumbe wa simu wenye taharifa mbaya.
   (c) Kurara badara ya kutafuta kazi ya kufanya kunasababisha maisha kuwa magumu.
   (d) Ama kweri erimu haina mwisho.
   (e) Rafiki yangu naja.
   (f) Ntoto wangu aumwa.
2. Andika upya sentensi hizo kwa kusahihisha makosa uliyoyabaini.
3. Andika sentensi tano zenye makosa ya kisarufi yanayotokana na athari za lugha mama au mazingira.

**Zingatia**
Lafudhi ni jinsi mtu anavyotamka maneno. Aidha, lafudhi humpa mzungumzaji utambulisho ama wa jamii au eneo analotoka. Lafudhi ya mtu hutokana na athari za lugha mama, au eneo la kijiografia analotoka.

FOR ONLINE USE ONLY

## Kazi ya 1.8

1. Chunguza kwa makini mazungumzo kati ya Zukwe na wenzake, kisha bainisha maneno mengine yenye makosa na uyaandike kwa usahihi.
2. Kwa nini Shaburi ametumia maneno kweri, erimu, kurara, badara, na kirimo kwenye mazungumzo yake?

**Zingatia**

Matamshi ni jinsi ya kutamka maneno katika lugha yoyote ile. Matamshi sahihi ni utamkaji wa maneno kwa kuzingatia kanuni za sarufi ya lugha inayohusika. Mzungumzaji akikosea kutamka neno humfanya msikilizaji asimwelewe kabisa au aelewe tofauti na alichokikusudia mzungumzaji. Kwa mfano, mtu akitamka *kura* badala ya *kula* atawasilisha maana tofauti na iliyotegemewa; hivyo, hukwamisha mawasiliano.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Kazi ya 1.9

*Chunguza sentensi zifuatazo, kisha bainisha tofauti zake.*

1. Baraka analima.
2. Baraka analima?
3. Baraka analima!
4. Baraka, lima.

**Zingatia**

Kila lugha ina utaratibu wake maalumu wa upandaji na ushukaji wa mawimbi ya sauti wakati wa kuzungumza. Utaratibu huo huitwa kiimbo. Matumizi ya kiimbo yanasaidia kubainisha lengo la mzungumzaji; kwa mfano, kuuliza swali, kutoa maelezo, kutoa amri, au kushangaa.

### Kazi ya 1.10

*Tenganisha silabi za maneno yafuatayo:*

1. Shusha
2. Ua
3. Pua
4. Gharama
5. Mpiganaji
6. Vilevile
7. Shangwe
8. Sikukuu
9. Kinanda
10. Kiswahili

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 12 05/09/2021 15:40

**Zingatia**

Silabi ni sehemu ya neno inayoundwa na konsonanti na irabu au irabu peke yake na hutamkwa kwa pamoja na mara moja kama fungu moja la sauti. Lugha ya Kiswahili hutamkwa kwa utaratibu wa kufuata silabi. Kwa mfano, neno *baba* limeundwa na silabi mbili ambazo ni $**ba**$ $**ba**$. Muundo wa silabi za Kiswahili unajibainisha katika miundo ifuatayo:

(i) Irabu pekee: Kwa mfano, silabi $**u**$ na $**a**$ katika neno *ua;*

(ii) Konsonanti moja na irabu moja: Kwa mfano, silabi $**la**$ na $**la**$ katika neno *lala;*

(iii) Konsonanti mbili au zaidi na irabu moja: Kwa mfano, silabi $**mba**$ katika neno *shamba*;

(iv) Konsonanti moja, kiyeyusho kimoja na irabu moja: Kwa mfano, silabi $**pya**$ katika neno *jipya*; na

(v) Konsonanti mbili, kiyeyusho kimoja na irabu moja: Kwa mfano, silabi $**mbwa**$ katika neno *pambwa*.

Irabu za Kiswahili ni **a**, **e**, **i**, **o**, na **u**. Konsonanti za Kiswahili ni **b**, **ch**, **d**, **dh**, **f**, **g**, **gh**, **h**, **j**, **k**, **l**, **m**, **n**, **ng'**, **ny**, **p**, **r**, **s**, **sh**, **t**, **th**, **v**, na **z**. Viyeyusho katika lugha ya Kiswahili ni **w** na **y**.

Silabi au mkusanyiko wa silabi unaotamkwa na kuleta maana fulani huitwa neno. Hata hivyo, silabi kama vile, $**na**$, $**kwa**$, na $**la**$ huweza kuwa neno pale ambapo zitatumika katika tungo. Aidha, neno au kifungu cha maneno kinachotoa taarifa kamili huitwa sentensi.

## Kazi ya 1.11

*Tamka kwa ufasaha maneno yafuatayo:*

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Muungano | 2. | Koo | 3. | Washirikishe | 4. | Bidhaa |
| 5. | Thamani | 6. | Shughuli | 7. | Ng´ombe | 8. | Nyanya |
| 9. | Ramani | 10. | Picha | | | | |

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE
FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 13 05/09/2021 15:40

**Zingatia**

Herufi za Kiswahili hutamkwa kwa kuhusisha herufi husika na irabu /**e**/ ambayo hupachikwa mbele ya herufi hiyo. Hata hivyo, herufi ambayo ni irabu hutamkwa kama inavyoandikwa. Rejea kielelezo namba 1.2 kinachoonesha herufi za Kiswahili na matamshi yake. Silabi za Kiswahili hutamkwa kutegemeana na irabu iliyopachikwa mbele ya konsonanti inayohusika; kwa mfano, $**ba**$, $**be**$, $**bi**$, $**bo**$, na $**bu**$.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| Herufi za alfabeti | Matamshi ya herufi |
|---|---|
| a | a |
| b | be |
| ch | che |
| d | de |
| dh | dhe |
| e | e |
| f | fe |
| g | ge |
| gh | ghe |
| h | he |
| i | i |
| j | je |
| k | ke |
| l | le |
| m | me |
| n | ne |
| ny | nye |
| ng’ | ng'e |
| o | o |
| p | pe |
| r | re |
| s | se |
| sh | she |
| t | te |
| th | the |
| u | u |
| v | ve |
| w | we |
| y | ye |
| z | ze |

**Kielelezo namba 1.2:** *Herufi na matamshi yake*

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 14 05/09/2021 15:40

### Kazi ya 1.12

Soma tena kisa chenye mazungumzo kati ya Zukwe na wenzake kwa kuzingatia usahihi wa matamshi, mkazo, kiimbo, na lafudhi sahihi ya Kiswahili.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zingatia**

Sauti ni sehemu ndogo sana ya neno ambayo haiwezi kugawanyika zaidi. Kwa maneno mengine, sauti ni vitamkwa vinavyotamkwa na binadamu kwa kutumia ala za sauti ambazo ni mapafu, koo, midomo, ulimi, ufizi, meno, na kadhalika. Sauti zimegawanyika katika aina mbili ambazo ni irabu na konsonanti. Irabu ni aina ya sauti za lugha ambazo hutamkwa bila kuzuia mkondohewa ilhali konsonanti ni sauti ambazo hutamkwa kwa kuandamana na mzuio wa mkondohewa. Lugha ni chombo cha mawasiliano. Ili mawasiliano yafanikiwe, inabidi lugha iwe fasaha. Hivyo, ni lazima kuepuka makosa mbalimbali ya kimatamshi katika mawasiliano. Makosa ya kimatamshi hujitokeza watu wanapozungumza kwa kushindwa kutamka baadhi ya sauti katika lugha kutokana na athari za lugha mama au mazingira aliyomo mzungumzaji; na hivyo, kukwamisha mawasiliano. Hali hii inaweza kupotosha maana. Aidha, ni vyema kuelewa kuwa kuna matamshi ya herufi za alfabeti ambazo huwakilisha pia sauti, hususani irabu. Aghalabu, katika Kiswahili sauti huandikwa kama zinavyotamkwa. Hata hivyo, kuna sauti chache ambazo herufi zake hutokana na muungano wa herufi mbili lakini ni sauti moja; kwa mfano, **th**, **dh**, **ch**, **ng'**, **ny**, **sh**, na **gh** katika maneno kama thamani, dhahabu, chai, ng'ombe, nyanya, shamba, ghadhabu, n.k.

### Kazi ya 1.13

Orodhesha makosa mbalimbali yasiyopungua sita (6) yanayofanywa na wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili, kisha rekebisha makosa hayo.

### Kazi ya 1.14

Fuatilia taarifa ya habari kwa njia ya redio au televisheni kwa lengo la kubainisha makosa ya kimatamshi yanayojitokeza, kisha andika maneno hayo kwa matamshi sahihi.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 15 05/09/2021 15:40

## Zoezi la 1.2

*Andika sentensi zifuatazo kwa usahihi.*

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

1. Zana ya neno ni mkusanyiko wa silabi wenye kuleta maana.
2. Alishiriki mazungumzo na wenzake aliyokuwa wakiyafanya kijiweni.
3. Nyumba na banda la kuku imebomolewa.
4. Baba alimkuta mama ameondoka.
5. Embe limeanguka kutoka juu ya mti.

## Zoezi la 1.3

*Chunguza sentensi zifuatazo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

1. Kaka alimpigia mpira mtoto wa jirani yetu.
2. Fatuma amechana kitabu cha rafiki yake Rose.
3. Binamu amenunua kanga.

## Maswali

1. Sentensi ulizopewa zina maana zaidi ya moja. Eleza maana za sentensi hizo.
2. Unafikiri sentensi zenye maana zaidi ya moja zinawezaje kuathiri mawasiliano?
3. Nini kifanyike ili kuondoa utata katika sentensi hizo?

**Zingatia**

Kwa ujumla, lugha imegawanyika katika tanzu kuu mbili ambazo ni lugha ya mazungumzo na lugha ya maandishi. Lugha ya mazungumzo huwasilishwa kwa mdomo ambapo chanzo ni mzungumzaji na kikomo ni msikilizaji. Lugha ya maandishi huwasilishwa kwa maandishi ambapo chanzo ni mwandishi na kikomo ni msomaji. Mzungumzaji au mwandishi anapaswa kuwa makini ili kuwezesha mawasiliano. Usahihi wa maandishi au mazungumzo hutawaliwa na sarufi ya lugha inayohusika. Sarufi imegawanywa katika matawi makuu manne ambayo ni sarufi matamshi (fonolojia), sarufi maumbo (mofolojia), sarufi miundo (sintaksia) na sarufi maana (semantiki). Sarufi matamshi inashughulika na utamkaji wa sauti za lugha inayohusika ilhali sarufi maumbo inashughulika na maumbo ya maneno. Aidha, sarufi miundo inashughulika na mpangilio wa maneno katika sentensi wakati sarufi maana inashughulika na maana za maneno na sentensi.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 16 05/09/2021 15:40

## Zoezi la marudio la 1

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

1. Chagua jibu sahihi katika maswali yafuatayo:
   (i) Dhima kuu ya lugha katika mawasiliano ni ipi kati ya hizi zifuatazo?
      (a) Kutambulisha utamaduni
      (b) Kutunza historia
      (c) Kupashana habari
      (d) Kuelimisha jamii
      (e) Kuburudisha jamii

   (ii) Kiimbo hufasiliwaje katika mazungumzo?
      (a) Kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti.
      (b) Kuzungumza na kuongea kwa sauti.
      (c) Kuzungumza kwa kupandisha mawimbi ya sauti.
      (d) Kuzungumza kwa kushusha mawimbi ya sauti.
      (e) Kuzungumza na kushuka kwa mawimbi ya sauti.

   (iii) Sentensi ipi kati ya hizi zifuatazo **haina** maana zaidi ya moja?
      (a) Kaka amefua nguo.
      (b) Nipe sahani ya kulia.
      (c) Suedi amenunua mbuzi.
      (d) Eva amenunua kanga.
      (e) Joni amempigia mpira.

   (iv) Dhana ipi kati ya zifuatazo huonesha utambulisho wa mzungumzaji?
      (a) Matamshi
      (b) Sauti
      (c) Silabi
      (d) Mkazo
      (e) Lafudhi

   (v) Neno **shurutishwa** limeundwa na silabi ngapi?
      (a) Tano
      (b) Nne
      (c) Tatu
      (d) Sita
      (e) Kumi

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 17 05/09/2021 15:40

2. Oanisha maana ya dhana katika orodha **A** na dhana zinazohusika kutoka orodha **B** kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| Orodha A | Orodha B |
|---|---|
| (i) Sehemu ya neno inayotamkwa mara moja na kwa pamoja kama fungu moja la sauti. | A. Lafudhi |
| | B. Matamshi |
| (ii) Utamkaji wa maneno unaozingatia kanuni za sarufi ya lugha. | C. Kiimbo |
| | D. Mkazo |
| (iii) Nguvu inayotumika kutamka sehemu fulani ya neno. | E. Silabi |
| (iv) Vitamkwa vinavyotamkwa na binadamu kwa kutumia viungo sauti. | F. Lugha |
| | G. Sauti |
| (v) Jinsi mtu anavyotamka maneno ya lugha. | |

3. Bainisha maneno yenye makosa katika sentensi zifuatazo kwa kuyapigia mstari, kisha andika sentensi hizo kwa usahihi.
   (a) Mwanafunzi ayejitambua hawapendagi mzaha katika masomo.
   (b) Shule yetu ina vifaa vya samani.
   (c) Napenda kuchukua nafasi hii kuwajulisha kuwa wagonjwa wote wamepona.
   (d) Mti uliokuwa karibu na bustani ya maua umedondoka.
   (e) Mzee Kiza amedhuru mbuga za wanyama.

4. Matumizi ya kiimbo husaidia kubainisha lengo la mzungumzaji. Fafanua malengo ya mzungumzaji katika sentensi zifuatazo:
   (a) Mwanafunzi anasoma kwa bidii.
   (b) Mwanafunzi, soma kwa bidii.
   (c) Mwanafunzi anasoma kwa bidii?
   (d) Mwanafunzi anasoma kwa bidii!

5. Eleza maana ya msamiati ufuatao, kisha tunga sentensi moja kwa kila msamiati.
   (a) baruapepe
   (b) mitandao ya jamii
   (c) tovuti
   (d) faksi
   (e) mawasiliano

FOR ONLINE USE ONLY

# Sura ya Pili

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Aina za maneno

**Utangulizi**

*Maneno hupangwa katika makundi mbalimbali. Makundi hayo ndiyo hujulikana kama aina za maneno. Katika sura hii utajifunza kubainisha na kufafanua aina za maneno katika sentensi, kutumia aina tofauti za maneno pamoja na kutumia kamusi kutafuta maana za maneno. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kuainisha na kutumia aina za maneno katika miktadha mbalimbali kwa kuzingatia sifa na dhima zake. Vilevile, utaweza kutumia kamusi kupata maana mbalimbali za maneno.*

### Dhana ya aina za maneno

**Kazi ya 2.1**

*Soma hadithi ifuatayo, kisha fanya mazoezi na kazi zinazofuata.*

**Safari ndotoni**

Siku moja, saa za jioni, nilikuwa nimeketi chini ya mti kando ya nyumba yangu. Ilikuwa siku ngumu kwangu kwa kuwa sikuwa na chochote cha kula jioni ile. Ghafla, nilijikuta nimeingia katika lindi zito la mawazo juu ya maisha. Niliwaza jinsi ambavyo ninaweza kuishi maisha mazuri. Niliwaza kuishi maisha ambayo yataniwezesha kula mlo kamili, kuishi katika nyumba nzuri pamoja na kumiliki vitu vingi vya muhimu katika maisha.

Nilifikiria ni kwa namna gani nitaweza kuyafikia maisha ya namna hiyo lakini sikuweza kupata majibu. Nilitafakari maisha ya watu wengine huku nikilinganisha na maisha yangu. Nilijiona ni mtu wa chini sana ambaye ni rahisi hata kupata magonjwa kutokana na kukosa mlo kamili. "Lo! Maisha haya! Hivi mimi ni maskini kiasi hiki! Nitawezaje kuondokana na umaskini huu ili niishi maisha niyatakayo?" Nilijisemea kimoyomoyo huku machozi yakinilengalenga.

Jua lilizama na giza likaifunika dunia. Niliingia ndani nikamwomba Mungu, kisha nikalala. Nilipata wakati mgumu kuupata usingizi kutokana na njaa niliyokuwa nayo. Katika muda nisioujua, nilijikuta katika usingizi mzito na kuanza kuota

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 19 05/09/2021 15:40

ndoto ya ajabu. Niliota niko safarini kwenda kuyatafuta maisha yale niliyokuwa nikiyawaza jioni ile. Nilichukua begi dogo nikaweka suruali moja na mashati mawili. Nilivaa vizuri nikaianza safari ya kwenda nisikokujua kwa matumaini ya kupata maisha mazuri na ya furaha.

Nilitembea kwa miguu kutoka nyumbani kuelekea kituo cha mabasi yaendayo katika mikoa mbalimbali na nchi za nje. Kabla ya kufika kituoni, nilipita kwenye mashine ya kutolea pesa (ATM). Nilihitaji kutoa kiasi cha shilingi milioni mbili lakini nikafanikiwa kutoa shilingi milioni moja tu. Nilipofika kituoni nilipanda basi la kwenda nchini Rwanda. Tulipofika Dodoma tuliruhusiwa kwenda kula kwa masharti ya kutumia dakika kumi tu. Basi lile lilikwenda kwa kasi sana. Kila wakati tulisimamishwa na askari wa usalama barabarani kutokana na mwendokasi tuliokuwa nao. Mimi nilihofu sana. Dereva mwenyewe hakujali kabisa. Abiria nao waligeuza viti vyao kuwa vitanda kwa kuuchapa usingizi.

Pembeni mwa kiti changu alikaa mwanaume mmoja na nyuma yangu alikaa mwanamke aliyekuwa na mtoto mdogo. Niliamua kuanza kuwasemesha na kujitambulisha kwao, “Kaka mkubwa habari! Mimi ninaitwa Juma, wewe unaitwa nani?” Nilimuuliza kwa upole. “Ahaa! Nzuri Juma, ninafurahi kukufahamu. Mimi ninaitwa Amani. Huyu ni mke wangu; yeye anaitwa Tumaini. Yule pale ni mtoto wetu; yeye anaitwa Habati.” Niliendelea kuwadodosa ili kujua tumepita wapi na tumefika wapi. Walinieleza kuwa safari yetu itapita mikoa mingi ikiwemo Singida, Tabora na Shinyanga. Hata hivyo, walisema hatutapita katika wilaya zote za mikoa hiyo bali chache tu. Kwa mfano, katika Mkoa wa Tabora, hatutapita Tabora mjini bali tutapita Wilaya ya Igunga na Nzega.

Walinieleza kuwa nitafanikiwa kuona Mto Kagera kabla ya kuingia nchini Rwanda. Walisema kwamba mto huo una maporomoko makubwa ya maji. Amani alisema kuwa, yeye ni Diwani wa Kata ya Kabanga Wilaya ya Ngara. Wilaya hii ipo Magharibi mwa Tanzania mpakani mwa Burundi. Aidha, alisema kuwa, ikiwa tutapita Mwanza tutaliona Ziwa Victoria.

Tulipofika mpakani sikuruhusiwa kuvuka kwa kuwa sikuwa na kibali cha kwenda nje ya nchi. Nilibaki nimezubaa nikiwa sijui cha kufanya. Nilikaa chini ya mti. Kulikuwa na upepo mwanana uliokuwa ukivuma na kuyumbisha miti. Nikiwa chini ya ule mti niliona kikosi cha watu wakiwa wamevalia sare. Walikuwa wanamgambo wanaosaidiana na askari kulinda mpaka wetu. Mmoja wao alikuja nilipokuwa nimekaa kuniuliza, “Una shida gani?” Nilimweleza kwa ufupi nilivyozuiwa kuvuka. Aliniamuru nitoke eneo lile kwa kuwa halikuwa



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 20 05/09/2021 15:40

salama sana. "Upi ulikuwa mustakabali wangu huko ugenini?" Lilikuwa swali lisilo na jibu. Nilianza kutembea taratibu kuelekea mahali alikonielekeza yule mwanamgambo. Nilifika katika eneo ambalo lilikuwa na watu wengi waliojishughulisha na biashara mbalimbali. Niliingia katika mgahawa na kuagiza chakula. Mwenye mgahawa, kwa kumtazama alionekana kuwa ni Mnyarwanda. Mwenyewe alionekana mpole; japo zilikuwa ni hisia zangu tu kutokana na nilivyomwona.

Nilikula chakula kidogo tu lakini nikashiba sana. Nikiwa pale mgahawani nilisikia watu wakiniongelea. Walikuwa kama wanabishana. "Huyu ndiye aliyeshuka pale mpakani?" "Hapana, si yeye. Yule alikuwa mrefu kiasi bwana." "Kumbe! Lakini mbona kama ni yeye?" Yalikuwa ni mabishano yao huku wakiniangalia kwa makini. Niliinama kana kwamba sijawasikia ingawa nilisikia kila walichokisema. Mtu mwingine alikuja kabla sijatoka mahali pale. Alinichangamkia na kuniuliza, "Habari za safari?" Alikuwa miongoni mwa abiria tuliokuwa ndani ya basi lakini yeye alishuka Benako kabla ya kufika mpakani. Nilimwona ni mtu katika watu. Alinichukua na kunipeleka nyumbani kwake baada ya kumweleza kilichonikuta.

Nilipofika kwake nilikuta ana maisha mazuri sana. Yeye alikuwa mkulima na mfugaji. Nilitamani kuwa na maisha kama aliyokuwa nayo. Wakati ningali nikitafakari jinsi safari yangu ilivyokuwa na jinsi nitakavyojikwamua kimaisha, ghafla nilitoka usingizini na kujiona niko palepale nyumbani kwangu. Ama kweli ndoto ni kitu cha ajabu sana.

## Zoezi la 2.1

*Chambua maneno katika habari uliyosoma, kisha uyaorodheshe katika makundi manane (8) yafuatayo kutegemeana na aina ya neno kama lilivyotumika katika habari.*

1. Maneno yanayotaja majina ya watu, vitu, mahali, hali au tendo.
2. Maneno yanayotumika badala ya majina katika sentensi au yanayotenda kazi badala ya majina.
3. Maneno yanayosifia au kutoa taarifa zaidi kuhusu majina au mbadala wa majina hayo.
4. Maneno yanayodokeza tukio au tendo linalotendeka, lililotendeka au litakalotendeka.
5. Maneno yanayotoa taarifa zaidi kuhusu matendo, sifa au kujielezea yenyewe.



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 21 05/09/2021 15:40

6. Maneno yanayounganisha pande mbili zenye hadhi sawa kisarufi ambazo zinaweza kuwa neno na neno au kifungu kimoja cha maneno na kifungu kingine.
7. Maneno yanayoonesha uhusiano kati ya majina na maneno mengine katika tungo.
8. Maneno yanayoonesha hisia kama vile huzuni, mshtuko, hasira, furaha, mshangao au huruma.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zingatia**

Kuna aina nane (8) za maneno ambazo ni nomino (N), viwakilishi (W), vivumishi (V), vitenzi (T), vielezi (E), viunganishi (U), vihusishi (H), na vihisishi (Hs). Nomino ni maneno yanayotaja majina ya watu, vitu, mahali, hali, au tendo; kwa mfano: *Juma, gari, Geita, hasira,* na *kuimba*. Viwakilishi ni maneno yanayotumika badala ya majina au nomino katika sentensi au yanayofanya kazi badala ya majina; kwa mfano: *Wewe, yeye, sisi, wao, nyinyi,* na *wafupi*. Vivumishi ni maneno yanayosifia au kutoa taarifa zaidi kuhusu majina au mbadala wa majina hayo (viwakilishi); kwa mfano: *Yetu*, *lile*, *refu*, *mabichi*, *mfupi* na *mbivu*. Vitenzi ni maneno yanayodokeza tukio au tendo linalotendeka, lililotendeka au litakalotendeka; kwa mfano: *Tunakumbuka, aliwaibia, limetutatanisha* na *yalikuwamo*. Vielezi ni maneno yanayotoa taarifa zaidi kuhusu matendo (vitenzi), sifa (vivumishi) au kujielezea yenyewe (vielezi); kwa mfano: *Mara tatu, kama mshale, nyumbani, usiku, kwa ujasiri,* na *kwa ufundi*. Viunganishi ni maneno yanayounganisha au kuweka pamoja pande mbili zenye hadhi sawa kisarufi ambazo zinaweza kuwa ni neno na neno au kifungu kimoja cha maneno na kifungu kingine; kwa mfano: *Hamida* <u>*na*</u> *Neema* (Neno na neno) na *Mshindi wa kwanza* <u>*au*</u> *wa pili atakuwapo* (Kifungu cha maneno na kifungu cha maneno). Vihusishi ni maneno yanayoonesha uhusiano uliopo kati ya majina na maneno mengine katika tungo; kwa mfano: *Juma anakula wali* <u>*kwa*</u> *kijiko*; *Niko Tanga* <u>*kwa zaidi ya*</u> *miaka miwili sasa*; *Tanzania imeshinda magoli mawili* <u>*kwa*</u> *moja*; *Walifika wanaume kumi* <u>*kati ya*</u> *kumi na watano*; *Wote wamezaliwa* <u>*na*</u> *baba mmoja,* na *Joashi ni mtu* <u>*katika*</u> *watu*. Vihisishi ni maneno yanayoonesha hisia kama vile huzuni, mshituko, hasira, furaha, mshangao au huruma; kwa mfano: *Kumbe!, Lo!, Nini!, Ebo!, Aise!*, na kadhalika.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 22 05/09/2021 15:40

## Nomino

### Zoezi la 2.2

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Jibu maswali yafuatayo kutokana na hadithi uliyosoma ya **Safari ndotoni**.*

1. Bainisha aina za nomino zilizopigiwa mstari katika tungo zifuatazo kutegemeana na muktadha zilimotumika katika hadithi uliyosoma.
   (a) Siku moja saa za jioni nilikuwa nimeketi chini ya mti.
   (b) Ama kweli ndoto ni kitu cha ajabu sana.
2. Chambua nomino za pekee kumi zilizotumika katika hadithi uliyosoma.
3. Taja mfano wa nomino moja kwa kila kundi katika makundi yafuatayo: Watu, mahali, dira, nchi, vyeo, maziwa na mikoa kutoka katika hadithi uliyosoma.
4. Bainisha nomino za kawaida kumi kutoka katika hadithi uliyosoma.
5. Orodhesha nomino dhahania ulizozibaini katika hadithi uliyosoma.
6. Taja nomino za jamii zilizotumika katika hadithi uliyosoma.

### Kazi ya 2.2

Tunga sentensi tano (5) katika kila aina ya nomino uliyopewa. Onesha nomino hizo kwa kuzipigia mstari.

1. Nomino za kawaida
2. Nomino za pekee
3. Nomino dhahania
4. Nomino za jumla

FOR ONLINE USE ONLY

**Zingatia**

Nomino zimegawanyika katika aina nne ambazo ni nomino za pekee, kawaida, dhahania, na za jamii au jumla. Nomino za pekee zinataja majina ya watu (kwa mfano, *Juma*); mito (kwa mfano, *Zambezi*); bahari (kwa mfano, *Hindi*); sayari (kwa mfano, *Pluto*); na mahali (kwa mfano, *Mwanza*). Kwa upande wa mahali, linaweza kuwa jina la kijiji, kata, wilaya, mkoa, nchi au bara. Vilevile, nomino za pekee hutaja majina ya uelekeo (dira), kwa mfano, *Kaskazini;* pamoja na vyeo vinavyoambatana na majina mahususi kama vile, *Mwenyekiti Joni.* Zinaitwa za pekee kwa kuwa hutaja kitu ambacho ni mahususi. Hivyo, upekee wa mtu au kitu ndio unaoifanya nomino hiyo kuwa ya pekee. Kumbuka kuwa unapoandika nomino za pekee sharti uanze kwa herufi kubwa. Nomino za kawaida zinataja vitu au mambo ya kawaida, kwa mfano: *Mti, kijiji, watu, nyoka,* na *ziwa.* Nomino



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 23 05/09/2021 15:40

hizi huandikwa kwa kuanza na herufi ndogo isipokuwa kama zitaanza mwanzoni mwa sentensi. Nomino dhahania zinataja mambo au vitu ambavyo huwezi kuviona wala kuvigusa kwa kuwa ni vya kufikirika tu; kwa mfano, *upepo, baridi,* na *Mungu.* Aidha, baadhi ya nomino dhahania zina sifa za pekee ingawa hazionekani; kwa mfano, *Mungu*. Nomino za jamii au jumla zinataja majina ya makundi ya watu au vitu; kwa mfano, *jeshi, kamati, baraza, ukoo, familia,* na *kikosi*. Ingawa nomino hizi zipo katika umoja, hazitaji kitu kimoja.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Viwakilishi

#### Zoezi la 2.3

1. Taja maneno kumi (10) yaliyotumika badala ya nomino katika hadithi uliyosoma.
2. Taja viwakilishi sita (6) vya nafsi vilivyotumika katika hadithi uliyosoma.
3. Bainisha viwakilishi viulizi vitano (5) kutoka katika hadithi uliyosoma.
4. Taja viwakilishi vioneshi vitano (5) vilivyotumika katika hadithi uliyosoma.
5. Bainisha viwakilishi vya idadi vitano (5) vinavyojitokeza katika hadithi uliyosoma.
6. Tunga sentensi tano (5) kwa kutumia viwakilishi tofauti vya mahali vilivyotumika katika hadithi uliyosoma.
7. Taja viwakilishi vya pekee vitano (5) vilivyotumika katika hadithi uliyosoma.

#### Kazi ya 2.3

Tunga sentensi sita (6) kwa kutumia aina tofautitofauti za viwakilishi, kisha pigia mstari viwakilishi hivyo.

**Zingatia**

Viwakilishi vimegawanyika katika aina sita (6) ambazo ni viwakilishi vya **nafsi**: kwa mfano; *mimi, sisi, wewe, ninyi, yeye,* na *wao;* viwakilishi vya **idadi**: kwa mfano; *mmoja, wawili, sita,* na *manane;* viwakilishi **vimilikishi**: kwa mfano; *yangu, lako,* na *chake;* viwakilishi **viulizi**: kwa mfano; *wangapi, kipi,* na *wapi;* viwakilishi **vioneshi**: kwa mfano; *pale, hapa,* na *humo;* na viwakilishi vya **pekee**: kwa mfano; *mwenyewe* na *wengine*. Kwa kuwa kiwakilishi hutumika badala ya nomino, ni dhahiri kuwa nomino na kiwakilishi haviwezi kutokea mahali pamoja katika sentensi. Ikitokea hivyo, kiwakilishi kitabadilika hadhi na kuwa kivumishi. Chunguza mifano ifuatayo:

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 24 05/09/2021 15:40

**Mwenyewe** hakujali.
Dereva **mwenyewe** hakujali.
Katika sentensi ya 1 neno **mwenyewe** ni kiwakilishi wakati katika sentensi ya 2 neno **mwenyewe** ni kivumishi.

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la 2.4

*Bainisha vivumishi mbalimbali kutoka katika hadithi uliyosoma, kisha:*
1. Tunga sentensi tano (5) kwa kutumia vivumishi vya idadi.
2. Tunga sentensi tano (5) kwa kutumia vivumishi vya sifa.
3. Taja vivumishi vya -a unganifu.
4. Bainisha vivumishi vya pekee vilivyotumika katika hadithi uliyosoma.
5. Taja vivumishi viulizi vilivyotumika katika hadithi uliyosoma.
6. Bainisha vivumishi vya jina vilivyotumika katika hadithi uliyosoma.
7. Taja vivumishi vioneshi vilivyotumika katika hadithi uliyosoma.

### Vivumishi

## Kazi ya 2.4

*Chunguza sentensi zifuatazo, kisha bainisha vivumishi vilivyotumika kwa kufafanua ni aina gani ya kivumishi.*
1. Kinu chake kimepotea.
2. Mawe yale yamekusanywa na mlinzi.
3. Mti upi umeangushwa na upepo?
4. Nyumba nzuri hujengwa kwa gharama kubwa.
5. Wanafunzi wengine wamechelewa.
6. Wezi wale wamekamatwa usiku huu.
7. Kitabu cha mwanafunzi kimepatikana.
8. Hiki kidogo kimeharibika.
9. Wamenunua ng'ombe wengi.
10. Wanafunzi wanachezea mpira mdogo.

FOR ONLINE USE ONLY

**Zingatia**
Kwa kuwa kivumishi husifia au hutoa taarifa zaidi kuhusu nomino au kiwakilishi, ni dhahiri kuwa kivumishi hutumika ikiwa kuna nomino au kiwakilishi. Ikiwa kivumishi kitabaki bila nomino au kiwakilishi, kitapoteza sifa ya kuwa kivumishi. Katika muktadha huo kitabeba dhima ya kiwakilishi. Chunguza mifano ifuatayo:



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 25 05/09/2021 15:40

(a) Mtoto **mzuri** amekuja.
(b) Hii **nyembamba** haiwezi kufunga kuni.
(c) **Mzuri** amekuja.
(d) **Nyembamba** haiwezi kufunga kuni.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Katika mifano (a) na (b) maneno **mzuri** na **nyembamba** ni vivumishi wakati katika sentensi (c) na (d) maneno **mzuri** na **nyembamba** ni viwakilishi. Vivumishi hutokea baada ya nomino au viwakilishi. Kuna aina mbalimbali za vivumishi kama vile: Vivumishi vya sifa: kwa mfano, *baya, jeupe, dogo, kali,* na *refu*; vya idadi: kwa mfano, *tatu, chache,* na *wengi*; viulizi: kwa mfano, *ngapi, yupi,* na *gani*; vioneshi: kwa mfano, *yule, kile, hiki, hapa,* na *hawa*. Aina nyingine ya vivumishi ni vya -a unganifu: kwa mfano, *wa Juma, la Heri* na *cha mama*; vimilikishi: kwa mfano, *yangu, letu, lao,* na *chenu*; pekee: kwa mfano, *-enyewe, -ote, -o-ote,* na *-ingine*. Baadhi ya nomino hufanya kazi ya kivumishi kwa vile huzifafanua nomino zingine. Nomino hizi huitwa vivumishi vya jina: kwa mfano, *Mwalimu* ***Hamisi*** na *Katibu* ***Kata***.

### Vitenzi

### Zoezi la 2.5

1. Chambua vitenzi vikuu vitano ulivyobaini katika hadithi uliyosoma.
2. Bainisha vitenzi visaidizi vitano kutoka katika hadithi uliyosoma.
3. Orodhesha vitenzi vishirikishi vitano kutoka katika hadithi uliyosoma.
4. Fafanua dhima ya vitenzi katika sentensi.
5. Eleza tofauti iliyopo kati ya vitenzi visaidizi na vitenzi vishirikishi kama vilivyotumika katika hadithi uliyosoma.

FOR ONLINE USE ONLY

### Kazi ya 2.5

Tunga sentensi tano (5) zenye aina tofautitofauti za vitenzi, kisha vipigie mstari na kueleza ni aina gani ya kitenzi.

**Zingatia**

Kitenzi kinaweza kujibainisha katika aina tatu ambazo ni kitenzi kikuu (T), kitenzi kisaidizi (Ts), na kitenzi kishirikishi (t). Kitenzi kikuu kinaarifu tendo kuu katika sentensi; hivyo, huitawala sentensi; kwa mfano, *Juma anakula chakula.* Kitenzi kisaidizi kinafanya kazi ya kusaidia kitenzi kikuu kukamilisha taarifa katika



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 26 05/09/2021 15:40

sentensi; kwa mfano, *Juma alikuwa anakula chakula*. Hii ina maana kwamba huwezi kutumia kitenzi kisaidizi peke yake katika sentensi bali utakitumia pamoja na kitenzi kikuu. Vilevile, huwezi kuwa na vitenzi vikuu zaidi ya kimoja vilivyofuatana katika sentensi. Ikitokea hivyo, kitenzi kimoja tu kitabaki kuwa kitenzi kikuu. Pia, kitenzi kishirikishi (t) kina dhima ya kuonesha kuwapo au kutokuwapo kwa kitu, hali, au jambo. Vitenzi vishirikishi ni kama vile: *Si, ni, ndiye, ndio, siyo*, na kadhalika.

## Vielezi

### Zoezi la 2.6

*Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno uliyopewa katika kisanduku.*

| wapi, kabisa, taratibu, chini ya mti, nchini, Kinyarwanda, jinsi |
|---|

1. Juma amejifunza kuzungumza ………....................................................
2. Mgeni wetu atawasili ……………………………………………... kesho.
3. Mwalimu alitaka waishi …………………………………………………?
4. Hapendi utani ..........................................................................................
5. Alisema tatizo litapungua ………………………………………………
6. Alisema kuwa amedondoka ......................................................................
7. Walikuwa wakinishangaa .................................................... nilivyochafuka.

### Kazi ya 2.6

*Chambua vielezi vilivyomo katika hadithi ya **Safari ndotoni** kisha:*

1. Eleza ni aina gani ya vielezi vimetumika.
2. Tumia vielezi vitano (5) kati ya ulivyovibainisha kisha tunga sentensi mbili (2) kwa kila kielezi.

**Zingatia**

Vielezi hutoa taarifa au ufafanuzi kuhusu tendo lilivyofanyika, limefanyikia wapi, limefanyika mara ngapi, limefanyika lini, na kadhalika. Vielezi vimegawanyika katika aina zifuatazo: Vielezi vya **mahali**; hivi hujibu swali wapi kuhusiana na kitenzi, kwa mfano, *mjini* na *chini ya meza*. Vielezi vya **wakati**; hivi hujibu swali lini tendo lilitendeka au limetendeka, kwa mfano, *mapema* na *wiki iliyopita*. Vielezi vya **namna** au **jinsi**; hivi hujibu swali vipi tendo lilitendwa, kwa mfano, *vizuri sana* na *polepole*. Vielezi vya **idadi** au **kiasi**; hivi hujibu swali mara ngapi au kiasi gani tendo limejirudia, kwa mfano, *mara mbili* na *tena na tena*.



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 27 05/09/2021 15:40

## Viunganishi

### Zoezi la 2.7

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

1. Bainisha viunganishi vilivyotumika katika hadithi ya **Safari ndotoni**.
2. Fafanua dhima za viunganishi ulivyobainisha katika swali la 1.

### Kazi ya 2.7

*Tumia viunganishi vifuatavyo kutunga sentensi mbili (2) kwa kila kiunganishi:*

1. na
2. ingawa
3. kisha
4. tena

**Zingatia**

Kiunganishi hutumiwa katika kuweka pamoja au kuunganisha pande mbili zenye hadhi sawa kisarufi. Pande hizo zinaweza kuwa neno na neno kama vile, nomino na nomino au kitenzi na kitenzi au kifungu cha maneno na kifungu kingine cha maneno. Kwa hiyo, huwezi kuunganisha aina tofauti za maneno kama kitenzi na nomino. Hivyo, unapounganisha unapaswa kuzingatia hadhi sawa ya vinavyounganishwa; kwa mfano:

(a) Anaimba **na** kucheza.
(b) Anasoma **ili** afaulu mtihani.
(c) Sura ya kwanza **hadi** sura ya tano zimepangwa vizuri.
(d) Watoto wanasoma sana **kwa sababu** wanataka kufanikiwa kimaisha.

FOR ONLINE USE ONLY

## Vihusishi

### Zoezi la 2.8

1. Kwa kutumia mifano kutoka katika hadithi uliyosoma, taja dhima kuu ya vihusishi katika lugha.
2. Chagua vihusishi vitano (5) kutoka katika hadithi uliyosoma, kisha tunga sentensi mbili kwa kila kihusishi.



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 28 05/09/2021 15:40

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya 2.8**

*Kwa kutumia vihusishi vifuatavyo, tunga sentensi mbili (2) kwa kila kimoja:*

1. kwa
2. katika
3. baada ya
4. juu ya
5. na

**Zingatia**

Vihusishi vinaonesha uhusiano kati ya neno na neno au kifungu cha maneno na kifungu kingine. Tofauti na ilivyo kwa viunganishi, vihusishi huhusisha tungo zenye hadhi tofauti kisarufi. Kwa mfano, katika sentensi *Mwinga anakula <u>kwa</u> kijiko,* neno *kwa* linahusisha kitenzi *anakula* na nomino *kijiko*. Mifano ya vihusishi ni kama vile, *kwa, na, juu ya, katika,* na kadhalika. Tofauti kubwa kati ya kiunganishi na kihusishi ni hadhi ya maneno au vifungu vya maneno vinavyounganishwa au kuhusishwa. Ikiwa vina hadhi sawa kitakuwa kiunganishi na ikiwa vina hadhi tofauti kitakuwa kihusishi.

## Vihisishi

**Kazi ya 2.9**

Bainisha maneno yote yanayoonesha hisia za msimuliaji kama yanavyojitokeza katika hadithi ya **Safari ndotoni**.

**Zoezi la 2.9**

*Chagua vihisishi vitano (5) kutoka kwenye hadithi uliyosoma, kisha:*

1. Tunga sentensi kwa kutumia vihisishi ulivyobainisha.
2. Eleza hisia zinazodokezwa na vihisishi ulivyovitumia kwenye sentensi ulizotunga.

**Zingatia**

Unapokuwa katika mazingira fulani unaweza kushuhudia matukio mbalimbali. Kuna matukio ya kuhuzunisha, kufurahisha, kuchukiza, kuchekesha, na mengineyo. Matukio haya yanaathiri uteuzi na namna ya kuyatumia maneno. Kwa hiyo, vihisishi (Hs) ni maneno yanayoonesha hisia za mzungumzaji kama vile huzuni, mshituko, hasira, furaha, mshangao, au huruma. Kwa mfano, *Kumbe!, Lo!, Nini!, Ebo!, Aise!*, na *Mungu wangu!*

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la 2.10

1. Taja aina za maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo:
   (i) Kabla ya kuanza kula nilikunywa maji.
   (ii) Ama kweli ndoto ni kitu cha ajabu sana.
   (iii) Lo! Kumbe ilikuwa ndoto bwana!
   (iv) Upi ulikuwa mustakabali wangu huko ugenini?
   (v) Dereva mwenyewe hakujali kabisa.
   (vi) Juzi usiku nikiwa nimelala niliota ndoto.
   (vii) Huyu ndiye aliyeshuka kule mpakani?
2. Eleza sababu mbili (2) zinazotofautisha nomino za pekee na nomino za kawaida.
3. Kwa mtazamo wako unafikiri kutatokea nini ikiwa nomino na kiwakilishi vitafuatana katika sentensi?
4. Kuna tofauti gani baina ya kitenzi kikuu na kitenzi kisaidizi?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 2.11

*Chagua neno moja kati ya maneno yaliyomo kwenye kisanduku, kisha jaza neno hilo kwa usahihi kwenye nafasi iliyoachwa wazi katika sentensi zinazofuata.*

| kanga, Lo, viti, ambavyo, vya, yupi, hii, kitabu, yetu, ndiye, na, yule, asubuhi |
|---|

1. Huyu … ……….. niliyekuwa ninamtafuta tangu …… ………
2. Aliona …… ……… vizuri zaidi.
3. Nchi …… ……… ina vivutio vingi …… ……… watalii.
4. Juma anasoma …… ……… kuandika kila siku.
5. Mtoto …… …….. amekuja na mpira.
6. Wanafunzi wanasoma …… ………
7. …… ………! Hata kama mmekuja, hamtamwona.
8. …… ……… wanaishi hapa.
9. Mtu …… ……… unayemsema?
10. Jerome amenunua vitabu …… ……… tulimwagiza?

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 30 05/09/2021 15:40

### Zoezi la 2.12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Bainisha aina za maneno zilizounda sentensi zifuatazo:*

1. Kaka ananihimiza kila mara kusoma kwa bidii.
2. Waziri amesema watu wafanye usafi ili kuepuka magonjwa hatari.
3. Mazoezi yanaimarisha afya ya mwili.
4. Huyu ndiye aliyevunja rekodi katika matokeo ya darasa la saba.
5. Epuka sana ndoa za utotoni ili usome mpaka chuo kikuu.
6. Mungu wangu! Kelele zetu zitatuponza leo.
7. Mtu aliyesumbua watu mitandaoni amejisalimisha katika kituo cha polisi yeye mwenyewe.
8. Mara nyingi Juma huja hapa kutoa elimu ya kodi.

### Kazi ya 2.10

*Kusanya maneno ya aina tofautitofauti kutoka katika mazingira unamoishi, kisha tunga sentensi zenye miundo ifuatayo kwa kutumia maneno hayo:*

1. N + Ts + T + N + E
2. N + V + T + E
3. W + V + Ts + T + H + N
4. W + t + N + V
5. N + V+ T + N
6. W + T+ N

### Kazi ya 2.11

*Panga maneno yafuatayo katika makundi manane (8) kulingana na aina za maneno, kisha tunga sentensi kwa kila neno kuonesha aina yake kulingana na ulivyolitumia katika sentensi (Neno moja linaweza kujirudia katika makundi tofauti ilimradi litumike kwa usahihi).*

| |
|---|
| Januari, ni, mfupi, mbele ya, ambaye, Mungu, katili, upesi, sura, lile, kwa, ili, chochote, ha!, ndiye, soma, shambani, kile, mmoja, baraka, mimi, si, Mungu!, ipo. |

FOR ONLINE USE ONLY




KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 31 05/09/2021 15:40

## Kazi ya 2.12

*Chunguza kielelezo kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.*

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE




**Kielelezo namba 2.1:** *Mti unaoonesha aina za maneno*

## Maswali

1. Fafanua kazi ya kila aina ya neno inayoonekana katika kielelezo hicho.
2. Fafanua aina ndogondogo zinazopatikana ndani ya aina za maneno yafuatayo:
   (a) Nomino
   (b) Viwakilishi
   (c) Vivumishi
   (d) Vitenzi
   (e) Vielezi

FOR ONLINE USE ONLY

**Zingatia**

Neno hujibainisha vizuri kuwa lipo katika aina fulani ya neno pale linapokuwa katika matumizi. Ni vigumu kubaini neno fulani ni la aina gani kama liko peke yake. Chunguza mifano ifuatayo:

1. **Dodoma** ni makao makuu ya nchi.
2. Mwalimu amekwenda **Dodoma**.
3. **Vizuri** vimeletwa.
4. Viti **vizuri** vimeletwa.
5. Wanaimba **vizuri**.

Katika sentensi ya kwanza, neno **Dodoma** limetumika kama nomino ilhali katika sentensi ya pili, neno **Dodoma** limetumika kama kielezi cha mahali. Vilevile, katika sentensi ya tatu, neno **vizuri** limetumika kama kiwakilishi ilhali katika sentensi ya nne, neno **vizuri** limetumika kama kivumishi. Aidha, neno hilohilo **vizuri** limetumika kama kielezi cha namna au jinsi katika sentensi ya tano.

### Matumizi ya kamusi

**Kazi ya 2.13**

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Kamusi ni kitabu cha marejeo chenye orodha ya maneno yaliyopangwa kwa utaratibu maalumu wa kialfabeti. Maneno hayo hukusanywa kutoka kwa wazungumzaji wa lugha inayotungiwa kamusi. Kwa kawaida, maneno hufafanuliwa kwa namna ambayo msomaji huweza kuelewa. Hata hivyo, ufafanuzi wa maneno kwenye kamusi hutegemea lengo la kamusi inayohusika.

Kuna aina mbalimbali za kamusi. Kuna kamusi ya lugha moja, yaani orodha ya maneno pamoja na maelezo yake yanakuwa katika lugha moja. Vilevile, kuna kamusi ya lugha mbili au zaidi, kwa maana ya neno kuwa lugha moja na kufafanuliwa kwa maelezo ya lugha nyingine. Aidha, kamusi inaweza kuwa ya somo mahususi au uwanja fulani kama vile methali, vitendawili, nahau, visawe, na kadhalika.

Kamusi ina umuhimu mkubwa katika lugha kwani husaidia kufafanua maneno mbalimbali. Hivyo, humwongezea wingi wa msamiati mtumiaji wa lugha inayohusika. Hata hivyo, wingi wa msamiati katika kamusi hutegemea lengo la mtunzi wa kamusi, kwani si rahisi maneno yote kuingizwa katika kamusi moja.

Kwa kawaida, maneno yote yanayoingizwa katika kamusi hupangwa kwa utaratibu wa alfabeti. Maneno yanayoanza na herufi **a**, huwekwa chini ya herufi A. Vivyo hivyo, kwa maneno yanayoanza na herufi **b**, **ch**, **d** hadi **z**. Ikiwa herufi za kwanza za maneno zinafanana, basi inaangaliwa herufi ya pili, tatu na kuendelea mpaka lipatikane neno linalostahili kuanza; kwa mfano, *kaka, keki, kiko, koti* na *kuti*. Maneno yote haya yanaanza na herufi **k**. Hivyo, imeangaliwa herufi ya pili ambayo ndiyo imeongoza kuyapanga maneno kwa kufuata irabu **a**, **e**, **i**, **o** na **u**. Kama herufi za pili zingefanana kwa maneno yote, tungeangalia herufi ya tatu na kuendelea mpaka maneno yote yapangwe kwa usahihi.



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 33 05/09/2021 15:40

Ili kuelewa vema dhana hii, chunguza kielelezo namba 2.2 kilichopo ukurasa wa 35 kinachoonesha jinsi maneno yalivyopangwa na taarifa zake.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Maneno yote katika kielelezo hicho yameanza na herufi **b** na herufi ya pili kwa maneno yote ni **u**. Kwa hiyo, imeangaliwa herufi ya tatu ambayo pia, kwa baadhi ya maneno, imefanana na kulazimika kuangalia herufi ya nne, tano na kuendelea. **Kidahizo** ndilo neno kuu katika kamusi; haya ni maneno yanayoorodheshwa kwenye kamusi kwa chapa iliyokozwa au kwa kuwekwa rangi kwa lengo la kutofautishwa na mengine ili yafafanuliwe. Kidahizo pamoja na maelezo yake kwa pamoja huitwa **Kitomeo**. Ikiwa neno lina maana zaidi ya moja, maana zote huorodheshwa kwa kupewa namba kama ilivyo katika neno **buluu, bumba, bumburuk.a** na **bunga** katika kielelezo 2.2 kilichopo ukurasa wa 35. Mtumiaji wa kamusi anapaswa kuzisoma na kuona ni ipi inaendana na kile anachokitafutia maana kwa kuhusisha mazingira ambamo neno linalohusika limetumika.

Kamusi huanza kwa utangulizi ambao humsaidia mtumiaji kuitumia. Pia, hujumuisha maelezo yanayohusu kamusi yenyewe, shukurani, mwongozo kwa mtumiaji, vifupisho vya maneno, alama za uandishi, na matumizi yake kama inavyoonekana katika kielelezo 2.3 kilichopo ukurasa wa 36.

Pia, kamusi ina sehemu ya kiini, yaani maneno na ufafanuzi wake. Kiini huwa na maneno mbalimbali yaliyopangwa kialfabeti na maana zake pamoja na taarifa nyingine zinazohusu maneno hayo. Taarifa hizo ni pamoja na asili ya neno linalohusika, kisawe cha neno hilo, kategoria/aina yake, wingi au umoja wake, matamshi yake pamoja na taarifa nyingine zinazoweza kutolewa kama zinavyoonekana katika kielelezo 2.2 kilichopo ukurasa wa 35.

Sehemu ya mwisho katika kamusi huwa na taarifa mbalimbali kama vile urejeano wa vibadala, sehemu za mwili wa mwanadamu, michoro ya mavazi, samaki, wanyama, wadudu, mimea, matunda, vyombo vya usafiri, ala za muziki, zana za kazi, viambishi vya maneno, majina ya nchi na vingine vingi. Tazama mfano katika kielelezo 2.4 kilichopo ukurasa wa 37.


FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 34 05/09/2021 15:40

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kubomolea na kuzolea majengo, majabali au michanga.



buldoza

**buli** /buli/ *nm (ma-) [li-/ya-]* chombo cha kutilia chai au kahawa; birika. (>Kre)

**bulibuli¹** /bulibuli/ *nm (-) [i-/zi-]* mfumo wa kofia nyeupe ya mwambao wa pwani ya Afrika Mashariki iliyotiwa nakshi; kofia ya kazi: *Kofia ya* ~. (>Kar)

**bulibuli²** /bulibuli/ *kv* -zuri, -ema: *Ana tabia* ~. (>Kar)

**bulina** /bulina/ *nm (-) [i-/zi-]* sehemu ya mbele ya chombo cha baharini.

**buluu** /bulu:/ pia **bluu** /blu:/ *nm (-) [i-/zi-]* **1** rangi ya samawati; nili. **2** dawa inayotumiwa kung'arisha nguo nyeupe baada ya kufuliwa. (>Kng)

**bumba** /bumba/ *nm (ma-) [li-/ya-]* **1** mfuko mdogo; kipeto, kifurushi, paketi: *~ la majani ya chai; ~ la tumbaku.* **2** fungu la vitu au wadudu: *~ la nyuki* kikundi cha nyuki waliosongamana na kushikana sana.

**bumbuazi** /bumbuwazi/ *nm (-) [i-/zi-]* hali ya kuwa kimya na kutojua la kufanya au kutosikia lisemwalo: *Pigwa na ~; Shikwa na ~*; butaa, butwaa, mshangao.

**bumbura** /bumbura/ *nm (-) [a-/wa-]* samaki wa maji chumvi mwenye macho manene afananaye na chewa au mzia lakini mfupi.

**bumburuk.a** /bumburuka/ *kt [sie]* **1** shtuka ghafla na kwenda mbio k.v. kundi la ndege au wanyama wanapokurupushwa; kurupuka. **2** amka kwa kitisho. *~ia, ~ika, ~isha.*

**bumbwi** /bumbwi/ pia **bwimbwi** /bwimbwi/ *nm (ma-) [li-/ya-]* unga wa mchele ulioumuliwa na kutiwa sukari, machicha ya nazi na maji kidogo au tui; kigodo.

**bumia** /bumija/ *nm (-) [i-/zi-]* (kb) kipande cha ubao kilichomo jahazini kinachofungwa kwenye mkuku na kubeba fashini. (>Kaj)

**bumu¹** /bumu/ *nm (ma-) [li-/ya-]* aina ya jahazi la kizamani.

**bumu²** /bumu/ *nm (-) [a-/wa-]* bundi, babewana.

**bumunda** /bumunda/ *nm (ma-) [li-/ya-]* andazi linalotengenezwa kwa ndizi mbivu na unga na kuokwa au unga wa bisi za mtama unaochanganywa na samli na kuviringwa kama ladu.

**bumut.a** /bumuta/ *kt [ele]* fufuta, buta, kung'uta. *~ana, ~ia, ~iana, ~ika, ~isha, ~iwa, ~wa.*

**bunda¹** /bunda/ *nm (ma-) [li-/ya-]* fungu la vitu kama karatasi au nguo vilivyofungwa pamoja; furushi, burungutu: *~ la noti; ~ la katani; ~ la karatasi.* (>Kng)

**bund.a²** /bunda/ *kt [ele]* shindwa mtihani: *Matokeo yanaonesha watoto wengi wame~ mitihani yao. ~ia, ~ika, ~isha, ~wa.*

**bundi** /bundi/ *nm (-) [a-/wa-]* ndege mkubwa arukaye usiku tu na mwenye macho makubwa yanayomwezesha kuona gizani, hudhaniwa kuwa ni ndege mwenye kuleta kisirani au msiba; bumu, babewana.



bundi

**bundi.a** /bundija/ *kt [sie]* kundaa, via. *~ka, ~lia, ~sha.*

**bunduki** /bunduki/ *nm (-) [i-/zi-]* silaha ya kufyatulia risasi kwa nguvu: *Piga ~; Elekeza ~.* (>Kar/Khi)



bunduki

**bunga¹** /bunga/ *nm (-) [a-/wa-]* mtu asiyeelewa mambo; mtu mpumbavu anayeonewa ovyo; zuzu.

**bunga²** /bunga/ ► *kv* -pumbavu.


**bungala** /bungala/ *nm (-) [i-/zi-]* aina ya mchele, ndizi au mua: *Ndizi za ~ aina*

**Kielelezo namba 2.2:** *Mfano wa ufafanuzi wa maneno katika kamusi*

**Chanzo**: TUKI (2013: 47)



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 35 05/09/2021 15:40





**Kielelezo namba 2.3:** *Sehemu ya utangulizi wa kamusi*

**Chanzo**: TUKI (2013: x)

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 36 05/09/2021 15:40




**Kielelezo namba 2.4:** *Sehemu ya mwisho wa kamusi*

**Chanzo**: TUKI (2013: 658)



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 37 05/09/2021 15:40

## Maswali

1. Bainisha sehemu kuu tatu (3) za kamusi.
2. Kamusi inakusaidiaje katika kupata maana za maneno?
3. Kwa kutumia mifano, fafanua tofauti iliyopo baina ya kidahizo na kitomeo.
4. Eleza uhusiano uliopo baina ya kidahizo na kitomeo kwa kutumia mifano kutoka kwenye kielelezo 2.2 ulichopewa.
5. Tafuta maana za maneno yafuatayo katika kamusi, kisha tunga sentensi moja kwa kila neno.
   (a) kalamu
   (b) soma
   (c) tara
   (d) kinagaubaga
   (e) msira
   (f) sokomeza

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Zoezi la marudio la 2

1. Chagua jibu sahihi katika maswali yafuatayo:
   (i) Mkisi amekwenda Dodoma. Neno Dodoma limetumika kama aina gani ya neno?
      (a) Nomino
      (b) Kihisishi
      (c) Kielezi
      (d) Kivumishi
      (e) Kiwakilishi

   (ii) Aina ya neno inayofafanua zaidi kuhusu nomino au viwakilishi huitwa …………..
      (a) kielezi
      (b) kihusishi
      (c) kitenzi
      (d) kiunganishi
      (e) kivumishi

FOR ONLINE USE ONLY

(iii) Wageni wetu walikaribishwa vizuri sana. Neno **sana** ni aina gani ya neno?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(a) Kielezi
(b) Kitenzi
(c) Kivumishi
(d) Kiwakilishi
(e) Kihisishi

(iv) Paka amelala **chini ya** meza. Maneno yaliyokozwa yametumika kama ..............................

(a) kiwakilishi
(b) kihusishi
(c) kiunganishi
(d) kielezi
(e) kivumishi

(v) Baba alinunua viatu vizuri. Vizuri vyote viliwekwa kabatini. Dada alivipanga vizuri. Katika mfuatano wa sentensi hizo neno **vizuri** limetumika kama ..............................

(a) kiwakilishi, kivumishi, na kielezi
(b) kivumishi, kielezi, na kiwakilishi
(c) kiwakilishi, kielezi, na kivumishi
(d) kivumishi, kiwakilishi, na kielezi
(e) kielezi, kivumishi, na kiwakilishi

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 39 05/09/2021 15:40

2. Oanisha sentensi zenye matumizi ya vivumishi katika orodha **A** na aina ya kivumishi husika kutoka orodha **B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| Orodha A | Orodha B |
|---|---|
| (i) Mwalimu wetu alileta kitabu darasani. | A. Kivumishi cha jina |
| (ii) Wanafunzi wale wanafanya mazoezi uwanjani. | B. Kivumishi cha kuuliza |
| (iii) Chukua kiti chochote. | C. Kivumishi cha idadi |
| (iv) Mjomba Kichau amesafiri. | D. Kivumishi cha sifa |
| (v) Wanakijiji wangapi wamepiga kura? | E. Kivumishi cha pekee |
| (vi) Watoto watatu wamesimuliwa hadithi. | F. Kivumishi kimilikishi |
| (vii) Askari hodari amemkamata mwizi. | G. Kivumishi kioneshi |
| | H. Kivumishi cha -a unganifu |
| | I. Kivumishi cha taarifa |

3. Bainisha aina za maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo:
   (a) <u>Wewe</u> umepata zawadi nzuri.
   (b) Kilimanjaro <u>ni</u> mlima mrefu.
   (c) Baba amekwenda <u>Tanga</u>.
   (d) Mwalimu <u>mpole</u> amekuja.
   (e) Shule yetu ni nzuri <u>sana</u>.
   (f) Wake <u>kwa</u> waume walihudhuria mkutano.
   (g) Vyombo vingine <u>vimevunjika</u>.
   (h) Kalamu <u>zipi</u> haziandiki?
   (i) <u>Lo</u>! Umechelewa, mwalimu ameondoka.
   (j) Wananchi <u>walitaka</u> kujenga shule.

FOR ONLINE USE ONLY

4. Tunga sentensi zenye aina za maneno yafuatayo:
   (a) N + T + N + E
   (b) N + V + T + N + V
   (c) W + Ts + T + N
   (d) N + t + N
   (e) H + T + E
   (f) N + U + N + T
   (g) N + T+ H + N



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 40 05/09/2021 15:40

5. Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno uliyopewa katika kisanduku.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| |
|---|
| *gari, mwema, wao, shambani, ili, aisee, katika, si, pikipiki, kwa sababu* |

(a) Mwanafunzi anatakiwa kusoma vitabu vingi ………. kupata maarifa.
(b) ………. lake limeharibika.
(c) Mtoto ………. huwaheshimu watu wote.
(d) ………. wamemaliza kazi yao kwa wakati.
(e) Mkulima amepanda mazao mengi ……….
(f) ……….! Kijana huyu anajituma sana.
(g) Maki ………. mtundu.
(h) Babu anapenda kupumzika ………. bustani ya maua.

FOR ONLINE USE ONLY

# Sura ya Tatu

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Fasihi kwa ujumla

### Utangulizi

*Fasihi ni kazi ya sanaa inayotumia lugha kufikisha ujumbe kwa jamii. Katika sura hii utajifunza fasihi na dhima zake, aina za fasihi, na tanzu za fasihi simulizi, na vipera vyake. Vilevile, utajifunza usimulizi wa hadithi. Pia, utajifunza kuhakiki kazi za fasihi simulizi na kuhakiki semi katika kazi mbalimbali za fasihi simulizi. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kutunga, kuhakiki, na kusimulia kazi za fasihi simulizi.*

### Fasihi na dhima zake

**Kazi ya 3.1**


*Soma masimulizi yafuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

"Mimi ninaitwa Fasihi, mtoto wa Mzee Sanaa. Leo ninataka kusimulia kuhusu familia yetu. Nitasimulia kuhusu mzazi wangu, mimi mwenyewe, wanangu, wajukuu, vitukuu hadi vilembwe na vilembwekeza au vinying'inya. Zamani watu walipewa majina kutokana na kazi zao. Mzazi wangu alipewa jina la Sanaa kwa kuwa hutumia ufundi katika kufanya shughuli zake za kila siku. Watu huvutiwa sana na kazi zake kwani ufundi wake huipamba kazi na kuifanya iwe na mvuto. Katika familia yetu tumezaliwa watoto tisa. Ndugu zangu ni *Ufinyanzi, Uchoraji, Ufumaji, Muziki, Uchongaji, Utarizi, Maonesho,* na *Ususi.*"

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 42 05/09/2021 15:40




**Kielelezo namba 3.1:** *Matawi ya sanaa*

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(*Bwana Fasihi anavuta pumzi na kushusha, kisha anaendelea kusimulia.*) "Mimi ni mtoto pekee niliye tofauti na ndugu zangu. Tofauti hiyo husababishwa na nyenzo tunazotumia katika shughuli zetu licha ya kwamba wote tunatumia ufundi. Mimi pekee ndiye ninatumia lugha kama nyenzo kuu katika shughuli zangu. Unaponizungumzia mimi, kamwe huwezi kukwepa kumzungumzia mfanyakazi wangu Fanani. Huyu ndiye ninayemtumia kufanya kazi zangu na kuziwasilisha kwa Hadhira ambao ndio wanufaika wa kazi zangu. Kazi zangu ni kuelimisha jamii, kuhamasisha na hata kuchochea ukombozi. Kazi nyingine ni kuburudisha na kuisisimua jamii pamoja na kuhifadhi utamaduni na kurithisha amali za jamii.

Watu hawana dogo bwana! Upende usipende, chochote utakachokifanya lazima kipewe jina. Kazi zangu ninazofanya kwa kushirikiana na wanangu, ambao pia humtumia *Fanani,* wanaziita *Maudhui*. Maudhui ni kile kinachofikishwa kwa hadhira. Kama nilivyosema hapo awali, sisi ni uzao wa *Sanaa* ambaye hutumia ufundi mkubwa katika kufanya kazi zake. Ufundi wa Sanaa huitwa Fani. Fani na maudhui ni sawa na pande mbili za shilingi moja. Hii ni kwa sababu huwezi kufikisha maudhui bila kutumia fani.

Ngoja nisimulie kwa ufupi jinsi ninavyofanya kazi zangu. Mimi ninawatumia wanangu katika kufanya kazi zangu. Aidha, wanangu wanamtumia mfanyakazi wetu Fanani kuyapeleka maudhui kwa Hadhira kwa kutumia fani. Maudhui huhusisha dhamira, migogoro, ujumbe, mtazamo, msimamo na falsafa. Vilevile,



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 43 05/09/2021 15:40

fani huhusika na matumizi ya lugha, mtindo, muundo, wahusika na mandhari. Ninapenda kufafanua kidogo kuhusu utendaji wa fani na maudhui kwa kuwa ndivyo vipengele vinavyofanikisha kazi zangu. Ninaanza kwa kusimulia masuala yanayojitokeza katika maudhui. *Dhamira* hulenga kueleza kusudio la kutunga kazi yenyewe na taarifa zinazobebwa na dhamira hizo hujulikana kama *ujumbe*. *Falsafa* yenyewe ni imani ya mtunzi wakati *migogoro* huelezwa kama hali ya kutokuelewana baina ya pande mbili au zaidi.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Ili kufanikisha kazi zangu kwa kutumia fani, ninazingatia *matumizi ya lugha* yanayohusisha mpangilio wa maneno na tamathali za semi kama vile sitiari, tashibiha, kejeli, na kadhalika. Ninazingatia pia *mtindo* ambao ni upekee wa utunzi au uandishi. *Muundo* ni mjengo wa kazi yenyewe ilhali *mandhari* ni eneo ambamo kazi zangu zinatendeka. Aidha, ninatumia *wahusika* ambao wanaweza kuwa watu, miti au viumbe vinavyowakilisha watendaji katika kazi yenyewe. Kwa leo ninapenda kuishia hapo ili nisikuchoshe sana. Tukutane katika masimulizi yajayo yatakayohusu wanangu." *(Anamaliza na kuondoka.)*

## Maswali

1. Kulingana na masimulizi uliyosoma, fasihi ina dhima gani katika jamii?
2. Kuna tofauti gani baina ya fasihi na matawi mengine ya sanaa?
3. Kuna tofauti gani baina ya fani na maudhui?
4. Kwa nini msimuliaji anasema fani na maudhui ni sawa na pande mbili za shilingi moja?
5. Kwa kutoa mifano, elezea kipengele cha matumizi ya lugha katika kazi za fasihi.

FOR ONLINE USE ONLY

### Aina za fasihi

#### Kazi ya 3.2

*Soma sehemu ya pili ya masimulizi, kisha jibu maswali yanayofuata.*

*(Fasihi anaanza masimulizi yake ya sehemu ya pili kwa kuwarejesha wasikilizaji wake pale alipoishia katika masimulizi ya kwanza.)* "Katika masimulizi yaliyopita, nilisimulia juu ya maisha yangu, kazi zangu pamoja na kuwataja ndugu zangu. Katika sehemu hii, ninasimulia kuhusu watoto wangu na jinsi ninavyofanya kazi. Mungu amenijalia kupata watoto wawili; wa kwanza anaitwa *Simulizi* na wa pili anaitwa *Andishi*. Watoto hawa wamepewa majina haya kutokana na jinsi wanavyofanya kazi zao. Wote wawili, kama nilivyodokeza, wanamtumia *Fanani* kufanikisha kazi zao. *Simulizi* humtumia *Fanani* kufanya



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 44 05/09/2021 15:40

kazi zake na kuzifikisha kwa hadhira kwa njia ya masimulizi wakati *Andishi* humwelekeza *Fanani* kufanya kazi zake na kuzifikisha kwa hadhira kwa njia ya maandishi. Kwa ufupi, hao ndio wanangu ambao ninashirikiana nao katika kutimiza majukumu yangu.

Msione kama ninawachosha kwa maneno mengi. “Mvumilivu hula mbivu. Sasa ninawakaribisha wanangu niliowatambulisha hapo awali ili wajieleze kinagaubaga.” *(Simulizi anajieleza.)* “Mimi ninaitwa *Simulizi*; ni mtoto wa kwanza wa Mzee Fasihi. Mimi nililiona jua kabla ya mdogo wangu *Andishi*. Mungu hamtupi mja wake, nimebahatika kuzaa watoto wanne. Watoto wangu ni *Hadithi*, *Ushairi*, *Semi* na *Sanaa za Maonesho*. Ninaomba nimkaribishe mdogo wangu naye ajieleze.” *(Andishi anasogea karibu na kuanza kujieleza.)* “Awali ya yote, ninamshukuru Mungu kwa kuniwezesha kuwepo katika familia hii. Jina langu ni *Andishi*. Mimi nina watoto watatu tu ambao ni *Riwaya*, *Tamthiliya* na *Ushairi*.”

(*Fasihi anaendelea.*) “Hao ndio wanangu wawili, kama mlivyowasikia wakijieleza wenyewe. Watoto hawa wanafanana kwa baadhi ya tabia lakini kuna baadhi ya tabia wanatofautiana. Sasa nitawakaribisha ili waeleze tofauti zao.” (*Simulizi anaanza kujipambanua.*) “Mimi *Simulizi* huwasilishwa kwa mdomo na ninaweza kubadilika papo kwa papo. Pia, ninapenda kujitokeza kama tu Fanani na Hadhira watakutana kwa pamoja na ninapenda kumilikiwa na jamii nzima; kwa hiyo, mtunzi wangu hajulikani. Ninaweza kuhifadhiwa kichwani, redioni au katika video ingawa ni rahisi kupoteza sanaa yangu kwa kuacha ufundi fulani katika kunisimulia. Aidha, umbo langu ni sahili kwani ni ufupisho wa ukweli ulio wa moja kwa moja. Mwisho kabisa, ninapenda nyinyi nyote mjue kuwa mimi ndiye mkongwe katika familia yetu, kwani nilianza kuwepo tangu binadamu aanze kuishi duniani.”

(*Fasihi anaendelea.*) “Asante sana *Simulizi* kwa sifa zako nzuri. Sasa ninamkaribisha *Andishi* naye ajipambanue.” (*Andishi naye anaanza kujipambanua.*) “Tofauti na ndugu yangu, mimi hujitokeza kwa hadhira kupitia maandishi na si rahisi kubadilika papo kwa papo nikishaandikwa. Ninaweza kwenda popote peke yangu bila kumkutanisha Fanani na Hadhira. Mtunzi wangu hana pa kujificha na ninamilikiwa na mwandishi wangu. Kwa kuwa hifadhi yangu ni maandishi, siwezi kupoteza sanaa yangu ya awali. Aghalabu, muundo wangu huruhusu urejeshi katika mwendo wa utendaji wangu. Ninahisi nimeeleweka barabara. Ooh! Nilisahau sifa ya umri wangu; mimi si mkongwe kama ndugu yangu kwani nilianza kuwepo maandishi yalipogunduliwa.”



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 45 05/09/2021 15:40

## Maswali

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

1. Eleza kwa kutoa mifano tofauti iliyopo baina ya fasihi simulizi na fasihi andishi kwa kuzingatia vipengele vya umri, uhifadhi, uwasilishwaji, mabadiliko, na umiliki.
2. Fafanua uhusiano uliopo baina ya tanzu za fasihi simulizi na fasihi andishi zilizorejelewa katika masimulizi ya sehemu ya pili uliyosoma.
3. Kwa mujibu wa sehemu ya pili ya masimulizi uliyosoma, unadhani *Fanani* ni nani katika kazi ya fasihi?
4. Hadhira hufanya kazi gani kwa mujibu wa masimulizi ya sehemu ya pili?
5. Umejifunza nini kutokana na masimulizi ya sehemu ya pili?

### Tanzu za fasihi simulizi na vipera vyake

#### Kazi ya 3.3

*Soma sehemu ya tatu ya masimulizi, kisha jibu maswali yanayofuata.*

*(Fasihi anaendelea na masimulizi yake.)* "Leo ninasimulia kuhusu watoto wa mwanangu *Simulizi*. Simulizi ana watoto wanne ambao ni *Hadithi, Ushairi, Semi* na *Sanaa za maonesho*."

*(Fasihi aliwataka wajukuu wake wajieleze mmoja baada ya mwingine pamoja na kuwatambulisha watoto wao. Hadithi alianza kujieleza.)*

(*Hadithi anajieleza*.) "Mimi ni mtoto wa *Simulizi*. Ninaitwa *Hadithi*. Ili kufahamu zaidi kazi zangu, utatakiwa kufuatilia kwa kina kazi za wanangu ambao nao watajitambulisha hapa mmoja baada ya mwingine." (*Hadithi anawaita watoto wake*.) "Njooni hapa mjieleze wenyewe." *(Watoto wa Hadithi walijitokeza na kuanza kujieleza kama ifuatavyo:)*

FOR ONLINE USE ONLY

**Ngano:** Mimi ni hadithi fupi zinazosimuliwa ili kuwaasa watoto juu ya maadili ya jamii. Mara nyingi ninaanza kwa maneno *Paukwa ... Pakawa* na kuishia na *wakaishi kwa raha mustarehe*. Wahusika wangu ni watu, wanyama na miti. Ninatumika sana kwenye mazingira ya starehe na mapumziko.

**Tarihi:** Mimi ni hadithi fupi zinazosimuliwa kuhusu matukio ya kihistoria ambayo huweza kuwa ya kweli au ya kubuni. Mara nyingi wahusika wangu ni binadamu ambao hupewa uwezo mkubwa au mdogo kulingana na matukio yanayosimuliwa. Mimi hujitokeza kama hivi:



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 46 05/09/2021 15:40

***A***: *Kiangazi kiliunguza kikaunguza. Mwaka huo sitausahau maana jua lilitoka lote bila kubakia. Basi, siku moja, wakati jua linawaka vile, tukatahamaki wingu kubwa jeusi linatokea Mashariki. Tukapata matumaini. Loo! Kumbe ni balaa jipya, nzige. Wadudu wale ... uwasikie tu redioni. Omba usiwaone. Walitua kwenye mikuyu mtoni. Dakika tano zilikuwa nyingi, mikuyu ilikuwa vijiti. Hatimaye, Januari mwaka elfu, tisa mia hamsini na sita mvua zikaanza, japo kwa maringo lakini matumaini yakaanza kurejea.*

***B***: *Miaka thelathini ya uhuru wa Tanganyika ilileta mabadiliko. Yalikuja mengi, mengine yakadharaulika na kusahaulika, kasoro la mageuzi. Ooo! Lilishika kwa uhakika. Mijadala ikawa tele tele. Watu walisema wakasema. Si ghalibu watu kupata nafasi ya kutoa pumzi za ukweli, basi wakasema. Wengi walihofu mageuzi ya fujo. Wakayakataa kwa nguvu zote. Wanamageuzi wakaja juu kama moshi wa vifuu vya nazi. Wakatetea uhuru na haki bila vikwazo.* ***Chama kimoja hakitendi haki, kinalala bila mpango*** *... Huu ukawa ndio msimamo walioubeba mgongoni na mabegani. Kauli zao zilichoma akilini kama miiba kidondani na kuchonyota kama upupu mwilini.*

*Hatimaye, mwafaka ulipatikana. Vyama vingi karibuni Tanzania! Waungwana wakashikana mikono kuonesha amani. Wengine walilaani tume. Walisema tume ilitumia fedha ambazo zingetumiwa kwa shughuli za maendeleo. Walidai kuwa hapakuwa na lazima ya kugharimia tume ili iwaulize wananchi kuwa wanataka haki zao au la!*

**Visasili:** Mimi ni masimulizi yanayoeleza asili au chimbuko la watu. Wengine wananiita hadithi za kale zenye kuwakilisha imani na mtazamo wa jamii inayohusika kuhusu asili ya ulimwengu na mwenendo wake, asili yao wenyewe, maana na shabaha yao wenyewe. Sifa yangu kubwa ni kueleza ukweli tofauti na walivyo ndugu zangu wa visa vya kubuni. Nimeenea sehemu kubwa. Mimi hujitokeza namna hii:



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 47 05/09/2021 15:40

***Asili ya watu kufa***

*Hapo zamani za kale, baada ya kuumbwa ulimwengu na vitu vyote ndani yake, vikiwa pamoja na watu, Mungu alifikiria sana juu ya uhai wa wanadamu. Akawa anatatizika katika kuamua iwapo wanadamu waishi milele na milele bila kufa, kama yeye, au wafe baada ya kuishi ulimwenguni kwa muda. Hatimaye, akawatuma viumbe wawili kumwambia mwanadamu afanye uamuzi wake mwenyewe kuhusu jambo hili.*

*Kwanza alimtuma kinyonga na kumpa ujumbe huu: "Mmeambiwa msizaane, mbaki nyinyi wawili tu ulimwenguni, mke na mumewe, na msife milele na milele."*

*Kinyonga akaupokea ujumbe na kuelekea ardhini. Kisha Mungu, nyuma, akamtuma Njiwa na ujumbe huu:*
*"Mmeambiwa mkitaka, mzaane, kisha mfe. Mkifa, uhai utaendelezwa na watoto, wajukuu, vitukuu, vilembwe, vilembwekeza, vinying'inya, na vinying'inyiza wenu. Kwa jinsi hiyo, ijapokuwa nyinyi wenyewe mtakufa, uhai hautaisha duniani. Utadumishwa na hao mtakaowazaa na watakaowazaa. Nanyi mtakumbukwa milele na milele."*

*Kinyonga, kama itakavyokumbukwa, alitumwa yeye mwanzo; lakini kwa sababu ya mwendo wake wa mbele na nyuma, akafika kwa wakati sawasawa na njiwa. Akaanza kutoa ujumbe wake ambao, japo ulikuwa mfupi, hakuuwasilisha haraka kwa sababu, jambo la kwanza, yeye aligugumiza. Pili, alirudiarudia maneno kiasi cha kuchosha. Hivyo basi, wanadamu walipoona kinyonga anachelewesha kuwasilisha ujumbe wa Mungu, wakamkemea na kumcheka. Wakamwambia njiwa atoe ujumbe*



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 48 05/09/2021 15:40

*wake kabla ya kinyonga kufanikiwa kufanya hivyo. Chapuchapu Njiwa akatoa ujumbe wake, japo ulikuwa mrefu. Wakausikiliza kwa makini, wakaona kuwa ni ujumbe mzuri, wakaukubali.*

*Walipoukubali tu, kinyonga naye akahitimisha kuwasilisha ujumbe wake. Huo wakauona ni mzuri zaidi, na hivyo wakataka kubadilisha uamuzi wao. Hapo sauti ya Mungu ikasikika ikisema kwamba kubadilisha haiwezekani, sababu alikuwa amekwishapokea tayari uamuzi wao, na alikwishaukubali. Walipotaka kuuliza maswali, sauti hiyo ikatoweka ghafla. Ikawa sasa ni kujilaumu wenyewe na kuwalaumu viumbe wale wawili, hasa kinyonga, kwa kigugumizi chake na mwendo wake wa polepole. Hata hivyo, lawama zao hazikufua dafu. Kikomo chao kikawa kimeshafungwa. Wakawa hawana budi kuzaana na kufa.*

**Vigano:** Mimi ni hadithi fupi zinazoelezea makosa au uovu wa watu fulani na kueleza maadili yanayofaa; na aghalabu hutumia sana methali na nahau katika kutoa mafunzo kwa hadhira. Lengo langu ni kuadilisha; hivyo, ninawatumia wahusika binadamu au wanyama. Katika hali halisi mimi niko hivi:

***Fisi aadhibiwa***

*Hapo zamani katika mbuga za Rijeni wanyama walikutana kwa siri kujadili uovu wa Fisi. Walikutana kwa siri kwa sababu walijua wanyama wakali kama Simba, Chui, na Fisi walikuwa na hamu kubwa ya kuwashambulia na kuwala. Swala alikuwa kiongozi wa mkutano na akawaambia wenzake, "Jamani, uonevu umezidi. Juma lililopita watoto wawili wa Kongoni waliliwa na Chui; tena Chui alisema hakushiba. Alitaka sana amshike Kongoni ili amle lakini Kongoni aliwahi kukimbia. Juzi mwanangu ameliwa na Fisi. Nilimpiga teke jichoni lakini bado sikufanikiwa kumwokoa mwanangu; nikakimbia. Sasa tufanyeje?"*



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 49 05/09/2021 15:40

*Basi wanyama walijadili kwa uchungu na kwa muda mrefu. Wote walitaka sana Chui na Fisi wauawe haraka. Tatizo lao kubwa lilikuwa jinsi ya kuwaua. Wengine walishauri kuwa waovu hao wategwe kwa mitego ya kamba, kisha wapofuliwe. Hata hivyo, ilionekana bado ni hatari.*
*Hatimaye, Sungura alitikisa masikio yake na kusema, "Kazi ya kuwaua niachieni mimi. Nipeni siku saba nitawaeleza na kuwaonesha nitakachokifanya." Basi mkutano ukafungwa kwa kumkubalia Sungura afanye kazi hiyo. Usiku ulipoingia, Sungura alikoka moto nje ya nyumba yake. Moto ulipokolea vizuri akatia jiwe moja ndani ya ule moto. Jiwe hilo lilikuwa na ukubwa wa mpira wa tenisi. Sungura akaongeza kuni mekoni halafu akaenda kumtafuta Fisi pangoni mwake.*

*Sungura alipofika mlangoni mwa pango alisema, "Hodi kwa mzee Fisi!" Fisi alifurahi moyoni kwa sababu aliijua ile sauti ya Sungura na alijua kuwa Sungura angeweza kuwa chakula chake. Fisi hakujibu haraka. Kwa hiyo, Sungura akasogea mlangoni na kubisha tena hodi. Hapo ndipo Sungura alipojikuta makuchani mwa Fisi! Sungura akaona kifo waziwazi. Sungura akamwambia, "Rafiki yangu mzee Fisi, vipi leo? Ninakuletea habari nzuri halafu unanikamata!" Fisi akasema, "Mimi nina njaa ya siku nne halafu unadai kuwa umeniletea habari nzuri? Wewe ni riziki yangu." Sungura akampoza, "Hata kama utanila hutashiba. Mimi nimekuja nikukaribishe kwangu. Huko kuna nyama tele." Fisi alifurahi na kucheka huku akimwachia Sungura. "Haya ongoza njia. Tena uongeze mwendo, siyo ule mwendo wako wa sisimizi."*

*Sungura na Fisi walifika nyumbani kwa Sungura huku mate yakimtoka Fisi kwa hamu ya nyama. Hapo Sungura akapanga vitimbi vyake; akasema, "Mzee Fisi, nyama ziko nyingi lakini hizi ni nyama za tambiko. Kwa desturi za kwetu, mnofu wa kwanza nitakulisha mimi mwenyewe; mradi ulale chali na ufumbe macho. Baada ya hapo nyama nyingine utakula kwa mikono yako." Kabla Sungura*



FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE
FOR ONLINE USE ONLY

*hajamaliza, Fisi alikwishalala chali na kufungua mdomo huku akiwa amefumba macho.*

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Sungura alicheka kimoyomoyo akatwaa kibanio, akabana lile jiwe la moto na kulitumbukiza mdomoni mwa Fisi. Kwa kuwa Fisi alikuwa amejiandaa kumeza nyama, alilimeza jiwe haraka sana. Looo! Fisi aliungua koo, kifua na tumbo. Fisi alibiringika akilia sana na kujitupa huku na huko hadi akakata roho.*

**Soga**: Mimi ni hadithi fupi zinazosimuliwa kwa nia ya kuchekesha na kukejeli hali inayohalisika kwa kusema ukweli unaoumiza na kuujengea kichekesho ili kupunguza ukali wa ukweli huo. Nitazame ninavyojitokeza hapa chini.

*Amini usiamini, haya ndiyo yaliyowasibu wanafunzi hawa. Majuto alikuwa Majuto kweli! Sikudhani ndio usiseme. Walikuwa na akili kama kompyuta. Tukipewa kazi ya kufanya darasani, wao ni sekunde tu wamemaliza. Akili zao zikawapa kiburi; hivyo hawakutaka kushirikiana na sisi. Muda wote walijitenga wakituona kama vinyago. Wapi bwana! Acha Mungu aitwe Mungu. Tuliweka mikakati ya kuhakikisha kwamba na sisi hatubaki nyuma. Tukasoma kwa bidii na siku ya mtihani ilipowadia sote tuliufanya kwa umakini mkubwa. Majuto na Sikudhani hawakuwa na shaka kwani waliamini kuwa hakuna yeyote aliyeweza kuwashinda.*

*Wahenga walisema, Mungu si Athumani. Kibao kiligeuka kwani wote tuliokuwa na ushirikiano tuliweza kufanya vizuri sana. Majuto na Sikudhani wakajikuta wameangukia pua. Hawakuamini kilichowatokea. Acha Mbiti awashambulie! "Nendeni mkamwone mwalimu. Haiwezekani wanafunzi wenye akili kama ninyi mpate daraja D; haiwezekani! Hata hivyo, kabla hamjaenda kumwona, yawapasa kujitafakari ili mjue ni kwa nini hamkufanya vizuri."*

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 51 05/09/2021 15:40

(*Fasihi alisema.*) "Sasa ni zamu ya ushairi, karibu!" (*Ushairi anajieleza.*) "Mimi wananiita Ushairi, mtoto wa Simulizi. Mimi huwafikia hadhira kwa njia ya uimbaji au kughani kupitia wanangu. Ninaomba kila mmoja ajieleze mwenyewe. Mashairi ninaomba uanze."

FOR ONLINE USE ONLY

**Mashairi:** Mimi nina mpangilio maalumu wa maneno wenye ruwaza mahususi ya silabi, lugha ya mkato na ya kinudhumu. Ninajipambanua kwa urari wa vina na mizani kwenye mapokeo na wakati mwingine sina urari wa vina na mizani kwenye usasa. Mimi hujitokeza tofautitofauti.

Pale ninapofuata urari wa vina na mizani ninaonekana hivi:

*Nchi yetu Tanzania, ina vingi vya thamani,*
*Madini twajichimbia, tena yalo ya thamani,*
*Hifadhi za kuvutia, mazao mengi shambani,*
*Tuipende nchi yetu, tudumishe uzalendo.*

*Uzalendo wetu kwanza, nchi yetu kuilinda,*
*Wasije wakatuponza, tukabaki tumepinda,*
*Mali zetu wakifyonza, nchi haiwezi kwenda,*
*Tuipende nchi yetu, tudumishe uzalendo.*

Pale nisipofuata urari wa vina na mizani ninaweza kuonekana hivi:

*Ukinitunza vizuri, na mimi nitakutunza,*
*Hewa nitakupatia, kivuli na dawa pia,*
*Mimi wa muhimu sana, katu usiniangamize,*
*Usinichome kwa yako tamaa, utakosa vitu vingi,*
*Mifugo yako punguza, ufuge kwa utaratibu,*
*Nisije kukasirika, yakakukuta majanga.*

FOR ONLINE USE ONLY

**Tenzi**: Mimi nina mpangilio wa silabi zinazolingana kwa kila mstari. Aghalabu, maudhui yangu huwa ya kihistoria yenye kuadilisha au kuadibu katika muundo wa usimulizi. Mimi huonekana namna hii:

*Leo nataka binti,*
*Ukae juu ya kiti,*
*Ili uandike hati,*
*Ndogo ya wasia.*



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 52 05/09/2021 15:40

*Mimi kwako ni baba,*
*Hati hii ya huba,*
*Andika iwe akiba,*
*Asaa itakufaa.*

*Bado ungali kijana,*
*Na dunia ngumu sana,*
*Kukufunza kuona,*
*Ni jambo la welekea...*

*Hati hii ni lulu,*
*Iweke utafaulu,*
*Wema hawatakuhulu,*
*Baraka kukuombea...*
*(Shaaban Robert)*

**Chanzo**: *Tenzi Tatu za Kale (Mulokozi, 2002:103)*

**Ngonjera**: Kama mlivyomsikiliza ndugu yangu Mashairi, nami nina tabia sawa na zake. Tofauti yetu ndogo ni kwamba mimi huwa ni mazungumzo baina ya watu wawili au zaidi, hasa yahusuyo mjadala au malumbano yenye kusudi la kutoa ujumbe maalumu. Ninajitokeza namna hii:

*Juma:* *Rafiki nakueleza, rushwa ni mti mkavu,*
*Jana nilipokamatwa, kidogo niwekwe ndani,*
*Nikawaza kuwazua, napaswa nifanye nini?*
*Ndipo mawazo yakaja, kuuzunguka mbuyu.*

*Amani:* *Rafiki unanikwaza, nyuma 'naturudisheni,*
*Twatangaza uzalendo, kuacha ya uhaini,*
*Rushwa adui wa haki, kamwe usiendekeze,*
*Ukifuata sheria, mambo yatawa murua.*

*Juma:* *Ni kweli uyasemayo, lakini yatulazimu,*
*Kuweza kujinusuru, vema unyoshe mkono,*
*Mambo huwa ni magumu, wakubwa wakikubana,*
*Ndiyo mana ni muhimu, kuwapa ili yaishe.*

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE
FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 53
05/09/2021 15:40

*Amani:* *Kamwe sitakushauri, mbuyu kuuzunguka,*
*Ungeilipa kwa haki, mapato ya serikali,*
*Miundombinu ingejengwa, sote tungenufaika,*
*Kuliko kunufaisha, yeye aliye mmoja.*

*Juma:* *Macho umenifumbua, ujinga umenitoka,*
*Jamaa kanifaidi, pesa yangu amekula,*
*Barabara bado mbovu, twazipita kwa taabu,*
*Sitatoa tena rushwa, mmoja kunufaisha.*

*Wote:* *Tuungane kwa pamoja, sauti yetu kupaza,*
*Rushwa hukiuka haki, maendeleo kukwama,*
*Wachache wanufaika, taifa kutokusonga,*
*Tukiitokomeza rushwa, uchumi tutainua.*

FOR ONLINE USE ONLY

**Nyimbo**: Mimi nina mpangilio maalumu wa maneno na mahadhi, yaani kupanda na kushuka kwa sauti. Mimi huimbwa nikiambatana na mapigo ya ala; japo si lazima. Jambo la msingi kwangu ni kuwapo kwa sauti.





KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 54 05/09/2021 15:41

*Haya shime wananchi tulime,*
*Kilimo, kilimo, kilimo ufalme,*
*Shime, tulime shime tulime x2*

*Mazao aina zote tulime,*
*Ya biashara na chakula tulime,*
*Shime, tulime shime tulime x2*

**Maghani**: Mimi husemwa au hughaniwa kwa sauti fulani ambayo ipo kati ya uzungumzaji na uimbaji. Pia, hutolewa kwa kutumia mapigo ya mwendokasi na sauti hupangiliwa ili kuleta ladha na maana. Ufuataо ndio mwonekano wa umbo langu:

*Mimi ni Simba wa nyika, mfalme wa wanyama,*
*Nina nguvu ya kutisha, dunia yanitambua.*

*Kwenye uwanja wa vita, kupambana ninaweza,*
*Kawaulize wenzangu, msituni wanijua.*

*Ningurumapo nyikani, ardhi hutetemeka,*
*Naomba ukae mbali, nisijekukurarua.*

*(Semi anayapokea mazungumzo na kuendelea.)*
"Mimi ninaitwa Semi, ni mtoto wa *Simulizi*. Nimejaliwa kupata watoto saba. Nitawaita watoto hao waeleze maumbo yao." (*Watoto wa Semi wanakuja na kuanza kujieleza*.)

**Methali**: Mimi huundwa kwa mpangilio wa maneno unaoonesha pande mbili za fikra. Kazi yangu kubwa ni kutoa hekima na busara kwa watu. Hujitokeza kama hivi:

*Asiyesikia la mkuu, huvunjika guu.*
*Aliyekupa kiti, ndiye aliyenipa kumbi.*

**Misemo**: Mimi ni kauli za jumla zenye ukweli zinazotumiwa kusema mambo mbalimbali yanayoafiki ukweli huo. Kwa kawaida, mimi huwa nina upande mmoja, yaani kauli inayotoa ukweli au hoja fulani. Kauli hiyo haioneshi ukinzani au kuijenga kauli nyingine. Sura yangu ina mwonekano huu:

*Mtu kwao, Akili ni mali, Mtu ni utu, Misitu ni uhai, Mtu ni afya, Akiba haiozi, Kilimo cha kufa na kupona.*

FOR ONLINE USE ONLY

**Nahau**: Mimi ni semi zinazotumia maneno ya kawaida lakini hutoa maana tofauti kabisa na ile iliyomo kwenye maneno hayo. Ninatumia lugha ya picha na tamathali za semi. Tazama hapa chini ninavyojitokeza:

*Tobuti ana mkono wa birika (bahili),*
*Bakari amepata jiko (ameoa),*
*Kisaka amepiga maji (amekunywa pombe); na*
*Hapa Kubikwa amekata mguu (haji tena hapa).*

**Mafumbo**: Mimi ni kauli zisizoeleza maana waziwazi. Mara nyingi ninatumia lugha ya picha. Ninatolewa kwa uficho ili kuwafikirisha wasikilizaji na kupunguza watu watakaoelewa. Kwa mfano, ukikuta wasichana wawili wamekaa wanapiga soga na mmoja wao hakujisitiri vizuri, basi unaweza kusema, *Jamani mchele umemwagika au tumbili wanakula mahindi*. Kwa kuwa kauli hizi hazihusiani na ukaaji wao pale, wale wasichana wataangaliana na hatimaye asiyejisitiri vizuri atajirekebisha.

**Mizungu**: Mimi ni semi zenye picha za mafumbo zinazoonesha ukinzani wa fikra au tukio. Ukinzani husaidia kumfikirisha msikilizaji jambo ambalo humpa changamoto ya kutafuta jibu. Ukisikia sentensi kama: *miti yote nitakwea, mtarawanda umenishinda* au *papai limeiva nyumbani ila nashindwa kulila,* ujue ni mimi Mizungu.

**Lakabu**: Mimi ni majina ya kupanga yasiyo halisi ambayo mtu au watu hujipa au hupewa kutokana na sifa walizonazo. Sifa hizo zinaweza kuwa za kimaumbile, kiujuzi, kimatendo na nyinginezo. Hujitokeza kama hivi: *Baba wa Taifa (Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere), Simba wa vita (Mzee Rashid Mfaume Kawawa).*

**Vitendawili**: Mimi ni semi zilizofumbwa ambazo hutolewa kwa hadhira ili iweze kuzifumbua. Kwa kawaida, fumbo huwa linafahamika katika jamii inayohusika na huwa na mafunzo mahususi katika jamii hiyo. Ninatumia mafumbo yenye sanaa ya hali ya juu ambayo huwachemsha bongo washiriki. Ili mshiriki aweze kufumbua kitendawili, huhitaji kutambua, kuhusisha na kulinganisha vitu vya aina mbalimbali vilivyomo katika mazingira. Mifano yangu ni kama ifuatayo:

*Nakunywa mchuzi, nyama natupa (muwa), popo mbili zavuka mto (macho).*



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 56 05/09/2021 15:41

(*Fasihi anaendelea.*) "Haya sasa, hayawi hayawi huwa. Hatimaye, ninamwita mtoto wa mwisho wa Simulizi. Huyu ana watoto wengi kuliko ndugu zake wote. Huyu si mwingine bali ni Sanaa za maonesho. Haya, sasa uwanja ni wako."

(*Sanaa za maonesho anajieleza.*) "Mimi ninaitwa Sanaa za maonesho. Mimi huwasilisha mawazo ana kwa ana kwa kutumia utendaji ambao hufungamana na dhana inayotendwa (tukio), mtendaji (fanani), uwanja wa kutendea (jukwaa), watazamaji (hadhira), na kusudio (maudhui). Nimejaliwa kupata watoto tisa. Ninaomba tuwasikilize."

**Maigizo**: Mimi hutumia watendaji kuiga tabia na matendo ya watu au viumbe wengine kwa lengo la kutoa burudani au funzo fulani. Huambatana na nyimbo, vichekesho, masimulizi ya hadithi na kazi zingine za kijadi kama vile, harusi pamoja na jando na unyago.

**Michezo ya Watoto**: Mimi ni sanaa zenye usanii ambao hujibainisha katika nyimbo, majibizano, vitendo na maigizo yanayofanywa na watoto.

**Vichekesho**: Mimi ni maigizo mafupi yanayokusudiwa kufurahisha na kuchekesha hadhira. Pia, huwa ninaonesha jambo au tatizo kwa njia ya uchekeshaji bila kulichambua kwa kina. Mimi hutoa vichekesho vifupi visivyo na uchambuzi wa kina kuhusu kisa kinachooneshwa. Ninatumia wahusika, lugha ya picha na tamathali za semi.

**Majigambo**: Mimi hujigamba ama kujitapa kwa kufanya jambo la kishujaa au lisilo la kawaida. Huwa ninasimulia na kutenda kwa mikogo huku nikionesha jinsi nilivyofanya jambo fulani. Mara nyingi ninaambatana na nyimbo za ngoma za makabila. Mimi hujitokeza namna hii:

*Mtambaji:* *Nani asonijua hapa?*
*Mkulima stadi mie ... mie!*
*Naam! Chakula changu jembe,*
*Nyumba yangu jembe,*
*Usingizi wangu jembe ...*
*Msimu ulopita si mliniona?*
*Pori nililaza upeo wa macho.*
*Shabash! ... Nyumbani nikawa sirudi ...*



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 57 05/09/2021 15:41

*Nalala hukohuko ...*
*Mvua mmmh! Nikapanda mie na wanangu ...*
*Sasa tumevuna au mwasemaje ...?*
*Mkulima mmmh!*

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Ngonjera**: Mimi ninaigizwa kwa kutumia mashairi. Nina pacha wangu ambaye ni mtoto wa *Ushairi*. Mimi na pacha wangu hatuna tofauti yoyote katika mwonekano na utendaji wetu. Huu hapa chini ndio mwonekano wangu.

***Nani afanye nini?***

*Anita:* *Kaka kusanya sahani, walizolia wazazi,*
*Kisha udeki jikoni, halafu menya viazi,*
*Pia utachanja kuni, ukaazime na mbuzi,*
*Mimi nakwenda bombani, nitapitia na nazi.*

*Abaya:* *Dada nakusihi koma, kazi hizo kazi zako,*
*Tena kuwa na heshima, viache vyako vituko,*
*Sifanyi kazi za mama, kwetu wanaume mwiko,*
*Nakataa ninasema, hata iwe kwa viboko.*

*Anita:* *Hakuna kazi ya kike, wala kazi ya kiume,*
*Maji kichwani jitwike, nami kuwinda nivume,*
*Tena jikoni upike, acha kasumba udume,*
*Na chungu ukainjike, hakuna cha mwanamume.*

*Abaya:* *Mwanamume kutafuta, akina dada kupika,*
*Kuwinda bila kusita, kidume kupapatika,*
*Sisi kupigana vita, kilimoni kutumika,*
*Kazi yenu ni kusuta, umbea mmefurika.*

*Anita:* *Ninakupa pole sana, kwayo imani potofu,*
*Nakueleza bayana, akili kama ya pofu,*
*Hebu acha kutukana, kuwa kaka mnyoofu,*
*Acha kabisa kutuna, kujizolea wasifu.*

*Abaya:* *Sijizolei wasifu, nakueleza ukweli,*
*Ninyi kwetu wahafifu, tepetepe yenu mili,*
*Hali zenu tahafifu, acha kataa kubali,*
*Pole kwa kuwakashifu, ila nakupa ukweli.*

FOR ONLINE USE ONLY

*Anita:* *Sisi sote wakulima, mazao tunazalisha,*
*Kila kazi tunavuma, kwa hili acha kubisha,*
*Vilivyo tunajituma, pengine hadi kukesha,*
*Masomo tunayasoma, ngazi zote tunatisha.*

*Ulimwengu kutufunda, wayaona maajabu,*
*Kwa sayansi si makinda, tunapata na majibu,*
*Imelia parapanda, hatuwezi jitanibu,*
*Mapambano kwa viwanda, maendeleo jawabu.*

*Abaya:* *Usemacho dada kweli, haupo mfumo dume,*
*Tupo sawa zetu hali, sote kazi tujitume,*
*Twajidunisha kimali, eti kisa wanaume,*
*Kabisa nimekubali, wenzangu tusitutume.*

*Leo umenifundisha, sasa nitawajibika,*
*Dhana udume komesha, kazi zote kufanyika,*
*Si vyombo tu kuviosha, na kupika nitapika,*
*Jikoni nitasafisha, moyoni sitokwazika.*

**Chanzo**: *Uduni wangu: Ngonjera za Watoto (Mbijima, 2020: 10-11)*

**Utani**: Mimi hupenda kufanyiana mizaha au masihara kwa watu ninaohusiana nao. Utani wetu huwa mahali popote. Yaweza kuwa msibani, harusini, au sehemu za kazi. Utani wetu unaweza kuwa kati ya mtu na mtu, ukoo na ukoo au kabila na kabila; kwa mfano, Wagogo na Wasukuma, au Wachaga na Wapare.

**Miviga**: Mimi hutumika kwenye sherehe za kijamii zinazofanywa katika kipindi maalumu cha mwaka na katika muktadha mahususi. Sherehe hizo zinaweza kuwa jando na unyago, harusi, au kutawazwa kwa mtemi. Mara nyingi ninaambatana na nyimbo na maigizo yanayohusiana na tukio linalohusika.

**Matambiko**: Mimi hujulikana kama ibada na utoaji wa sadaka kwa Mungu, miungu au mizimu. Hufanyika katika mazingira maalumu na huzingatia vipengele kama mavazi maalumu (yajulikanayo kama maleba), umri na lengo maalumu.

**Ngomezi**: Mimi ni sanaa ya kuwasiliana kupitia midundo ya ngoma. Mawasiliano yetu hubeba taarifa za matukio mbalimbali katika hali ya mafumbo kiasi kwamba jamii inayohusika ndiyo tu huweza kubaini maana ya midundo inayosikika.



FOR ONLINE USE ONLY

*(Baada ya watoto wa Sanaa za maonesho kujieleza, Fasihi alidakia na kusema,)* "Kila lenye mwanzo halikosi kuwa na mwisho. Nimekueleza kwa kina na uwazi kuhusu familia yangu. Utakumbuka kuwa nimewaelezea wanangu lakini nikajikita zaidi katika kufafanua uzao wa mwanangu wa kwanza aitwaye Simulizi. Ni matumaini yangu kuwa ulikuwa na hamu ya kusikia juu ya mwanangu Andishi. Usikose kufuatilia masimulizi juu yake kwa siku zijazo ili naye umfahamu kwa undani."

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maswali

1. Umepata maarifa gani kuhusu tanzu na vipera vya fasihi simulizi kutokana na masimulizi uliyoyasoma?
2. Maarifa uliyoyapata katika masimulizi haya yatakusaidiaje katika maisha yako ya kila siku?
3. Fafanua kufanana na kutofautiana kwa vitendawili na mizungu.
4. Eleza tofauti iliyopo baina ya methali na misemo.
5. Methali zina faida gani katika jamii?

**Zingatia**

Fasihi simulizi ina tanzu nne ambazo ni hadithi, ushairi, semi, na sanaa za maonesho. Kila utanzu una vipera kadhaa kama inavyoonekana kwenye kielelezo namba 3.2. Kumbuka kuwa Fasihi simulizi ikihifadhiwa kwenye maandishi au maumbo mengine, hupoteza ushirikishwaji wa hadhira na uwezo wa kupokea mabadiliko ya papo kwa papo. Wakati mwingine hadithi za masimulizi yaliyoandikwa hutatanisha wasomaji kwani hudhani kuwa ni Fasihi Andishi. Baadhi ya sifa zinazotambulisha kazi za usimulizi ni **mianzo** kama vile, *paukwa* ... au *kitendawili* ... na **miisho** kama vile, *na hadithi yangu inaishia hapo* au *wakaishi raha mustarehe*. Aghalabu, masimulizi hufuata mtiririko sahili na wa moja kwa moja. Baadhi ya fasihi simulizi huanza kuandikwa lakini si kwa makusudio ya kusomwa. Mara nyingi nyimbo za kwaya, taarabu na nyimbo za bendi huanza kwa kuandikwa na kupangiwa noti za kimuziki; hata hivyo, huwa kwa makusudi ya kufanyia mazoezi tu. Lengo la kazi hizi ni kuwasilishwa kwa njia ya sauti na utendaji na si kwa kusomwa.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 60 05/09/2021 15:41

**Fasihi simulizi**

| Hadithi | Ushairi | Semi | Sanaa za maonesho |
|---|---|---|---|
| Ngano | Mashairi | Methali | Michezo ya watoto |
| Tarihi | Tenzi | Misemo | Vichekesho |
| Visasili | Ngonjera | Nahau | Majigambo |
| Vigano | Nyimbo | Mafumbo | Ngonjera |
| Soga | Maghani | Vitendawili | Maigizo |
| | | Mizungu | Utani |
| | | Lakabu | Matambiko |
| | | | Miviga |
| | | | Ngomezi |

**Kielelezo namba 3.2:** *Tanzu za fasihi simulizi na vipera vyake*

## Kazi ya 3.4

*Chunguza picha ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*





KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 61 05/09/2021 15:41

## Maswali

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

1. Watu wanaoonekana katika picha wanafanya nini?
2. Hicho wanachofanya kinaweza kuwekwa katika kipera gani cha fasihi simulizi? Eleza kwa nini unafikiri hivyo?
3. Fafanua mandhari yanayoweza kutumika katika uwasilishwaji wa kazi hiyo.
4. Wahusika wake wanaweza kuwa wa kundi gani la umri?
5. Je, wanafunzi wanaweza kujiunga na kundi hilo au lingine lolote? Eleza sababu za jibu lako.

### Usimulizi wa hadithi

**Kazi ya 3.5**

1. Wasimulie wanafunzi wenzako hadithi yoyote uliyowahi kusimuliwa na mtu au kusikia ikisimuliwa mahali fulani, kisha useme ni hadithi ya kipera gani.
2. Fafanua ujumbe unaopatikana katika hadithi uliyoisimulia.

**Kazi ya 3.6**

*Soma ngano ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Paukwaa …! Pakawaa …! Paukwaa …! Pakawaa! Hapo zamani za kale alikuwepo Mfalme aliyeitwa Kizito. Mfalme Kizito alioa na kupata mtoto wa kike aliyeitwa Chaurembo. Mtoto huyo alikua na kuwa binti mkubwa na mrembo. Binti huyo alisifiwa na kila mtu katika milki yote ya Mfalme Kizito kwa urembo wake. Siku moja walijitokeza marafiki wawili, Bwege na Kanjanja, kwenda kumchumbia Chaurembo ambapo kila mmoja alitaka kumwoa. Bwege alikuwa na umbo kubwa la miraba minne na miguu mirefu kama mlingoti. Kanjanja alikuwa na umbo dogo kama mbilikimo. Marafiki hao walianza kuoneana gere kwani kila mmoja alitaka kumwona Chaurembo.

FOR ONLINE USE ONLY

Kila mmoja, kati ya wale marafiki wawili, alipitia mlango wa nyuma na kwenda nyumbani kwa Mfalme Kizito ili kumposa bila ya mwenziwe kujua. Mfalme aliposikia vile aliamua kupiga mbiu kwa ajili ya mkutano wa wananchi wote. Mfalme aliwajulisha lengo la kuitishwa kwa mkutano huo kuwa ni posa ya bintiye na kuoneshwa waposaji hao, Bwege na Kanjanja. Waposaji hao wote walikuwa ni marafiki. Kila mmoja alipigwa na butwaa kuona wanamgombania binti mmoja. Mfalme alisema, "Mtaka cha uvunguni, sharti ainame. Ili binti yangu aolewe sharti waoaji watembee kuzunguka mipaka ya ufalme wangu. Atakayekuwa wa kwanza ndiye atakayemwoa binti yangu."



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 62 05/09/2021 15:41

Kusikia vile, Bwege alimcheka Kanjanja na kuuliza, "Haka kadubwasha ndiko kanaweza kushindana mwendo na mimi?" Asijue kwamba "Ukubwa wa pua si wingi wa makamasi." Siku ilipowadia, Bwege alijiandaa na Kanjanja alijiuliza, "Nitafanya nini ili nifike mapema?" Lilimjia wazo zuri na akaamua kuwa atatoka kwake mapema kabla ya siku yenyewe na kukaa kwenye ukumbi wa Mfalme. Atavaa mavazi yaliyofanana na nyasi mbichi. Hivyo, hataweza kuonekana vizuri. Siku ilipowadia, Bwege alianza kutoka mbio akazunguka himaya yote. Alifika kwenye ukumbi ule uliojaa watu akiwa choka mbaya. Alipoangaza macho huku na kule hakumwona Kanjanja. Alianza kufurahi akidhani kwamba hajafika. Kwa hiyo, alihisi yeye ndiye atakayekuwa mshindi.

Alipotaka tu kukaa kwenye nyasi, alisikia sauti ya Kanjanja ikimuuliza, "Mbona unataka kunikalia?" Bwege aliposikia sauti ile ya Kanjanja alisinyaa, akawa kondoo. Aliimba kwa sauti ya huzuni,

"Ningekuwa kwetu, aaaiiiiiiii! x 2
Ningekuwa kwetu, kwetu Mirumbani ningemlilia mama,
Ningemlilia mama! x 3
Ningekuwa kwetu, aaaiiiiiiii! x 2
Ningekuwa kwetu, kwetu Mirumbani ningemlilia mama,
Ningemlilia mama! x 3"

Aliona kwamba tayari amemkosa mke kwa kuchelewa kufika. Hapo Mfalme Kizito alisimama, na Kanjanja akachaguliwa kwa kufika mapema na kuozeshwa binti wa mfalme. Kanjanja alifurahi sana kwa kuona amemshinda mshindani wake kwa kutumia ujanja wa kujibadilisha rangi na kufanana na majani mabichi. Hapo Kanjanja akaanza kubadili nguo za rangi za kila aina hadi leo. Mpaka sasa Kanjanja na mkewe wanaishi kwa furaha.

## Maswali

1. Unafikiri tabia za Kanjanja zinafanana na tabia za mnyama gani?
2. Ungekuwa wewe ndiye Kanjanja, ungetumia mbinu gani kumshinda mpinzani wako?
3. Hakiki vipengele vifuatavyo vya lugha kama vilivyotumika katika ngano uliyosoma.
   (i) methali
   (ii) nahau
   (iii) dhihaka

FOR ONLINE USE ONLY

**Zingatia**

Hadithi ni maelezo yenye mtiririko wa moja kwa moja ambayo yanahusisha visa katika matukio mbalimbali. Mara nyingi visa hivyo ni vya kubuni. Hushirikisha wahusika kama vile binadamu, wanyama, ndege na vitu vingine vya kufikirika. Mianzo ya hadithi huanza na *"Hadithi! Hadithi!"* na hadhira huitikia *"hadithi njoo, ukweli njoo, utamu kolea!"* Mara nyingi miisho ya hadithi huwa *"wakaishi kwa raha mustarehe"* au *"hadithi yangu imeishia hapo"*. Mambo yanayopaswa kuzingatiwa wakati wa masimulizi ya hadithi ni matamshi sahihi, mpangilio mzuri wa mawazo, matumizi ya lugha, na urefu wa mazungumzo.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Uhakiki wa kazi za fasihi simulizi

### Kazi ya 3.7

*Soma mashairi yafuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Shairi A**

*Nchi yetu Tanzania, ina vingi vya thamani,*
*Madini twajichimbia, tena yalo ya thamani,*
*Hifadhi za kuvutia, mazao mengi shambani,*
*Tuipende nchi yetu, tudumishe uzalendo.*

*Uzalendo wetu kwanza, nchi yetu kuilinda,*
*Wasije wakatuponza, tukabaki tumepinda,*
*Mali zetu wakifyonza, nchi haiwezi kwenda,*
*Tuipende nchi yetu tudumishe uzalendo.*

**Shairi B**

*Ukinitunza vizuri, na mimi nitakutunza,*
*Hewa nitakupatia, kivuli na dawa pia,*
*Mimi wa muhimu sana, katu usiniangamize,*
*Usinichome kwa yako tamaa, utakosa vitu vingi,*
*Mifugo yako punguza, ufuge kwa utaratibu,*
*Nisije kukasirika, yakakukuta majanga.*

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 64 05/09/2021 15:41

## Maswali

1. Kuna tofauti gani ya kimuundo kati ya shairi **A** na shairi **B**?
2. Ni ujumbe gani unaoupata katika shairi **A** na shairi **B**?
3. Mtunzi ana maana gani anaposema, "*Mali zetu wakifyonza, nchi haiwezi kwenda"* katika ubeti wa pili wa shairi **A**?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zingatia**

Shairi hubeba mpangilio maalumu wa maneno wenye ruwaza mahususi ya silabi, lugha ya mkato na lugha ya kitamathali. Baadhi ya mashairi yana urari wa vina na mizani na mengine hayana. Shairi hutumia tamathali mbalimbali za semi na misemo kadha wa kadha.

### Kazi ya 3.8

1. Tunga shairi lenye beti tatu (3) kuhusu jambo lolote unalolipenda.
2. Eleza ujumbe uliomo katika shairi hilo.

### Kazi ya 3.9

*Chunguza utunzi ufuatao wa Mbaraka Mwinshehe, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Hakuna kitu kibaya sana humu duniani kama shida,
Haichagui mtu, siku wala mwaka,
Haina katu taarifa shida huingia shida bila hodi,
Si mtoto wala mkubwa wote shida,
Kila siku shida shida haiishi mpaka siku ya mwisho.

Shida kamwe haikosekani hata kama siku ya harusi,
Na uwe na mapesa mengi ipo shida,
Haina ngoja wala aibu popote shida hutokeza,
Kwa maskini matajiri wote shida,
Kila siku shida shida haiishi mpaka siku ya mwisho.

FOR ONLINE USE ONLY

## Maswali

1. Eleza ujumbe unaopatikana katika utunzi huo.
2. Kutokana na utunzi huo tunapata dhamira gani?
3. Unafikiri ni kwa nini mtunzi anasema "shida haina mtu, siku wala mwaka, maskini wala tajiri?"



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 65 05/09/2021 15:41

4. Je, utunzi huo ni kipera gani cha ushairi?
5. Eleza tofauti ya kimuundo kati ya nyimbo na mashairi.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zingatia**

Nyimbo zinaweza kuimbwa zikiambatana na mapigo ya ala; ingawa si lazima. Nyimbo zinaweza kuimbwa na mtu mmoja au kikundi cha watu. Mara nyingi nyimbo huimbwa katika bendi, kwaya, taarabu na vikundi vya ngoma za jadi. Nyimbo hutumia lugha ya mkato, matumizi ya picha na mapigo ya kisilabi. Jambo la msingi katika nyimbo ni kuwapo kwa sauti. Kuna aina kadhaa za nyimbo na huwa na kazi nyingi katika jamii. Kuna nyimbo zinazohamasisha kazi mbalimbali, nyimbo za sherehe kama vile, harusi na nyinginezo. Aidha, kuna nyimbo za maombolezo, siasa, dansi, na za taarabu. Pia, nyimbo hutumika katika kuhimiza kampeni mbalimbali.

## Kazi ya 3.10

*Soma hadithi ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Hapo zamani za kale palikuwa na kijiji kimoja kilichoitwa Tulieni. Wakazi wa kijiji hicho walikuwa ni wakulima. Mwaka fulani baa la ukame lilikikumba Kijiji cha Tulieni na maeneo jirani. Baa la ukame liliharibu mazao yote yaliyokuwa shambani na kuwaacha wanakijiji wakihaha kwa njaa. Kutokana na baa hilo la ukame, maisha ya wanakijiji wa Tulieni yalibadilika yakawa duni sana. Wanakijiji hawakujua wafanye nini. Hawakuwa na mahali pa kupata chakula kwani hata vijiji vya jirani hakukuwa na chakula.

Siku moja, vijana wa Kijiji cha Tulieni waliitisha mkutano wa vijana wote. Mkutano huo ulilenga kutafuta mbinu ya kutatua tatizo la ukame ili waweze kujikwamua kutokana na hali duni inayowakabili. Walikuwa na mengi ya kujadili. Wanakijiji wa Tulieni hawakuwahi kushuhudia kijiji chao kikikumbwa na ukame kwa miaka mingi. Siku zote walikuwa wakifurahia maisha kwa wingi wa chakula na biashara ya mazao. Walijiuliza, ni kwa nini mwaka ule walikumbwa na ukame? Baada ya kujiuliza kwa muda mrefu, waligundua kwamba ukataji miti ovyo ndicho chanzo kikubwa kilichosababisha tatizo la ukame katika kijiji chao.

Kijiji cha Tulieni kilikuwa na kiongozi aliyeitwa Ngarisa. Kiongozi huyo alikuwa mtoto wa kwanza wa mzee Isaya. Alikuwa mwerevu na mwenye hekima na busara. Ngarisa alipendwa na watu wa rika zote katika Kijiji cha Tulieni. Kiongozi huyo alisimamia kampeni ya kuzuia ukataji miti ovyo. Siku moja aliamua kumwalika mtaalamu wa mazingira ili aje kijijini hapo kuzungumza na wanakijiji juu ya athari za ukataji miti ovyo.



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 66 05/09/2021 15:41

Siku ilipowadia, mtaalamu huyo aliwasili pale kijijini. Alizungumza na wanakijiji na kuwaasa kuacha kukata miti ovyo ili kuzuia athari za ukame. Wanakijiji waliifurahia elimu iliyotolewa na mtaalamu huyo. Wote walikubaliana kutokata miti ovyo. Pia, walikubaliana kuwa, yeyote atakayebainika anakata miti atachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwa ni pamoja na kufukuzwa katika kijiji chao.

Baada ya mkutano, wanakijiji walianza kutekeleza sheria walizokubaliana chini ya uongozi wa Ngarisa. Mtu yeyote aliyekwenda kinyume na makubaliano waliyojiwekea alichukuliwa hatua za kisheria; na ilipobidi alifukuzwa kijijini hapo. Baada ya miaka kadhaa kupita, kijiji kikawa na miti ya kutosha. Mvua zilianza kunyesha, ardhi ikawa na rutuba ya kutosha na tatizo la ukame likatoweka kabisa. Wanakijiji walianza kupata mazao ya kutosha. Hali duni ya maisha waliyokuwa nayo ikatoweka na kurejea kwenye maisha yao ya awali.

Wanakijiji walimshukuru sana Ngarisa kwa kuwaletea mtaalamu wa mazingira ambaye aliwapatia elimu iliyowasaidia kuondokana na tatizo la ukame. Kwa sasa wanakijiji wa Kijiji cha Tulieni wanaishi kwa raha mustarehe kama ilivyokuwa hapo awali.

FOR ONLINE USE ONLY

### Zoezi la 3.1

1. Fafanua mambo matatu (3) muhimu ya kuzingatia wakati wa masimulizi.
2. Eleza muundo wa hadithi hii uliyosoma.
3. Eleza mambo matano (5) yaliyoibuliwa kwenye hadithi uliyosoma.
4. Chambua sifa za wahusika na kazi zao katika hadithi uliyosoma.
5. Chambua lugha iliyotumiwa na mtunzi wa hadithi uliyosoma.

### Kazi ya 3.11

Wamiliki wa vyombo vya usafiri hupenda kuandika misemo mbalimbali kwenye vyombo vyao vya usafiri. Orodhesha misemo kumi (10) ambayo umewahi kuisoma kwenye vyombo mbalimbali vya usafiri.

### Zoezi la 3.2

Tega na kutegua vitendawili vitano (5), kisha eleza wahusika waliomo katika vitendawili hivyo.



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 67 05/09/2021 15:41

**Zingatia**

Uhakiki ni kitendo cha kusoma au kupitia kazi ya fasihi na kuichambua kwa lengo la kupima ubora wake. Kazi za fasihi simulizi zinaweza kupimwa na kuonekana zinafaa au hazifai. Kazi hizi hupimwa kwa kuzingatia uhusiano wake na hali halisi ya jamii. Hivyo, uhakiki wa kazi za fasihi simulizi ni uchambuzi wa kina wa vipengele vya fani na maudhui vya kazi inayohusika na kubaini kama ina ubora unaostahili pamoja na kuainisha udhaifu wake. Umuhimu wa uhakiki wa kazi ya fasihi simulizi ni pamoja na kubaini ubora wa kazi inayohusika, kubaini vipengele mbalimbali vya fani na maudhui, kupima namna kazi inavyoambatana na mazingira inamotokea, kupima kufaa na kutokufaa kwa fasihi simulizi, kubaini ukweli wa mambo yanayoelezwa, kuangalia uhalisi wa watu na mazingira katika jamii na kubaini umuhimu wa kazi ya fasihi katika jamii inayohusika.

Uhakiki wa kazi ya fasihi huzingatia vigezo viwili ambavyo ni fani na maudhui, kama vilivyochambuliwa kwenye masimulizi. Mhakiki hujiuliza maswali juu ya ujumbe unaotolewa kama ni wa kweli na unafaa au la; kama maadili yanayotolewa yanalingana na wakati tulionao au la; nahau misemo, methali na tamathali zilizotumika zinalingana na jambo linalosemwa au la; mtiririko wa matukio unamsaidia msikilizaji kuelewa kisa au unamchanganya? Maswali ya namna hiyo humsaidia mpimaji, ambaye ni mhakiki, kuelewa ubora wa kazi ya fasihi simulizi. Pia, yanaweza kutumiwa na mtunzi wa kazi ya fasihi simulizi hiyo kurekebisha kazi yake na kuifanya iwe bora zaidi. Hivyo, ni lazima kuzingatia hayo yote katika kuhakiki hadithi.

Uhakiki wa semi katika fasihi umejikita katika kuangalia usahihi wa matumizi ya vipengele mbalimbali vya lugha katika kazi ya fasihi inayohusika. Vipengele hivyo ni misemo, nahau na mafumbo. Vilevile, uhakiki wa semi umejikita katika kuchunguza namna lugha ilivyofuzu kigezo cha kwenda na wakati.

**Kazi ya 3.12**

*Soma hadithi ifuatayo, kisha hakiki kazi hiyo kwa kuzingatia vipengele vyote vya fani na maudhui.*

**Chura aliutaka uzuri**

Hapo kale, Chura na Jongoo walikuwa marafiki. Chura, kama kawaida, aliishi mtoni lakini njaa ilipokuwa ikimbana aliruka majanini kutafuta wadudu. Basi, siku moja Chura alihangaika vichakani lakini hakupata mdudu wa kumla.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE
FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 68 05/09/2021 15:41

Jioni alipokuwa anarudi mtoni alikutana na sahibu wake Jongoo. Wakaanza mazungumzo.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE




**Chura**: Lo! Rafiki yangu Jongoo habari za siku tele? Umepotelea wapi?

**Jongoo**: Aah! Sijambo mwanamaji. Wewe ndiye uliyezamia mtoni usionekane.

**Chura**: Aah! Wapi bwana! Mto hauna kitu! Hapa nilipo nina njaa isiyomithilika.

**Jongoo**: Pole sana. Tena kuna jambo moja nilitaka tuzungumze nikawa ninasahau kila mara. Unajua wadudu wanatukwepa kwa kuwa sura zetu ni mbaya. Mdudu akikuona tu anapata hofu na kurukia mbali sana.

**Chura**: Tena kweli bwana! Mara nyingine mdudu sijamsogelea, tayari pyuu! Sasa tufanyeje rafiki yangu?

FOR ONLINE USE ONLY

**Jongoo**: Mimi nimewaza na kuwazua nikagundua kuwa kaka Sungura anayo dawa ya uzuri; atatusaidia.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Chura**: Basi! Ndiyo maana ninakupenda. Una mawazo mazuri kama wahenga. Tumfuate mara moja. *(Hapo Jongoo na Chura wakaongozana harakaharaka mpaka kwa Sungura. Walipofika kwa Sungura, wakakaribishwa vizuri halafu wakamwelezea Sungura shida yao. Mazungumzo yao yakaendelea hivi:)*

**Sungura**: Ndiyo, kweli dawa ya uzuri ninayo. Huu ukurutu wako Chura utaondoka, na haya makwaruzo yako Jongoo yatatoweka.

**Chura**: Loo! Kaka Sungura fanya haraka tuondolee balaa hili. Sura hizi zinatunyima chakula.

**Sungura**: Sawasawa. Kwanza kila mmoja wenu akifika nyumbani kwake achemshe maji kwenye chungu, yachemke sana.

**Chura:** Ehee yachemke sana ...

**Sungura:** Yakishachemka utie dawa hii, halafu ...

**Chura**: Halafu tujitumbukize ... Sungura umeniponya, sitakusahau.

**Jongoo**: Mbona unakwenda mbio sana? Huna subira!

**Chura**: Bwana mimi ninawahi niandae dawa yangu niondokane na njaa hii. *(Basi hapo Chura akaondoka kwa miruko yake ya hatua ndefu. Alipofika nyumbani kwake akachemsha maji. Maji yalipochemka akanyunyiza ile dawa ndani ya maji na kurukia ndani ya maji yaliyokuwa yakichemka. Loo! Chura aliungua vibaya sana. Haraka akatoka majini akihema na kutweta. Alikuwa amechubuka sana. Chura aliugua kwa muda mrefu: Wakati alipokuwa akiugua, Jongoo alikuwa akimtembelea kumtaka hali. Siku moja wakawa na mazungumzo haya:)*

**Chura**: Loo! Niliungua sana rafiki yangu. Hivi wewe ulipotumia dawa ya Sungura hukuungua? Ninaona mwili wako ni mwororo sana.

FOR ONLINE USE ONLY

**Jongoo**: Laa! Mimi nilimsikiliza Sungura hadi mwisho. Wewe ulifanya pupa na haraka; lakini pole sana rafiki yangu. Kuanguka mtini ndio kushuka.

**Chura**: Loo! Basi pupa zangu zimeniponza. Sasa mwili wangu umejaa makovu na mabaka. *(Hatimaye Chura alipona, lakini alibaki na mabaka yake na miguu iliyopinda.)*

**Chanzo**: *Taasisi ya Elimu Tanzania (1996:2-4)*

## Kazi ya 3.13

*Soma sehemu ya utenzi ufuatao, kisha hakiki kwa kujibu maswali yanayofuata:*

Usawa wa kijinsia,
Ni haki zingatia,
Japo wagugumia,
Haki sawa zakwama.

Ukatili kijinsia,
Upigwe vita sikia,
Haki kwa wote tolea,
Usawa kuzingatia.

Kazi zote wanaweza,
Hata pia kuongoza,
Sipende hata kubeza,
Wote wako na usawa.

Majukumu yatolewe,
Kwa nini wabaguliwe,
Wote wasibaguliwe,
Haki na fursa kwa wote.

Shuleni nako nyumbani,
Ofisini na shambani,
Kadhalika viwandani,
Usawa uzingatiwe.

FOR ONLINE USE ONLY

## Maswali

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

1. Mtunzi wa utenzi huu ana dhamira gani?
2. Utenzi huu una jumla ya beti ngapi?
3. Je, unafikiri mtunzi amezingatia urari wa mizani katika utunzi huu? Toa sababu.
4. Mtunzi amekemea mambo gani katika utenzi huu?
5. Linganisha maudhui ya utenzi huu na uhalisia wa jamii unamoishi.

### Kazi ya 3.14

*Soma hadithi ifuatayo, kisha hakiki kwa kujibu maswali yanayofuata:*

**Chautundu akiona cha mtemakuni**

Hapo zamani za kale palikuwa na bibi mmoja aliyeitwa Nyasalige. Bibi huyu aliishi katika kijiji cha Mwipori. Aliishi huko na wajukuu wake wanne: Mkaya, Nyantongwa, Mati, na Mabuta. Wajukuu hawa walikuwa watoto wa binti yake Nyanfilo na kijana wake Mulilo. Bibi huyu alipenda sana kuwasimulia hadithi wajukuu wake. Mara nyingi alianza hadithi zake kwa "paukwa … pakawa."

Kwa kuwa bibi huyu alikuwa mzee sana, kazi nyingi zilifanywa na wajukuu wake. Watoto hawa walifanya kazi kwa ushirikiano mkubwa. Mkaya ambaye ndiye alikuwa mkubwa alikuwa akiwaelekeza wenzake namna ya kufanya kazi mbalimbali. Mati na Nyantongwa walikuwa watiifu wakifuata maelekezo waliyokuwa wakipewa na bibi yao pamoja na yale ya Mkaya. Mabuta alikuwa mkaidi na hakutaka kufuata maelekezo, hasa yaliyotolewa na Mkaya. Mara nyingi hakutaka kufuatana na ndugu zake. Alikuwa na marafiki zake ambao alipenda kwenda kucheza nao. Kutokana na ukaidi wake, walimbatiza jina la Chautundu. Baadhi ya marafiki zake walikuwa na tabia mbaya ikiwemo tabia ya udokozi na kutokuheshimu watu wakubwa.

FOR ONLINE USE ONLY

Baada ya bibi yake Mabuta kugundua tabia hiyo alimkanya na kumshauri asiendelee na tabia hiyo. Alimsihi asifuatane tena na hao marafiki zake kwa kuwa alihofia kuwa ataiga tabia zao mbaya. "Mjukuu wangu! Wahenga walisema ukitembea na mwizi nawe utakuwa mwizi. Nimesikia siku hizi umejiunga na marafiki zako wengine na hutaki kushirikiana na ndugu zako. Ninakuonya usirudie kushirikiana na makundi ya vijana hao wasiopenda kufanya kazi." Hayo yalikuwa ni maneno ya bibi kwa mjukuu wake Mabuta.



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 72 05/09/2021 15:41

Hata hivyo, mwonja asali haonji mara moja. Mabuta alikuwa amekwishajifunza tabia ya udokozi; hivyo, ilikuwa vigumu kuacha. Aliendelea na tabia ile bila kujali ushauri aliopewa na bibi yake. Mkaya naye alimwonya sana Mabuta huku akitumia methali inayosema, "Asiyesikia la mkuu, huvunjika guu."

Siku moja, Mati aliamua kukaa na ndugu yake, Mabuta, na kuongea naye kwa muda mrefu. Alimwambia, "Mabuta kaka yangu! Kwa nini hutaki kusikia ushauri unaopewa? Mimi mwenzio sipendi kuzurura ovyo. Wewe pia ulitakiwa ukae nami muda mwingi ili tucheze pamoja; lakini hunijali. Wahenga walisema asiyefunzwa na mamaye, hufunzwa na ulimwengu." Alimaliza na kumtaka Mabuta abadilike na kuwa mtoto mwema. Mabuta alikaa kimya muda wote na mwisho akasema, "Wewe ni mdogo sana kwangu. Isitoshe, hutakiwi kufuatilia maisha yangu."

Siku za mwizi ni arobaini. Hazikupita siku nyingi Mabuta akakamatwa akiwa ameiba karanga za watu. Alipigwa huku akiwa amefungwa kamba mpaka akashindwa kutembea. Wasamaria waliomkuta akiwa ametupwa huko njiani ndio waliompeleka nyumbani. Alikuwa ameumizwa vibaya. Bibi yake alipomwona vile, alimgombeza kwa maneno makali. "Mtoto hutulii nyumbani! Umekuwa kama fisi kutangatanga kutafuta chakula au umekuwa paka asiye na makazi. Sasa hivi nitakuwa mkali kama simba mpaka utakaponyooka." Alisema Bibi Nyasalige.

Usiku ule bibi yao aliwakusanya pamoja na kuanza kuongea nao. Mabuta, ambaye, hapo awali hakutaka kumsikiliza bibi, alikaa kimya na kumsikiliza bibi yake. Mwishoni, aliomba msamaha na kuahidi kutorudia.






KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 73 05/09/2021 15:41

"Nimepigwa vibaya sana. Walitaka kunichoma moto. Sitarudia tena kuiba na kuanzia sasa nitashirikiana na wenzangu kufanya kazi zote za hapa nyumbani."

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Bibi aliendelea kuwasimulia hadithi mbalimbali. Aliwaambia watoto wema huwa watu wema hata wawapo wakubwa. Alisema baadhi ya viongozi wamekosa maadili kutokana na kutokulelewa vema. Wamejikuta wakiwa kama nyangumi kutaka kuwanyayasa wenzao bila kujali utu wao. Aliwasihi wapendane wasije kuwa kama samaki wakubwa wanavyowameza samaki wadogo huko baharini bila kujali kuwa wote ni samaki.



"Mkijifunza kupendana na kuwapenda wengine mkiwa bado wadogo mtakuwa raia wema wenye kupendana, kuwapenda wengine na kuipenda nchi yenu hapo baadaye." Alimaliza na kuwaaga wajukuu wake, kisha akaenda kulala.

## Maswali

1. Hakiki matumizi ya semi katika hadithi uliyosoma.
2. Chambua wahusika katika hadithi uliyosoma.
3. Umejifunza nini katika hadithi uliyosoma?
4. Ujumbe unaotolewa katika kisa hicho una uhalisia gani katika jamii yako?
5. Eleza kwa ufupi ujumbe uliomo katika picha zilizotumika katika hadithi uliyosoma.

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la marudio la 3

1. Chagua jibu sahihi katika maswali yafuatayo:

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

   (i) "Mtangazaji wa televisheni huhakikisha watazamaji wanapata habari sahihi kwa wakati." Katika fasihi, kazi hiyo hufanywa na nani kati ya hawa wafuatao?
   (a) Wasilikizaji
   (b) Hadhira
   (c) Fanani
   (d) Wasomaji
   (e) Wazungumzaji

   (ii) Mawazo makuu ya mtunzi wa kazi ya fasihi humfikia mlengwa kwa njia ipi kati ya hizi zifuatazo?
   (a) Fani
   (b) Maudhui
   (c) Dhamira
   (d) Falsafa
   (e) Migogoro

   (iii) Uwasilishaji wa kazi za fasihi unaotofautiana kati ya mtunzi mmoja na mwingine huitwaje?
   (a) Muundo
   (b) Mtindo
   (c) Maudhui
   (d) Falsafa
   (e) Fani

   (iv) Ipi ni tofauti ya msingi kati ya mashairi na ngonjera?
   (a) Mpangilio wa vina na mizani
   (b) Idadi ya mizani na mishororo
   (c) Majibizano baina ya watu wawili au zaidi
   (d) Mpangilio maalumu wa silabi na lugha ya mkato
   (e) Mapigo ya kimuziki na ridhimu

FOR ONLINE USE ONLY

(v) Katika tungo zifuatazo, ni kauli ipi ina dhima tofauti na nyingine?
  (a) Akili ni nywele kila mtu ana zake.
  (b) Siku za mwizi ni arobaini.
  (c) Adui mpende.
  (d) Aisifuye mvua imemnyea.
  (e) Amevaa miwani.

2. Oanisha maana za vipera vya hadithi katika orodha **A** na vipera vinavyohusika katika orodha **B** kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi.

| **Orodha A** | **Orodha B** |
|---|---|
| (i) Husimuliwa kama mifano ya kuadilisha watu. | A. Soga |
| (ii) Husimulia chimbuko la asili na ukweli wa mambo. | B. Tarihi |
| (iii) Husimuliwa kwa nia ya kuchekesha na kukejeli. | C. Vigano |
| (iv) Husimuliwa kwa lengo la kuwaasa watoto. | D. Visasili |
| (v) Husimulia matukio ya kihistoria. | E. Ngano |
| | F. Mizungu |
| | G. Hadithi |

3. Eleza tofauti ya msingi ya uwasilishaji wa fasihi simulizi na fasihi andishi.
4. Fafanua kazi tatu za fasihi simulizi katika jamii.
5. Linganua mafumbo na vitendawili kama kauli zinazomfikirisha msikilizaji.

FOR ONLINE USE ONLY
FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 76 05/09/2021 15:41

# Sura ya Nne

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Uandishi wa insha na barua

### Utangulizi

*Kuna uandishi wa aina mbalimbali kama vile insha, barua, na kadi za mialiko. Uandishi wa insha na barua ni njia muhimu katika kufikisha habari kwa watu. Katika sura hii utajifunza uandishi wa insha na barua za kirafiki. Katika insha utajifunza kuandika insha za wasifu za kisanaa na zisizo za kisanaa. Pia, utajifunza kuandika barua za kirafiki na njia mbalimbali za kutuma barua. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kuandika insha za wasifu za kisanaa na zisizo za kisanaa kwa kuzingatia muundo wa insha. Pia, utaweza kuandika barua za kirafiki kwa kuzingatia muundo sahihi.*

### Kuandika insha za wasifu za kisanaa na zisizo za kisanaa

**Kazi ya 4.1**

*Soma insha ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**MLIMA KILIMANJARO**

Mlima ni sehemu ya ardhi iliyoinuka. Mwinuko wa mlima mmoja hutofautiana na miinuko ya milima mingine. Baadhi ya milima huwa mirefu na mingine huwa mifupi. Mlima unaweza kuwa na mawe, misitu, miti, au theluji. Hali ya hewa inayopatikana sehemu za milimani huwa ya baridi zaidi kadiri mtu anavyopanda kuelekea juu.

Mlima Kilimanjaro ni moja ya milima maarufu sana duniani. Mlima huu unapatikana nchini Tanzania katika Mkoa wa Kilimanjaro. Ni mlima mrefu kuliko milima yote barani Afrika.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 77 05/09/2021 15:41




Uzuri wake huwavutia watalii kutoka mataifa mbalimbali. Mlima huu umezungukwa na misitu na mito. Misitu hiyo huhifadhi wanyama kama vile tembo, mbega, nyani, swala, na ndege mbalimbali ambao huwavutia sana watalii. Hivyo, eneo la Mlima Kilimanajaro ni mojawapo ya hifadhi za taifa.

Mlima Kilimanjaro huingiza mapato katika nchi yetu kwani watalii wengi huja nchini Tanzania kwa lengo la kuupanda. Pia, huwapatia ajira Watanzania wengi wanaowaongoza watalii kupanda mlima huo.

Misitu inayozunguka Mlima Kilimanjaro imechangia sana kuwapo kwa hali ya hewa nzuri katika mkoa huo. Pia, imekuwa chanzo cha kuleta mvua mkoani humo. Hivyo, mlima na mazingira yake huwavutia sana watalii kutoka nchi mbalimbali duniani.

Pamoja na faida hizo, mlima huu pia una changamoto chache ambazo huwa zinachukuliwa hatua pindi zinapotokea. Miongoni mwa changamoto hizo ni athari ziletwazo na wanyama waliomo katika hifadhi hiyo. Wakati mwingine wanyama hutoka katika hifadhi hiyo na kuwafanya wananchi wanaoishi jirani na mlima kuhofia usalama wao. Pia, baadhi ya watu huwawinda wanyama hao kwa ajili ya kitoweo bila idhini ya serikali. Hivyo, hujikuta wakifanya uwindaji haramu na kuanza kushughulikiwa na serikali.

Kwa ujumla, mlima huu una faida nyingi kwa nchi yetu ya Tanzania. Kwa hiyo, tuupende, tuulinde na tuyatunze mazingira yake. Huu ni miongoni mwa milima inayovutia barani Afrika na dunia nzima.

FOR ONLINE USE ONLY

## Maswali

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

1. Unafikiri mwandishi wa insha hii amemwandikia nani?
2. Lengo la mwandishi wa insha hii ni lipi?
3. Insha hii ina umuhimu gani katika jamii yetu?
4. Lugha iliyotumika katika insha hii ina sifa zipi?
5. Taja mambo ya msingi yaliyozingatiwa katika uandishi wa insha hii.
6. Insha hiyo imeundwa na sehemu zipi?
7. Eleza kwa ufupi (aya mbili) kuhusu Mlima Kilimanjaro kutokana na insha hii.
8. Uandishi wa insha una umuhimu wowote? Kwa nini?

### Kazi ya 4.2

*Soma insha ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**MVUA KUBWA**

Siku moja alfajiri Ngonja alisikika akimgongea mlango Nyamuzi huku akimwambia, "Wewe! Mgaagaa na upwa hali wali mkavu." Nyamuzi alishituka mithili ya mbwa aliyekuwa anakimbilia mnofu. Akafungua mlango kumkaribisha Ngonja huku akimwambia, "Karibu! Karibu! Karibu sana ndani." Ngonja akamwambia, "Muda wa kwenda shambani umewadia, tujiandae haraka kabla jua halijachomoza." Wakaanza kujiandaa. Nyamuzi akaelekea ndani kuchukua majembe. Alipofika aliyakuta majembe yakiwa yametulia kama maji mtungini. Ngonja alipoona Nyamuzi amechelewa, akamfuata. Akamkuta amesimama akiangalia yale majembe. Kwa nguvu akasema, "We! We! Mchagua jembe si mkulima bwana: Chukua majembe mawili hapo." Wakacheka kwa pamoja; Ha! Ha! Ha! Wakaanza safari ya kuelekea shambani. Walibeba mbegu za mahindi na majembe yao. Walipofika shambani walipanda mahindi kwa bidii huku wakiamini kuwa jembe halimtupi mkulima. Ingawa ilikuwa asubuhi, walivuja jasho kama watu waliokuwa juani.

FOR ONLINE USE ONLY

Ilipofika alasiri, ghafla walisikia ngurumo ya kutisha ikiambatana na radi kubwa iliyotikisa anga la eneo lile. Waliendelea tu kupiga jembe kwa nguvu zao zote huku wakipiga moyo konde. Ama kweli jambo usilolijua ni kama usiku wa giza. Mara waliona mvua imeanza kutema cheche mithili ya moto uliokolezwa. Punde si punde, walitupa majembe na kuanza kutafuta pa kujihifadhi. Walisimama chini ya mti. Mara, nyuma yao wakasikia puu! Kugeuka nyuma, kumbe mti uliokuwa karibu yao ulikuwa umeanguka. Walipokuwa wakitahamaki kwa tukio



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 79 05/09/2021 15:41

hilo, ghafla walishituka kuona miti mirefu iliyokuwa karibu na shamba la jirani ikianguka mmoja baada ya mwingine. Majabali makubwa yaliviringishwa na maji na kutupiliwa mbali kama jiwe lililorushwa na manati ya kuwindia ndege.

FOR ONLINE USE ONLY

Walipigwa na bumbuwazi huku wakilegea mioyo yao na kuanza kukimbia kurudi nyumbani. Mvua kubwa iliendelea kunyesha ikiambatana na mawe meupe madogomadogo mithili ya changarawe. Nguo walizokuwa wamevaa zilikuwa tayari zimetota maji yaliyokuwa yanawachuruzika kama maji katika koki ya bomba iliyokuwa imefunguliwa. Waliendelea kuchanja mbuga kuelekea nyumbani. Ngonja alisikika akimwambia Nyamuzi, "Simama wima rafiki yangu kila mwomba Mungu hakosi fungu lake." Hata hivyo, hawakukumbuka kama majembe yao waliyapa kisogo palepale walipokuwa wanalima.



Katika patashika hiyo, walijikuta wamefika kijiji cha jirani. Loo! Mto uligeuka jito; maji yalijaa na kuacha njia na kuingia kwenye nyumba za watu. Migomba iliyokuwa pembeni mwa nyumba hizo na majani ya miti vilionekana vikielea juu ya maji yasiyokuwa na huruma. Nyamuzi alionekana amekata tamaa na kutweta. Ngonja akamwambia, "Tulia, kila ngoma ina mchezo wake." Watu wengi walishaondoka kijijini hapo kukimbia dhoruba hiyo. Hivyo, walihangaika sana kupata msaada. Baadaye wakafanikiwa kuona nyumba iliyopo karibu na mlima;



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 80 05/09/2021 15:41

na mtu mmoja akiwapungia mkono kama ishara ya kuwaita. Nyuso zao zilijaa tabasamu pana huku zikiwa na matumaini mapya. Wote wawili walielekea katika nyumba ile. Wakati huo mvua ilikuwa imeanza kupungua. Wakakaribishwa ndani. Giza lilipoanza kuingia, hali ilikuwa imeanza kutengemaa. Walimshukuru mwenye nyumba na kuanza safari ya kurejea nyumbani kwao.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maswali

1. Orodhesha vipengele vya matumizi ya lugha katika insha uliyosoma, kisha eleza dhima ya kila kipengele.
2. Vipengele hivyo vinadokeza aina gani ya insha? Toa sababu ya jibu lako.
3. Unafikiri kwa nini mwandishi ametumia lugha ya aina hiyo?
4. Tofautisha vipengele vya lugha iliyotumika katika insha ya Mlima Kilimanjaro na insha ya Mvua Kubwa.
5. Umejifunza nini kutokana na insha uliyosoma?
6. Kichwa gani cha insha kingine kingefaa kutumika badala ya "Mvua Kubwa?"
7. Unafikiri insha ina mchango gani katika lugha?
8. Lugha ina mchango gani katika uandishi wa insha?
9. Eleza namna lugha inavyoweza kuathiri uandishi wa insha.

**Zingatia**

Kuna aina mbalimbali za insha. Katika sura hii zimejadiliwa insha za wasifu za kisanaa na zisizo za kisanaa. Insha za wasifu huelezea sifa binafsi. Sifa hizo huweza kueleza uzuri au ubora wa kitu au mtu pamoja na udhaifu au ubaya wa mtu au kitu kinachoelezewa. Kuna insha za kisanaa na zisizo za kisanaa. Insha za kisanaa hutumia lugha ya kisanaa kama vile lugha ya picha na wahusika wa kubuni. Pia, hutumia lugha yenye mvuto, nahau, misemo, methali, tamathali za semi, na ishara. Insha zisizo za kisanaa hutumia lugha ya kawaida katika kuelezea sifa za kitu, mtu, au mahali. Insha za namna hii huweka vitu bayana tofauti na insha za kisanaa ambazo ujumbe wake huweza kufichwa kutokana na lugha ya kisanaa iliyotumika.

FOR ONLINE USE ONLY

**Kazi ya 4.3**

Tafuta vitabu vyenye insha mbalimbali, kisha soma insha zisizo za kisanaa. Chunguza miundo yake na uandike insha isiyo ya kisanaa yenye maneno yasiyopungua mia mbili (200) na yasiyozidi mia mbili na hamsini (250) kuhusu kivutio kingine chochote kilichoko Tanzania.



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 81 05/09/2021 15:41

### Kazi ya 4.4

Andika insha ya kisanaa isiyozidi maneno mia mbili na hamsini (250) kuhusu umuhimu wa kilimo.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Kazi ya 4.5

*Soma kifungu cha habari kifuatacho, kisha kiandike kwa kufuata taratibu za uandishi. Andika kichwa cha habari, tenga aya, na utumie alama za uandishi na herufi kubwa kwa usahihi.*

kubo ni mwanafunzi wa kidato cha kwanza anayependa sana kujisomea hujisomea masomo yote ili aweze kupata maarifa ujuzi na umahiri wakati wa vipindi darasani hutulia kumsikiliza mwalimu mwalimu asipokuwepo hutumia muda huo kujisomea Siku moja wakati wa somo la Kiswahili alichaguliwa kusoma insha alisoma vizuri sana sisi sote pia tulisoma vizuri kwa sababu tunapenda kusoma pia mwalimu alituambia jipongezeni tukajipongeza kwa makofi paa paa paa. Ilipofika wakati wa somo la kiingereza kubo alijibu maswali mengi kuliko sisi mwalimu alimpongeza sana kubo alisema kuwa wote tuige mfano wa kubo kwa sababu ni muhimu kuelewa vizuri kila somo tangu siku hiyo wanafunzi wote tulianza kujisomea darasani kama kubo ili tuweze kufanya vizuri katika masomo yote tuling'amua kwamba hii itatusaidia kupata elimu itakayotuwezesha kukabiliana na mazingira ya kila siku.

**Zingatia**

Kuna utaratibu maalumu ambao huzingatiwa ili kuandika insha bora. Kwanza, uelewe vyema jambo unaloliandikia kwa sababu itakusaidia kuandika mambo kwa upana wake ili kufikisha mafunzo stahiki kwa hadhira inayohusika. Aidha, kumbuka kufuata mtiririko mzuri wa mawazo ili kupangilia visa au maudhui kuanzia mwanzo. Muundo wa insha unazingatia vipengele vifuatavyo: Kichwa cha insha ambacho huandikwa kwa herufi kubwa, juu kabla ya mwanzo wa insha, sehemu ya katikati na kupigiwa mstari. Kichwa cha insha lazima kiakisi maudhui ya insha inayohusika. Mwanzo wa insha huwa na utangulizi ambao huandikwa katika aya moja inayoeleza lengo kuu la insha kwa muhtasari. Vilevile, insha huwa na kiini. Hii ni sehemu kuu inayobeba kazi nzima au mawazo ya mwandishi. Mawazo hayo huandikwa katika mtiririko wa aya kwa mtindo wa aya moja kuwa na wazo moja. Hatimaye, mwisho wa insha ambao unatoa hitimisho juu ya mawazo hayo. Haya yote yatakuwezesha kufikisha ulichokikusudia na utamwezesha msomaji kupata uelewa wa jambo ulililoliandika na kupata ujumbe

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 82 05/09/2021 15:41

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

uliokusudiwa. Pili, tumia lugha fasaha na sanifu katika uandishi. Kufanya hivyo kutamsaidia msomaji kuelewa na kukuza lugha inayohusika kwa ufasaha. Tatu, zingatia alama za uandishi. Alama hizo ni kama vile: alama ya kuuliza, nukta, mkato, funga na fungua semi, na matumizi ya herufi kubwa. Zifuatazo ni baadhi ya alama na matumizi yake: Kituo kikuu au nukta (**.**). Hii hutumika mwishoni mwa sentensi kuonesha pumziko refu, kufupisha maneno, kutenganisha tarehe, na kuonesha desimali. Nukta pacha (**:**) hutumika kuonesha uwiano, kabla ya orodha ya vitu, kumtenga mhusika na maelezo yake katika ngonjera, tamthiliya, au majibizano, na kutenganisha saa na dakika. Mkato au koma (**,**) hutumika kuonesha kituo kidogo au pumziko fupi ndani ya sentensi, kutenganisha vitu katika orodha na kutenga sentensi kabla ya alama za kufungua na kufunga usemi. Nukta mkato (**;**) hutumika kuonesha pumziko refu kidogo kabla ya kituo kikubwa na kutenga orodha ya vitu vilivyo katika mafungu. Kistari (-) mwishoni mwa pambizo hutumika kuashiria neno lililokatwa katika sentensi ambalo linaendelea katika mstari unaofuata. Kwa kawaida, neno lililokatwa lazima liishie na silabi. Pia, hutumika baada ya nukta pacha, kutenganisha tarehe na kuunganisha baadhi ya maneno yaliyoundwa kwa maneno mawili. Fungua na funga semi au alama za mitajo (**" "**) hutumika kufunga neno lililonukuliwa kama lilivyo. Mstari wa mshazari (/) hutumika kuonesha neno mbadala au visawe na kutenganisha tarehe. Mabano (**( )**) hutumika kuonesha msisitizo wa kilichosemwa, kufafanua au kuonesha maana ya ziada. Alama ya Mshangao (**!**) hutumika baada ya neno la mshangao au kushituka, uchungu au huzuni. Alama ya kuuliza (**?**) hutumika katika kuuliza maswali. Baada ya alama hii sentensi inayofuata huanza na herufi kubwa. Nukta katishi (**...**) hutumika kukatisha jambo au maoni. Ritifaa (**'**) hutumika kutofautisha sauti *ng* na *ng'* kama katika *ngoma* na *ng'ombe*, au *ngumi* na *ng'onda*. Aidha, herufi kubwa ni miongoni mwa alama za uakifishaji zinazotumika katika uandishi. Hutumika mwanzoni mwa sentensi, katika majina ya pekee na katika vifupisho vya maneno. Pia, neno linalofuata baada ya nukta, alama ya mshangao na alama ya kuuliza huanza kwa herufi kubwa.

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la 4.1

1. Unafikiri insha ina mchango gani katika lugha?
2. Kwa nini unapoandika insha ni muhimu kuzingatia alama za uandishi?
3. Ni mambo gani unapaswa kuyazingatia katika uandishi wa insha ili isiwe na makosa ya kisarufi na kimantiki?
4. Utazingatia sifa zipi unapoandika insha ya wasifu?
5. Ni mambo gani yanaweza kuifanya insha isiwe bora?



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 83 05/09/2021 15:41

**Kazi ya 4.6**

Andika insha yenye maneno yasiyopungua mia mbili (200) na yasiyozidi mia mbili na hamsini (250) kuhusu utunzaji wa mazingira huku ukizingatia matumizi ya alama za uandishi katika kazi yako.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kuandika barua ya kirafiki

**Kazi ya 4.7**

*Soma barua ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Shule ya Sekondari Lungo,
S.L.P. 83,
Ngara.
20-03-2020.

Mama mpendwa,

Shikamoo! Habari za hapo nyumbani? Je, baba alifika salama alipotoka huku? Kusudi la barua hii ni kutaka kukujulisha kuwa nimekwishaanza kuzoea maisha ya hapa shuleni. Tayari tumeanza masomo; kwa hiyo, ninakazana kujifunza na kusoma kwa bidii ili niweze kupata elimu itakayonisaidia kukabiliana na maisha ya kila siku.

Pia, ratiba yetu ya shule huwa inaanza mapema sana. Tunaamka alfajiri na kuchelewa kulala kwa ajili ya kujisomea. Kwa kawaida, tunalala saa nne usiku na kuamka saa kumi na moja alfajiri. Vilevile, mchana tunakuwa na kazi za nje. Kazi hizo ni kuchota maji ya kupikia na kuoga. Halikadhalika, tuna muda kwa ajili ya kufanya mazoezi ya viungo ili kuboresha afya zetu.

Mama, ninakuomba umkumbushe baba aninunulie vitabu vya Hisabati na Kiswahili. Ninaishia hapa kwa leo.

Mwanao mpendwa,

Mnyandagaro.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 84 05/09/2021 15:41

## Maswali

1. Barua hiyo imeandikwa na nani?
2. Aliyeandika barua hiyo anaishi wapi?
3. Mwandishi alimwandikia nani barua hiyo?
4. Lengo la barua hiyo lilikuwa lipi?
5. Sehemu ipi inaonesha mwisho wa barua?
6. Eleza sababu ya kuweka salamu na maagano katika barua ya kirafiki.
7. Kwa nini barua hii haina anwani ya mwandikiwa?
8. Eleza hatua utakazozitumia kuandika barua ya kirafiki?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Kazi ya 4.8

Jifanye wewe ni mama yake Mnyandagaro, kisha jibu barua hiyo uliyoandikiwa.

**Zingatia**

Barua za kirafiki huandikwa kwenda kwa ndugu, jamaa na marafiki kwa lengo la kusalimiana, kupashana habari, kuomba msaada, kushukuru au kupongeza. Kwa kawaida, barua za kirafiki humpa mwandishi uhuru wa kutumia lugha jinsi anavyopenda. Mara nyingi ni lugha isiyo rasmi bali hutegemeana na uhusiano uliopo kati ya mwandishi na mwandikiwa. Uhuru huu humruhusu mwandishi kuandika barua yenye urefu anaoutaka.

### Kazi ya 4.9

1. Kusanya barua za aina tofauti, zisome kwa umakini, kisha chunguza muundo wake, lugha iliyotumika na ueleze jinsi zinavyofanana na kutofautiana.
2. Chora kielelezo cha muundo wa barua ya kirafiki.

FOR ONLINE USE ONLY

**Zingatia**

Barua ya kirafiki huzingatia vipengele muhimu vifuatavyo: Kwanza, anwani ya mwandishi ambayo huandikwa juu upande wa kulia wa karatasi kwa kuzingatia vituo na taratibu za uandishi. Anwani huonesha maskani ya mwandishi kwa kuwa ndiyo hutumiwa na mwandikiwa pale anapotaka kujibu. Pili, tarehe ambayo huandikwa upande wa kulia wa karatasi chini ya anwani ya mwandishi. Hii humsaidia mwandikiwa kujua barua iliandikwa lini na kubaini kama imefika kwa wakati au imechelewa. Tarehe hiyo huweza kuandikwa kwa mitindo mbalimbali kama vile: 19.03.2020, 19/03/2019, 19-03-2020, 19 Machi 2020, au Machi 19,




KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 85 05/09/2021 15:41

2020. Tatu, mwanzo wa barua ambao huandikwa salamu za awali zinazozingatia uhusiano uliopo baina ya mwandishi na mwandikiwa. Kwa kawaida, huandikwa kwa kuruka mstari mmoja baada ya tarehe. Nne, kiini cha barua ambacho ni madhumuni ya barua. Sehemu hii inaweza kuwa na aya moja au zaidi ambazo sharti ziandikwe vizuri ili lengo la barua liwe bayana. Tano, mwisho wa barua ambao huwa na salamu za kuagana. Maneno yanayotumika katika salamu hizo hutegemea uhusiano wa mwandishi na mwandikiwa. Sita, jina la mwandishi ambalo huandikwa mwishoni mwa barua. Lengo ni kuonesha nani ameandika barua. Jina siyo sehemu ya anwani; hivyo, halipaswi kuandikwa kwenye anwani.

## Kazi ya 4.10

1. Mwandikie barua dada yako anayefanya kazi katika shirika la reli la Mkoa wa Kigoma lenye Sanduku la Posta 12021, ukimtaarifu aje kukupokea kwenye kituo cha treni utakapofunga shule.
2. Tazama bahasha zifuatazo, kisha jibu maswali katika zoezi linalofuata.




**Kielelezo namba 4.1:** *Anwani ya mwandikiwa mbele ya bahasha*

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE
FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 86 05/09/2021 15:41




**Kielelezo namba 4.2:** *Anwani ya mwandishi nyuma ya bahasha*

## Maswali

1. Unafikiri kwa nini anwani ya mwandikiwa inakaa mbele ya bahasha?
2. Eleza sababu za kuandika anwani ya mwandishi nyuma ya bahasha?
3. Fafanua umuhimu wa bahasha katika kutuma barua.
4. Nini kitatokea iwapo utaandika anwani juu ya bahasha bila kuandika sehemu ilikotoka?
5. Eleza mazingira ambamo unaweza kuandika barua na kumpa uliyemwandikia bila kuiweka katika bahasha?

### Zingatia

Baada ya kuandika barua, huna budi kutafuta bahasha na kuiandika anwani ya mtu unayemtumia barua mbele ya bahasha hiyo. Baada ya kuandika anwani, bahasha hubandikwa stempu inayolingana na gharama za kuisafirishia barua inayohusika. Hii inategemea uzito na umbali inaopelekwa. Ni vizuri kuandika anwani ya mwandishi nyuma ya bahasha kama inavyoonekana kwenye kielelezo namba 4.2. Uandishi wa anwani hiyo utamsaidia mtu anayeipokea kujua barua imetoka kwa nani hata kabla hajaifungua. Pia, husaidia kurudishwa kwa barua kwa mwandishi pale inaposhindwa kumfikia mwandikiwa. Utaratibu huu ni mzuri, hasa kwa barua zinazosafirishwa kwa njia ya posta japo siyo lazima.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 87 05/09/2021 15:41

### Kazi ya 4.11

Andaa karatasi, gundi na wembe au mkasi, kisha tengeneza bahasha. Andika anwani ya mwandikiwa mbele ya bahasha na anwani ya mwandishi nyuma ya bahasha hiyo. Anwani ya mwandishi iwe Shule ya Sekondari Maarifa, S.L.P. 260, Nansio. Anwani ya mwandikiwa iwe Shule ya Sekondari Magufuli yenye Sanduku la Posta 35013, Chato, Geita.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4.2

1. Unafikiri ni njia gani hutumika zaidi katika kutuma barua?
2. Unafikiri kwa nini baadhi ya njia za kutuma barua hazitumiki zaidi?
3. Eleza umuhimu wa kujua njia mbalimbali unazoweza kutumia kutuma barua.
4. Fafanua faida na hasara ya kutumia njia ya mkono kutuma barua.
5. Linganisha na linganua njia ya posta ya kawaida na njia ya Huduma ya Utumaji wa Haraka (EMS).

**Zingatia**

Barua ikishaandikwa huweza kutumwa kwa njia yoyote kati ya hizi zifuatazo:

**Posta**: Njia hii huwa na gharama za usafirishaji kutegemeana na uzito na uharaka wa barua inayohusika. Kuna barua zinazotumwa kwa njia ya kawaida, zenye kuwekwa stempu na zisizo na stempu. *Stempu* ni kipande kidogo cha karatasi cha posta chenye alama maalumu kinachonunuliwa na kubandikwa juu ya bahasha yenye barua ili kuthibitisha ulipwaji wa gharama ya kutuma barua inayohusika.

**Rejesta**: Ni bahasha maalumu inayotumiwa kupostia vitu vya thamani au barua muhimu inayopatikana posta. Barua inayotumwa kwa njia hii humlazimu mpokeaji kuthibitisha upokeaji wa rejesta inayohusika na kurudishwa kwa mtumaji.

**Huduma ya Utumaji wa Haraka (Express Mail Service - EMS)**: Husafirisha barua au kifurushi bila kuwekwa stempu. Bahasha inayotumika kwa usafirishaji wa haraka huwa na anwani mbili, yaani anwani ya mtumaji upande mmoja na ya mpokeaji upande wa pili. Anwani hizo mbili hujumuisha namba za simu kwa ajili ya kurahisisha mawasiliano ya kumfikishia mhusika barua au kifurushi.

**Njia ya mkono**: Hii siyo rasmi japo huweza kutumiwa pale inapoonekana kuwa na uhitaji huo ambapo barua humfikia mpokeaji bila kupitia posta. Mara nyingi hutumika kusafirisha barua kwenda kwa watu wa karibu. Barua huweza kuwekwa kwenye bahasha au isiwekwe kwenye bahasha kwa kuwa mhusika hukabidhiwa ana kwa ana na mwandishi au aliyeagizwa.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 88 05/09/2021 15:41

## Zoezi la marudio la 4

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

1. Kwa kuzingatia uandishi wa barua ya kirafiki, oanisha kauli katika orodha **A** kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi kutoka orodha **B**.

| Orodha A | Orodha B |
|---|---|
| (i) Mpendwa mama, shikamoo! Habari za nyumbani … | A. Anwani ya mwandishi |
| | B. Tarehe |
| (ii) Wako mwanao mpendwa Bahati. | C. Mwanzo wa barua |
| (iii) S. L. P. 1025, Manyara. | D. Anwani ya mwandikiwa |
| (iv) Naomba unitumie fedha za matumizi. | E. Kichwa cha habari |
| (v) 10/08/1990. | F. Mwisho wa barua |
| | G. Kiini cha barua |

2. Mwandishi wa insha za kisanaa ana mchango gani katika kukuza lugha?
3. Bainisha tofauti kati ya insha za kisanaa na zisizo za kisanaa.
4. Eleza matumizi ya herufi kubwa katika uandishi wa insha.
5. Unafikiri nini kitatokea iwapo mwandishi wa insha hatazingatia alama za uakifishaji?
6. Barua ya kirafiki kama njia ya mawasiliano inakabiliwa na changamoto gani kwa sasa?
7. Zipi ni sababu za msingi zinazomfanya mwandishi wa barua asiandike jina la mwandishi katika anwani?
8. Ni kipengele gani cha barua kitakachomwezesha mpokeaji kujua kama barua imewahi au imechelewa?
9. Ukitaka kutuma barua ya kirafiki kwa urahisi, utachagua njia gani? Toa sababu za jibu lako.
10. Chagua mtu mmojawapo wa kuandikiwa barua ya kirafiki, kisha mwandikie barua hiyo.

FOR ONLINE USE ONLY

# Sura ya Tano

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Ufahamu

### Utangulizi

*Ufahamu ni jambo la msingi katika maisha ya kila siku ya mwanadamu. Katika sura hii utajifunza ufahamu wa kusikiliza, kuona na kusoma matini mbalimbali za Kiswahili. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kusikiliza na kusoma habari kwa kuzingatia kanuni za usomaji. Vilevile, utaweza kueleza na kusimulia kwa ufupi ujumbe au mawazo kuhusu tukio ulililoliona. Aidha, utaweza kubaini mawazo yaliyomo katika habari uliyosoma au kuisikiliza na kuweza kufupisha.*

### Dhana ya ufahamu

**Kazi ya 5.1**

*Chunguza picha ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*




FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 90 05/09/2021 15:41

## Maswali

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

1. Unaona nini katika picha hiyo?
2. Unaweza kusema nini kutokana na picha hiyo?
3. Kwa kuzingatia picha hiyo, mtu anaweza kupata taarifa mbalimbali kwa njia gani?
4. Maarifa anayoyapata yanamsaidiaje katika maisha yake ya kila siku?

**Zingatia**

Ufahamu ni hali ya kuelewa jambo na kuweza kulifafanua au kulitolea taarifa. Ufahamu unatokana na kuona, kusoma, au kusikiliza. Umakini mkubwa unahitajika katika kutafakari jambo ulililoona, kulisoma, au kulisikiliza ili uweze kutoa taarifa iliyo sahihi au kujibu maswali kwa usahihi.

Aidha, unaweza kupata uelewa wa jambo au habari kwa kusimuliwa, kusoma, au kujionea mwenyewe. Ili kupata uelewa unapaswa kuwa makini katika kutafakari jambo ulilosoma au kulisikiliza. Ukiwa na ufahamu juu ya jambo fulani unaweza kuokoa muda kwa kutoa taarifa mbalimbali kwa muhtasari. Unaweza pia kulielezea au kuliandika kwa ufupi na kuokoa muda wako na wa yule anayekusikiliza. Aidha, ukiwa na uwezo wa kuelewa jambo ulilosikiliza, kusoma, au kuona utajipatia mafunzo mbalimbali na kuelimika.

Ufahamu ni muhimu katika maisha yetu ya kila siku kwa kuwa hutuwezesha kukuza uelewa wa mambo mbalimbali kama vile: kukuza stadi za kusikiliza, kuzungumza, kusoma, na kuandika; kukuza uwezo wa kujenga hoja juu ya mambo mbalimbali; na kujieleza kwa ufasaha na kwa maelezo mafupi. Vilevile, ufahamu hukuza uwezo wa kuchambua mambo mbalimbali na kuchochea ari ya kujisomea.

FOR ONLINE USE ONLY

## Ufahamu wa kuona

### Kazi ya 5.2

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Chunguza picha ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata kwa kuzungumza na kuandika.*



## Maswali

1. Umeona nini katika picha hiyo?
2. Una maoni gani juu ya kile ulichokiona katika picha hiyo?
3. Unafikiri ni kitu gani kinatakiwa kufanyika ili kuzuia vitendo kama hivyo?
4. Tunga sentensi tano (5) zinazotoa ujumbe kutokana na picha uliyoiona.



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 92 05/09/2021 15:41

## Kazi ya 5.3

*Chunguza picha ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE




## Maswali

1. Tukio gani linaonekana katika picha hiyo?
2. Unafikiri kwa nini polisi wamefika katika eneo la tukio?
3. Andika insha yenye maneno mia mbili (200) hadi mia mbili na hamsini (250) inayohusu tukio ulililoona katika picha hiyo. Insha yako ieleze mambo yafuatayo:
   (i) Vyanzo mbalimbali vya matukio kama hayo.
   (ii) Madhara yatokanayo na matukio kama hayo.
   (iii) Njia mbalimbali za kuepuka matukio kama hayo.
4. Simulia tukio lolote ambalo umewahi kushuhudia kwa macho yako likakusababishia furaha.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 93 05/09/2021 15:41

**Zingatia**

Ufahamu wa kuona unahusu kutazama vitu au matukio na kuyatafakari kwa lengo la kupata ujumbe. Kila siku katika maisha yako umekuwa ukishiriki katika ufahamu wa aina hii bila kujua. Kwa mfano, ukihudhuria kwenye tukio la harusi unaweza kutazama tukio zima na kung'amua jambo fulani ambalo unaweza kulisimulia kwa mtu mwingine hata akapata picha ya kilichokuwa kinaendelea kwenye tukio hilo. Vilevile, matukio mengine huhifadhiwa katika picha. Hivyo, ukichunguza picha hizo kwa makini unaweza kupata ujumbe na kuusimulia kwa mdomo au kwa maandishi. Aidha, unaweza kutumia picha hizo kujibu maswali mbalimbali utakayopewa. Kwa kufanya hivi utakuwa mwepesi kufikiri, kuhusisha matukio na picha, pamoja na kuumba kitu kinachoelezeka katika akili yako.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Ufahamu wa kusikiliza

### Kazi ya 5.4

*Chunguza picha ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*



## Maswali

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

1. Mwalimu anafanya nini katika picha hiyo?
2. Wanafunzi wanafanya nini katika picha hiyo?
3. Kwa nini baadhi ya wanafunzi wanaonekana wakiandika?
4. Unafikiri ni mambo gani ya msingi ambayo wanafunzi wanapaswa kuyazingatia ili tukio unaloona kwenye picha lifanikiwe?

**Zingatia**

Katika ufahamu wa kusikiliza, unapaswa kupata taarifa kwa kusikiliza habari unayosomewa au unayosimuliwa kwa mdomo au kutoka kwenye kifaa cha kurekodia kwa njia ya televisheni, redio, kompyuta, simu ya mkononi, au kwa njia ya mtandao. Ili uelewe vizuri habari au taarifa unayosimuliwa, unatakiwa kwanza, uwe makini kwa kile kinachosimuliwa au kusomwa kwa kuelekeza akili yote kwa mzungumzaji ili uweze kusikia vizuri. Pili, unatakiwa kubainisha mambo muhimu yanayoelezwa katika habari unayosimuliwa. Unashauriwa, kama msikilizaji, uwe na kalamu na karatasi kwa ajili ya kuandika mambo muhimu tu kutoka kwenye habari unayoisikiliza. Tatu, unatakiwa kumtazama usoni msimuliaji ili uweze kupata taarifa za ziada ambazo msimuliaji anaweza kutoa kwa kutumia ishara za mwili. Nne, unapaswa kuwa makini na sarufi ya lugha inayozungumzwa na lafudhi ya msimuliaji. Lafudhi ya msimuliaji inaweza kukukwamisha kuelewa kile kinachosimuliwa iwapo hutakuwa makini. Vilevile, unapaswa kuwa makini kusikiliza misemo, nahau, au methali ambazo zimetumika katika habari unayosikiliza.

FOR ONLINE USE ONLY

### Kazi ya 5.5

*Mwombe mwanafunzi mwenzako akusomee habari ifuatayo wakati wewe ukiwa unamsikiliza kwa makini, kisha akuulize maswali na uyajibu kwa mdomo.*

Kwa mujibu wa Sheria ya Wakimbizi ya mwaka 1998, mkimbizi ni mtu yeyote aliyekwenda nje ya nchi yake kwa sababu ya hofu ya maisha yake kuwa hatarini kutokana na rangi yake, dini, utaifa au kuwa mwanachama wa kikundi fulani cha kijamii au kuwa na maoni ya kisiasa yaliyo tofauti na utawala wa nchi inayohusika. Masuala ya wakimbizi yamekuwa yakiongozwa kisheria duniani. Miongoni mwa sheria zinazoongoza masuala ya wakimbizi duniani ni pamoja na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Wakimbizi wa mwaka 1951, Itifaki ya Umoja wa Mataifa ya mwaka 1967, Itifaki za Maziwa Makuu za mwaka 2009, na Mkataba wa Kampala unaohusu wakimbizi wa ndani wa mwaka 2009.



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 95 05/09/2021 15:41

Akifafanua zaidi kuhusu dhana ya ukimbizi hivi karibuni katika mkutano wa wadau uliofanyika jijini Dar es Salaam, Profesa wa Sheria Khoti Kamanga anawagawa wakimbizi katika makundi mawili. Kuna wale waliolazimika kuzikimbia nchi zao kutokana na hali mbaya ya usalama na wale wanaoyakimbia makazi yao wakiwa ndani ya nchi. Wote hao huchukuliwa kama wakimbizi.

**Chanzo**: *Mwananchi mtandaoni, 06/01/2021*

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maswali

1. Unafikiri ni kichwa gani cha habari kinafaa kwa habari uliyoisikiliza?
2. Sheria iliyotajwa katika habari uliyosikiliza inayofasili dhana ya mkimbizi ni ya mwaka gani?
3. Ni nani aliyefafanua dhana ya ukimbizi katika mkutano wa wadau uliofanyika jijini Dar es Salaam?
4. Makundi yapi ya wakimbizi yamebainishwa katika habari uliyoisikiliza?
5. Unafikiri kwa nini kuna mikataba ya kimataifa inayoongoza masuala ya wakimbizi?

### Kazi ya 5.6

*Mwombe mwanafunzi mwenzako akusomee hadithi ifuatayo, kisha sikiliza kwa makini maswali utakayoulizwa na uyajibu kwa mdomo.*

Bota ni mtoto wa kiume wa familia ya Mzee Bure aliyezaliwa na kulelewa katika mazingira ya kijijini. Baada ya kuhitimu elimu ya msingi, Bota hakubahatika kuchaguliwa kuendelea na masomo ya elimu ya sekondari ingawa alifaulu mtihani. Suse, mama yake Bota, alimshauri mumewe wampeleke kijana wao katika shule binafsi ili aweze kupata elimu ya sekondari. Bure alionesha kusita kwa kuwa hakuwa na uwezo mzuri kifedha. Hata hivyo, kutokana na ushawishi wa mkewe, alikubali ushauri huo na akauza ng'ombe mmoja aliyekuwa naye kisha akampeleka mtoto wake shuleni.

FOR ONLINE USE ONLY

Kutokana na hali ya uchumi kuwa ngumu, wakati mwingine Bota alichelewa kwenda shuleni kwa sababu ya kukosa ada. Mama yake aliumizwa sana na hali hiyo; hivyo, akaamua kuanzisha biashara ya kuchuuza samaki. Aliuza samaki hao kwa kubadilishana na mazao kisha aliuza mazao hayo na kujipatia fedha. Kila faida aliyopata aliielekeza kumsomesha Bota. Maisha yalizidi kuwa magumu kwani kuna wakati walikula mboga bila chumvi na kuoga bila sabuni ili tu Bota apate ada na mahitaji ya shuleni.



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 96 05/09/2021 15:41

Baada ya kuhitimu kidato cha nne, Bota alichaguliwa kujiunga na chuo cha uvuvi ambako alihitimu mafunzo yake. Alipomaliza, hakusubiri kuajiriwa na serikali bali aliamua kujiunga na kikundi cha vijana wajasiriamali. Alichukua mkopo kwenye kikundi chake akanunua zana za uvuvi na kuamua kujiajiri kwenye sekta ya uvuvi.

Mungu si Athumani, biashara ya uvuvi ilimletea tija kwani Bota alipata mtaji mkubwa kiasi cha kuweza kusafirisha samaki ndani na nje ya nchi. Maisha yake na familia yalibadilika na kuwa mazuri. Aliweza kupata fedha za kuwajengea wazazi wake nyumba nzuri na kununua gari. Mama yake alikumbuka maisha ya awali na kusema, "Ama kweli mchumia juani hulia kivulini."

## Maswali

1. Hadithi uliyosikiliza inahusu nini?
2. Kama ungekuwa mzazi wa Bota, ungefanya nini baada ya Bota kutokuchaguliwa kujiunga na masomo ya sekondari?
3. Umejifunza nini kutokana na habari uliyosikiliza?
4. Ukipewa nafasi ya kushauri, utawashauri nini wahitimu wanaosubiri kuajiriwa?

### Ufahamu wa kusoma

**Kazi ya 5.7**

*Chunguza picha ifuatayo, kisha jibu maswali ya zoezi linalofuata.*






KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 97 05/09/2021 15:41

## Maswali

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

1. Mwanafunzi anayeonekana katika picha anafanya nini?
2. Kuna faida gani za kukaa katika mazingira kama hayo?
3. Kwa nini kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na kitabu chake?
4. Unafikiri kalamu na shajara zilizoko katika picha hiyo zitatumika kwa kazi gani?

**Zingatia**

Ili uweze kusoma kwa ufahamu, unatakiwa kuzingatia mambo kadhaa kabla, wakati, na baada ya kusoma. Mambo haya ndiyo yatakusaidia kusoma kwa ufasaha na kuelewa kile kinachoelezwa katika habari hiyo. Mathalani, kabla ya kuanza kusoma, unatakiwa uzingatie akilini mwako mawazo makuu ya habari utakayosoma. Hivyo, jiandae kuelekeza akili yako katika kutafuta mawazo makuu yaliyomo katika habari utakapoanza kuisoma. Kwa kawaida, mawazo makuu ndiyo hujenga na kuifafanua mada inayozungumzwa kwenye habari inayosomwa. Vilevile, kabla ya kuanza kusoma unatakiwa kuelewa mtindo ambao umetumika kuandika habari hiyo. Unatakiwa uelewe kuwa kuna mitindo mbalimbali ya lugha kama vile mtindo wa kishairi, kinathari, dayalojia, au hata mtindo wa kitaaluma. Zaidi ya hayo, unatakiwa uelewe kuwa habari utakayosoma imejengwa na msamiati mbalimbali na huenda ukakutana na maneno mapya kabisa kwako. Unatakiwa uelewe kuwa maneno mapya siyo magumu. Yanaonekana kutoeleweka kwa sababu tu umekutana nayo kwa mara ya kwanza. Ili uelewe maana za maneno hayo mapya, unatakiwa uzingatie muktadha wa matumizi yake katika habari utakayosoma; na wakati mwingine unaweza kutumia kamusi kupata maana za maneno hayo.

FOR ONLINE USE ONLY

Hatua inayofuata baada ya maandalizi ni hatua ya usomaji wenyewe. Wakati wa kusoma habari unatakiwa kuzingatia mambo yote ya maandalizi katika hatua ya kwanza kabla ya kuanza kusoma. Hii ina maana kwamba wakati wa usomaji unatakiwa kuelekeza akili yako kutambua mawazo makuu. Hivyo, unatakiwa kusoma huku ukirejelea maswali uliyojiuliza akilini wakati wa kujiandaa kusoma. Kwa mfano, habari hii inahusu nini? Mawazo makuu katika habari hii ni yapi? Mawazo mengine madogo yanayojenga mawazo makuu ni yapi? Vilevile, unatakiwa kuelekeza akili yako kwenye mitindo ya lugha iliyotumika kuandaa habari hiyo kwa kuelekeza akili yako katika muktadha wa matumizi ya msamiati mpya unaokutana nao wakati wa kusoma.



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 98 05/09/2021 15:41

Hatua inayofuata baada ya kumaliza kusoma ni kupima ufahamu wako. Utaulizwa maswali mbalimbali kama vile kufafanua dhana fulani, kueleza maana za baadhi ya maneno kama yalivyotumika katika habari uliyosoma, kutoa tathmini yako juu ya kile ulichosoma na kupendekeza kichwa cha habari uliyosoma. Maswali mengine yanaweza kulenga kupima uelewa wako juu ya matumizi ya misemo, methali, au nahau kama zilivyotumika katika habari uliyosoma. Unatakiwa kuyajibu maswali ya namna hii kwa kuzingatia uelewa wako wa jumla juu ya lugha pamoja na kuhusisha matumizi yake katika habari uliyosoma. Hivyo, kama utakuwa umejiandaa vizuri kabla ya kuanza kusoma habari na ukazingatia umakini wakati wa kusoma, utakuwa kwenye nafasi nzuri ya kujibu maswali kwa ufasaha.

Kuna aina mbili za usomaji ambazo unaweza kutumia unaposoma habari au taarifa yoyote. Unaweza kusoma kwa haraka au taratibu na kwa umakini. Unaposoma haraka unaimarisha kasi yako ya usomaji kwa kutumia muda maalumu uliotengwa na kiasi maalumu cha maneno. Usomaji wa aina hii unakuwezesha kupitia mambo mengi kwa muda mfupi. Wasomaji wa magazeti, vitabu vya hadithi na wanaojiandaa kwa mitihani hutumia njia hii. Kwa upande mwingine, unaweza kusoma taratibu na kwa umakini ingawa utatumia muda mrefu ukitaka kuchunguza mambo mengi katika habari unayosoma. Usomaji huu hulenga kutafuta mawazo muhimu na vidokezo vya msingi vya mawazo hayo. Unaweza kutumia aina hii ya usomaji unaposoma makala ndefu za kiuchunguzi au vitabu vya kitaaluma.

FOR ONLINE USE ONLY

### Kazi ya 5.8

*Soma kifungu cha habari kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Wavuvi walilazimika kusimamisha kazi yao kwa **takribani** wiki mbili au tatu. Hii ilitokana na mtumbwi wao kuharibika na kuanza kuingiza maji mengi sana kupitia katika mianya iliyokuwa imejitokeza kwenye maungio ya mbao zake. Ingawa kulikuwa na **upo** mzuri wa kufanyia kazi waliokuwa wakitumia, uvujaji wa maji ulikuwa mkubwa mno. Uvujaji huo ulifanya kazi ya **kukumba** maji hayo isiwezekane. Kwa kweli, tatizo hilo lilitokana na uzembe wao wenyewe. Kama wangechukua **hadhari** mapema, tatizo hilo lisingekuwa kubwa kiasi hicho. Kutokana na hali hiyo, ilibidi mtumbwi usimamishwe kufanya kazi ili **ukalafatiwe** kwanza. Hata hivyo, kazi yenyewe ya **ukalafati** haikuwa kubwa na isingeweza kuchukua muda mrefu kiasi hicho, lakini kuliibuka **mushikeli**. Fundi aliyekuwa anaifanya kazi hiyo aliishiwa na **kalafati** ikabidi waagize nyingine kutoka Tanga. Baada ya kalafati kuletwa fundi alilazimika **kuchapusha** kazi



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 99 05/09/2021 15:41

kwani walikuwa wamechelewa sana kufanya kazi yao ya uvuvi. Kutokana na kazi kufanywa kwa njia hiyo, baada ya siku sita tu kazi ikawa imemalizika. Kazi yao ya uvuvi ilianza mara moja; hapakuwa na **ajizi** yoyote.

Walifanya kazi usiku na mchana ili kufidia siku walizopoteza. Aidha, waliamua kuhama kule walikokuwa wakivulia samaki siku zote na kwenda sehemu nyingine kwa matumaini kwamba wangepata samaki wengi zaidi; lakini wapi! Hawakupata samaki wengi kama walivyotarajia huku baadhi yao wakiandamwa na magonjwa. Wavuvi hao waliamua kurudi kule walikozoea, ambako siku zote kulikuwa hakuwatupi mkono. Kama wahenga wanenavyo, "Zimwi likujualo halikuli likakwisha", waliporudi kwenye eneo lao la awali walipata samaki si haba.

## Maswali

1. Habari hii inahusu nini?
2. Eleza maana za maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika habari uliyosoma.
   (i) takribani
   (ii) upo
   (iii) kukumba
   (iv) hadhari
   (v) kalafati
   (vi) mushikeli
   (vii) chapusha
   (viii) ajizi
3. Kwa nini zoezi la ukalafati lilichelewa?
4. Kwa nini wavuvi waliamua kwenda kuvua samaki mahali kwingine badala ya walikokuwa wamezoea?
5. Pendekeza kichwa cha habari kinachofaa kwa habari uliyosoma.

### Kazi ya 5.9

*Soma hadithi hii kimyakimya, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Hapo zamani za kale alikuwepo bwana mmoja aliyeitwa Ngadure. Alijenga nyumba kubwa pale kijijini, kisha akaoa. Waliishi pamoja na mkewe na kubahatika kupata mtoto wa kiume. Katika kuendelea na maisha yao, waliamua kutafuta paka na kumfuga. Paka huyo akawa mkubwa na kubadilika kuwa **nunda**. Nunda huyo aliwameza watu wote pale **kiamboni** na nyumba zao zikasalia

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 100 05/09/2021 15:41

tupu; hazina watu. Ngadure naye alimezwa, wakabaki mke wake na mtoto wake tu ambao walienda kumtembelea kaka wa mke wa Ngadure.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Siku moja mtoto alimuuliza mama yake, "Mbona nyumba hizi zote hazina watu wanaoishi humo?" Mama yake alimjibu, "Mhh! Mwanangu, hapo zamani baba yako alimfuga paka. Paka yule aligeuka nunda na kuwameza watu wote pamoja na baba yako isipokuwa sisi tu ndio hatukumezwa na paka huyo." Baada ya kusikia hivyo, mtoto yule alimwambia mama yake atafutiwe vibuyu saba na **manda** saba. Vikatafutwa na akapatiwa. Aliomba pia apatiwe upinde na mishale ya baba yake. Mtoto huyo aliondoka na kuelekea mwituni.

Mtoto huyo akarandaranda huko mwituni siku ya kwanza, ya pili, ya tatu, ya nne, ya tano, hadi siku ya sita. Ilipotimu majira ya adhuhuri ya siku ya saba alimwona kima akamkamata na kurudi naye nyumbani kwao huku akiimba, "Mama wee! Huyu ndiye nunda mla watu! Eee, eeee mama!" Aliimba wimbo huo mpaka akafika nyumbani kwao. Mama yake alipomwona alimwambia, "Makubwa! Mwanangu wee, huyo siye nunda mla watu. Eee! Mwana eee!" Baada ya siku mbili mtoto alimwagiza mama yake amtafutie tena vibuyu vingine saba vya maji na manda saba. Alipewa, vitu hivyo na kuelekea tena kule mwituni.

Huko alimkamata paa na kurudi kwao huku akiimba, "Mama wee! Huyu ndiye nunda mla watu! Eee, eeee mama!" Alipofika nyumbani akaambiwa siye. Akakaa siku mbili akapumzika. Hapo akasema, "Sirudi nyumbani tena mpaka nije naye." Alirudi mwituni na kumtafuta mpaka ikafika siku ya saba vilipomalizika vitu vyake, yaani maji na manda. Siku hiyo alikutana na mnyama mkubwa sana akampiga, akaondoka naye. Alipofika nyumbani, mama yake alithibitisha kuwa mnyama yule ndiye nunda mla watu.

Ilipofika asubuhi akatafutiwa **staftahi**. Alipomaliza staftahi yake aliomba kisu cha baba yake, akaletewa. Alipoletewa kisu kile akapasua tumbo la mnyama yule. Ama kweli, "Ukistaajabu ya Musa utaona ya Firauni." Tumbo lile lilikuwa limejaa watu wote waliomezwa. Wote wakatoka kwa furaha.

Watu wale walifanya karamu kubwa na kumpongeza kijana yule kwa kuwaokoa. Usiku kucha ilisikika mirindimo ya ngoma, **tumba**, zeze, marimba, vinubi, na vinanda vilivyokuwa **vikihanikizwa** na sauti za vigelegele vya akina mama. Kijana yule alipewa zawadi nyingi, na Mfalme wa **kiambo** kile alimpa nusu ya ufalme wake.

FOR ONLINE USE ONLY

## Maswali

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

1. Hadithi uliyosoma inahusu nini?
2. Umejifunza nini kutokana na hadithi uliyosoma?
3. Maneno yafuatayo yanamaanisha nini katika hadithi uliyosoma?
   (i) nunda
   (ii) kiambo
   (iii) manda
   (iv) staftahi
   (v) tumba
   (vi) hanikiza
4. Unafikiri kwa nini Mfalme alimpatia yule kijana nusu ya ufalme wake?
5. Wasimulie wenzako hadithi hiyo kwa maneno yako mwenyewe.

**Zingatia**

Unaweza kusoma kimyakimya bila kutoa sauti. Katika usomaji huu unatakiwa kupitisha macho katika kila mstari harakaharaka bila kutoa sauti. Unaunganisha neno lililotangulia na lile linalofuata huku ukielekeza akili yako kuchambua mambo muhimu yanayojitokeza na kuyahifadhi kichwani. Ukitumia namna hii ya usomaji utapata nafasi ya kupima kiasi cha kuelewa mambo. Vilevile, wakati mwingine, utajiepusha na lawama ya kusumbua wengine kwa kelele za sauti na unaweza kusoma maandishi mengi kuliko ambavyo ungesoma kwa sauti.

### Kazi ya 5.10

*Soma taarifa ifuatayo, kwa sauti huku ukizingatia matamshi na lafudhi fasaha ya Kiswahili, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Kazamoyo**

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia Ajira za Watoto (TAKUAWA) nchini Sagamoyo, Dkt. Kamagaza Kanihura, ametangaza kiama kwa wale wote wanaowaajiri watoto walio chini ya umri wa miaka kumi na minane (18). Akiongea na vyombo vya habari jijini Kazamoyo leo, Dkt. Kanihura amesisitiza kuwa TAKUAWA itahakikisha inawakamata na kuwachukulia hatua za kisheria wale wote ambao wanawaajiri watoto wadogo. Pamoja na kutoa kauli hiyo, Dkt. Kanihura amekabidhi taarifa ya awali ya uchunguzi wa ajira kwa watoto kwa Waziri wa Haki, Mheshimiwa Tafuna Kamamchwa. Taarifa hii ilihusu utafiti uliofanywa na TAKUAWA ambapo ilitakiwa kuchunguza kuwapo kwa watoto walioajiriwa nchini Sagamoyo. Kupitia uchunguzi huu ambao unafanyika kwa awamu, TAKUAWA tayari imefanikiwa kuokoa zaidi ya watoto kumi.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 102 05/09/2021 15:41

**Katumbarazi**

Wakazi wa Kijiji cha Janda, mkoani Katumbarazi, wameamua kushirikiana kujenga mabweni kwa ajili ya shule ya sekondari iliyoko kijijini humo. Akiongea kwa bashasha katika hafla ya kuzindua mabweni hayo, Mkuu wa Mkoa wa Katumbarazi, Brigedia Chekero Rukweche, amewashukuru wanakijiji hao kwa kuona umuhimu wa kujenga mabweni kwa sababu wanafunzi walikuwa wakihangaika kutembea umbali mrefu kwenda shuleni na kurudi nyumbani. Jumla ya mabweni manne yamekamilika, ambapo mawili yatatumiwa na wavulana na mawili yatatumiwa na wasichana. Ujenzi wa mabweni hayo umegharimu zaidi ya shilingi milioni 150.9 ambazo ni michango iliyotolewa na wanakijiji hao sambamba na nguvukazi.

## Maswali

1. Unafikiri kwa nini nchi ya Sagamoyo iliamua kuwa na Taasisi ya Kuzuia Ajira za Watoto?
2. Kwa nini Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia ajira ya watoto nchini Sagamoyo alikabidhi ripoti ya ukaguzi wa ajira kwa watoto kwa waziri?
3. Unafikiri juhudi zipi zinapaswa kuchukuliwa ili kuondoa vitendo vya kuajiri watoto katika jamii yako?
4. Wakazi wa Kijiji cha Janda mkoani Katumbarazi walifanya jambo gani?
5. Unafikiri kwa nini wakazi wa Kijiji cha Janda hawakusubiri serikali ifanye jambo ambalo walilifanya wao?

**Zingatia**

Kinyume cha kusoma kimyakimya ni kusoma kwa sauti. Kusoma kwa sauti kutakuwezesha kuimarisha ujuzi wako katika kutamka maneno kwa kufuata kanuni na lafudhi ya Kiswahili sanifu. Usomaji wa namna hii utakusaidia kujipima uwezo wako wa kutamka maneno jinsi inavyotakiwa, kupima kasi yako ya usomaji, pamoja na uwezo wako wa kuelewa yale unayosoma. Hivyo, unaposoma kwa sauti, hakikisha unazingatia matumizi sahihi ya alama za uandishi, matamshi sahihi ya maneno pamoja na kasi ya usomaji ili kama kuna msikilizaji naye apate maana sahihi ya habari unayosoma. Njia mojawapo ya kujifunza matamshi ya lugha ni kusoma maandishi kwa sauti na kuzingatia kanuni za lugha hiyo. Endapo utakosea matamshi ya baadhi ya maneno au kiimbo cha sentensi unaweza kusababisha mabadiliko ya maana au ukaibua neno ambalo halina maana kabisa katika lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, endapo utatamka neno *kura* badala ya *kula* katika usomaji wako, utasababisha msikilizaji ahangaike kuelewa



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 103 05/09/2021 15:41

unachomaanisha. Vilevile, iwapo mwandishi wa tungo, *"Alilima barabara ikapendeza sana"* alikuwa na maana ya *barabara*, yaani njia; halafu ukatamka *"Alilima ba**ra**bara ikapendeza sana"* utaibua maana ambayo siyo ya *njia* kwa sababu mkazo umetiwa pasipostahili kulingana na maana iliyokusudiwa. Kwa hiyo, msomaji hana budi kuepuka makosa katika usomaji wake.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kusoma kwa burudani

### Kazi ya 5.11

*Chunguza picha ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata kwa njia ya mazungumzo na kwa kuandika.*




## Maswali

1. Wanafunzi wanafanya nini katika picha hiyo?
2. Unafikiri kwa nini wanafunzi hao wanaonekana kuwa makini kwenye vitabu vyao ?
3. Unafikiri unaweza kunufaika na kitendo kinachofanyika kwenye picha? Kwa nini?
4. Kwa nini kila mwanafunzi ana kitabu chake ambacho ni tofauti na cha mwenzake?



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 104 05/09/2021 15:41

**Zingatia**

Kusoma kwa burudani kunaweza kufanyika kwa kusoma kwa sauti au kusoma kimyakimya. Lengo la usomaji huu huwa ni kujiburudisha tu. Usomaji wa aina hii unahusisha kujisomea magazeti, majarida na vitabu tofauti na vile vinavyotumika darasani. Katika usomaji wa burudani, unaweza kwenda maktabani kujisomea vitabu, magazeti, majarida au kuazima kitabu unachokihitaji siku hiyo. Pamoja na kujiburudisha, unaweza pia kujiongezea maarifa yanayoihusu jamii. Vilevile, unaweza kuimarisha uwezo wako wa kutumia lugha katika miktadha mbalimbali. Pamoja na kuburudika, unapaswa pia kujijengea tabia ya kujipima kila unaposoma matini yoyote. Kujipima huku kunaweza kufanywa kwa kujiundia utaratibu wa kuweka kumbukumbu ya vitu au makala uliyojisomea. Vilevile, unaweza kuwa unaandika dondoo za mawazo makuu ya makala, vitabu, au majarida uliyojisomea.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kazi ya 5.12

*Soma shairi lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Badilisha mtazamo, yaache ya **kukariri**,
Maisha yabadilika, wakati wawa ukuta,
Kazi yataka ujuzi, vyeti using'ang'anie,
Hapa kazi ndiyo mbiu, sije jisahaulisha.

Agizo uzingatie, acha **randaranda** ovyo,
Tumia ujuzi wako, zao la elimu yako,
Kazi fanya kwa bidii, upate mradi wako,
Siku zote zingatia, kujua ndiko kuishi.

Siangalie ya ndugu, wala jirani mzee,
Yeye ajira lipata, kwa hizo zama za nyuma,
Zama zimepinduliwa, hilo weka akilini,
Tumia ujuzi wako, upate wako mradi.

Lako pato ukishika, madhila **hukuambaa**,
Kuku wa John kaibwa, wewe kando utakuwa,
Hayakusumbui nafsi, moyo wako **utabwaga**,
Usikose zingatia, ujuzi **kipaumbele**.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 105 05/09/2021 15:41

## Maswali

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

1. Shairi hili linahusu nini?
2. Pendekeza kichwa kinachofaa kwa shairi hili.
3. Ni ujumbe gani unaoupata kutoka katika shairi hili?
4. Eleza mawazo makuu yanayopatikana katika shairi ulilolisoma.
5. Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi hilo.
   (a) kukariri
   (b) randaranda
   (c) hukuambaa
   (d) utabwaga
   (e) kipaumbele

### Kazi ya 5.13

*Chagua kitabu kimoja chenye hadithi unachokipenda, kisha kisome na kutoa ripoti ya kitabu hicho. Andika ripoti hiyo kwa maneno kati ya mia mbili (200) hadi mia mbili hamsini (250). Unapoandika ripoti hii zingatia mambo yafuatayo:*

(i) Jina la kitabu
(ii) Mwandishi wa kitabu
(iii) Mchapishaji wa kitabu na mwaka kilipochapishwa
(iv) Maudhui ya kitabu
(v) Lugha iliyotumika katika kitabu hicho
(vi) Mafunzo yanayopatikana katika kitabu hicho
(vii) Tathmini yako ukihusisha na jamii unamoishi

FOR ONLINE USE ONLY

## Ufupisho

### Kazi ya 5.14

*Mwombe mwanafunzi mwenzako akusomee hadithi ifuatayo, kisha ifupishe kwa kuzungumza.*

"Aaaa, kile kilikuwa kisasili tu! Ni utabiri wa aina fulani uliokuwa na madhumuni ya kuwahadharisha watu juu ya yanayokuja." Tulicheka tena kwa jinsi Ngobongo alivyolitumia neno lile "kisasili". Hata hivyo, mimi nilimdunga Ngobongo katika kucheka kwangu. Alicheka kwa namna ileile ya kawaida. "Sawa," nilikubaliana na kauli ya Ngobongo lakini sikutaka tena kumpa nafasi. Maadamu kaanza, lazima nimalize. Basi nikaendelea, "Lakini utabiri wenyewe ulikuwa na msingi wa uchawi. Isitoshe uchawi ni uchawi tu Ngobongo," nilimwambia. "Vipi, habari



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 106 05/09/2021 15:41

ya kupiga mateke mapakacha huko kwenu Kirungu? Nasikia ukitembea usiku huko na kuliona pakacha usilipige teke. Ukilipiga, hiari yako. Mara utalisikia likikuambia, "Bwana we, huoni kwamba unaniumiza? Katafute mpira uupige shuti, mimi ni binadamu mwenzako!" Vicheko vingine vya pamoja vikapasuka.

"Wewe Ngobongo, kakusimulia nani hadithi hiyo?" Nilikuwa nikikiendeleza kicheko changu huku nikijiambia moyoni kwamba hivyo ndivyo watu wengi wa huku vijijini wanavyoamini; tukiwemo sisi wenyewe wa Kirungu. Kwa hakika, ndivyo wengi tunavyoamini bila ya kuuliza maswali. Hata hivyo, mimi najua huo ni upuuzi mtupu kwani utotoni mwangu nimeshapiga mateke mapakacha mengi na sikusikia pakacha hata moja likisema, kwiii!

"Sikusimuliwa na mtu, nimesikia tu maneno yanayopita hewani." Alijibu Ngobongo pasi na kunitazama usoni. "Basi kusikia si kuona Ngobongo." Nilijaribu kuvunja makali ya maneno yake. Nikamaliza jibu langu huku napiga funda lingine la sharubati ya baridi. "Kweli Kwiyanga." Aliungama Ngobongo kwa upole wake uleule unaozimua joto mara moja na kupeperusha hamaki kama zimeanza. "Hata hivyo, mimi sikukasirika, niliona ni vyema tu kukusanya kadhia zinazochekesha na kuelimisha."

**Zingatia**

Unapaswa kuzingatia kwa makini lugha iliyotumiwa unapofupisha habari uliyosoma au kusikiliza. Katika kufanya hivyo, unatakiwa kutafuta maelezo ya ziada ambayo unaweza kuyaondoa bila kuathiri ujumbe uliokusudiwa. Vilevile, unapaswa kutafuta maneno mapya yanayoweza kutumika badala ya fungu fulani la maneno au badala ya sentensi nzima. Kwa mfano, fungu la maneno "nyanya, vitunguu, hoho, mchicha, chumvi, bizari, mdalasini, spinachi, kabiji na ngogwe" yanaweza kufupishwa kwa kusema "viungo na mbogamboga." Aidha, unapofupisha habari unatakiwa kuangalia mambo muhimu yanayojitokeza katika habari ili usipunguze ujumbe unaotolewa. Inashauriwa kuwa usiondoe maneno ya msingi ambayo yamo katika habari.



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 107 05/09/2021 15:41

### Kazi ya 5.15

*Soma habari ifuatayo, kisha ifupishe kwa maneno yasiyozidi hamsini (50).*

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Wakapita nyika, pululu na tambarare kwenye eneo la Safu ya Milima ya Usambara. Walipokaribia eneo la Mto Wami, walikabiliana na lori refu la kubebea shehena nzitonzito. Lori hilo lililokuwa linatokea Dar es Salaam kuelekea Arusha lilikuwa limewasha taa mchana. Lilikuwa likija kwa kasi huku likiyumbayumba barabarani. Dereva wa daladala iliyokuwa inaelekea Chalinze aling'amua ghafla kwamba mambo ni tenge tahanani. Alijaribu kukikwepa kichwa cha lori kilichokuwa kimemkodolea macho kama simba wa Hifadhi ya Wanyama ya Serengeti bila mafanikio. Alikuwa amechelewa mno.

Lori lile lilikwangua daladala na kuirarua. Ulisikika mlio, kwa-ka-ra-kwa-ka-ra, pfyuuuuuuu! Likapita juu ya ile daladala na kwenda *kuyafukunyua* magari mengine sita yaliyofuatana nayo. Vyuma vilikutana na vyuma, mabati yakaumana na mabati na viungo vya watu kumenyeka na kukatika. Kufumba na kufumbua wingu la vumbi lilikuwa limetanda barabarani.

Baadhi ya wanahabari waliokuja kupiga picha walijikuta wamelazwa hospitalini kwa mshtuko kutokana na mandhari yale ya kutisha. Walikuwa hawajawahi kuona mkasa mbaya kama huo barabarani. Watu arobaini walifariki papo hapo na wengine kumi na watatu walijeruhiwa. Baadhi ya majeruhi hao waliumizwa vibaya sana.

Mwenyekiti wa Chama cha Nyumbani alinusurika na alionekana pasi kupata jeraha lolote. Alionekana akikimbia huku na kule kuwaokoa majeruhi na kuopoa maiti. Waliomwona akijumuika na wenyeji wa eneo la tukio katika uokoaji, wanasema hakuonesha kujeruhiwa; isipokuwa uchovu tu. Alisimama ghafla akajishika nyongani na kusema, "Jamani ni muhimu kuzingatia suala la kasi katika uendeshaji wa vyombo vya usafiri na sheria nyingine za barabarani."

FOR ONLINE USE ONLY

## Kazi ya 5.16

*Soma mazungumzo haya, kisha jibu maswali yanayofuata.*

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Nanzia**: *(Akimkumbatia rafiki yake Helena.)*

Hee! Helena! Helena habari za likizo?

**Helena**: Ni nzuri Nanzia.

**Nanzia**: Habari za Masasi?

**Helena**: Nzuri pia rafiki yangu.

**Nanzia**: Jamani poleni kwa mafuriko; yanatisha!

**Helena**: Usiseme Nanzia. Mafuriko yanatisha.
Tulifikiri ni kama ...

**Nuru**: *(Akidakiza.)* Enhe! Hebu tusimulie dada.

**Helena**: Hapo kwetu ndipo hasa mkondo wa maji na mawe ulipopitia. Ilikuwa bahati, kwani mzee mmoja aliwahi kupiga kelele tukatoka nje kabla ya balaa lile; halafu tukakimbilia kwenye mwinuko.

**Nanzia**: Ilikuwa usiku au mchana?

**Helena**: Usiku, kama saa tano au sita maana tulikuwa tumekwishalala.

**Nuru**: Yaani mlikimbia?

**Helena**: Yule mzee aliwahi kuona yale maporomoko ya mawe na miti na maji mengi yakitiririka toka mlimani …

**Nuru**: Jamani Helena, mawe na miti?

**Helena**: Eee! Mawe makubwa yaliviringishwa nayo yakavunja miti huku maji yakimong'onyoa ardhi. Chochote kilichokutwa na maji hayo kilisombwa. Gari la misheni lilikumbwa, likasombwa na kuharibiwa kabisa. Basi, maji yale yalipofika kijijini kwetu, loo!

**Nanzia**: *(Akishika midomo kwa masikitiko.)* Nyumba zenu?

**Helena**: Nyumba zetu zilifagiliwa tukiziona hivihivi kwa macho yetu. Vitu vyote vilisombwa tukabaki hivihivi bila hata bakuli, sufuria wala kijiko …

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 109 05/09/2021 15:41

**Nuru**: *(Akiwa ameshika kichwa.)* Helena unasema kweli? Sasa ikawaje?

**Nanzia**: Sasa wewe na ndugu zako mlilala wapi?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Helena**: Wee! Tulipata shida. Tulilala nje. Tulikata miti tukatengeneza wigo. Baada ya siku mbili tatu tuliletewa mahema na misaada mingine.

**Nanzia**: Jamani! Helena poleni sana. Tulipopata habari za mafuriko, tulikukumbuka na kukusikitikia.

**Helena**: Asante sana rafiki yangu.

## Maswali

1. Mafuriko yanayozungumziwa yalitokea wilaya gani?
2. Kwa nini Helena alifikiri mafuriko ni kiama?
3. Mafuriko yalitokea wakati gani?
4. Taja vitu vilivyoharibiwa na maji katika mazungumzo hayo.
5. Andika kichwa cha habari hii kisichozidi maneno matano.
6. Andika ufupisho wa habari hii kwa sentensi zisizozidi tano.

### Zoezi la marudio la 5

1. Ghani shairi lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata.

**Ndege wangu nampenda**

Mhariri mchapaji, niweke japo pembeni,
Niwaeleze walaji, walao ndege porini,
Ndege wangu mjuaji, mgumu hapatikani,
Nampenda ndege wangu, sababu kanipa tabu.

Ndege nahangaikia, huku na kule porini,
Naye **kanidengulia**, nikawa nipo tabuni,
Wengi nikawatumia, mafanikio sioni,
Nampenda ndege wangu, sababu kanipa tabu.

Wa kwanza nikamtuma, jinale ndiye Mwazani,
Amshike kwa mtama, hata kama mtegoni,
Mwazani akachutama, hakumtia **kapuni**,
Nampenda ndege wangu, sababu kanipa tabu.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 110 05/09/2021 15:41

Domitila ni wa pili, nikamweleza yakini,
Fanya kila **hila** hali, nimtie mikononi,
Ndege japo ni mkali, tamtuliza tunduni,
Nampenda ndege wangu, sababu kanipa tabu.

Afiswa ndiye wa tatu, nitamweleza yakini,
Katika ndege watatu, mmoja namtamani,
Usimlete kifutu, ambaye simtamani,
Nampenda ndege wangu, sababu kanipa tabu.

Afiswa katekeleza, akamtega mtini,
Na mtama wa kumeza, ndege akautamani,
Akajaa kama pweza, anavyojaa wavuni,
Nampenda ndege wangu, sababu kanipa tabu.

Ndege nikakabidhiwa, nikamtia tunduni,
Sitaki akatolewa, na mwingine asilani,
Na jina akatungiwa, MAGNET la utani,
Nampenda ndege wangu, sababu kanipa tabu.

Siku napata safari, ya kwenda zangu mjini,
Nanunua vya **fahari**, ndege awe furahani,
Fulana na vya **hariri**, kitambaa na **kidani**,
Nampenda ndege wangu, sababu kanipa tabu.

Tama hapa nimefika, ndege yuko furahani,
Hakuna wa kumshika, na sasa yupo nyumbani,
Chumbani arukaruka, hajali wala haoni,
Nampenda ndege wangu, sababu kanipa tabu.

**Chanzo**: *Uhuru, Aprili 12, 1991*

## Maswali

i. Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi ulilolghani: (a) kanidengulia (b) kapuni (c) hila (d) fahari (e) hariri (f) kidani
ii. Unafikiria ni walaji gani anaozungumzia mwandishi katika ubeti wa kwanza?
iii. Mwandishi aliwapenda ndege wangapi?
iv. Mtama anaozungumzia mwandishi katika ubeti wa sita unaweza kulinganishwa na nini katika hali ya kila siku maishani?
v. Unafikiri ni kwa nini mwandishi anamalizia na sentensi hiyo katika mstari wa mwisho wa kila ubeti?



FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE
FOR ONLINE USE ONLY

2. Chagua jibu sahihi katika maswali yafuatayo:
   (i) Dhana ya ufahamu hufasiliwaje?
   (a) Kujua, kufikiri, na kuelewa jambo na vitu
   (b) Kuona, kusikiliza, na kutafakari
   (c) Kujua, kuelewa, na kuweza kufafanua jambo
   (d) Kusoma, kusikiliza, na kuona
   (e) Kugusa, kuonja, na kuona

   (ii) Ufahamu unasaidia jamii katika mambo mengi yakiwemo:
   (a) Kufurahisha na kuelimisha jamii.
   (b) Kuokoa muda na kupunguza gharama.
   (c) Kutafakarisha na kusikiliza.
   (d) Kuelimisha, kuchekesha, na kusoma.
   (e) Kutafakarisha na kutambua mawazo makuu.

   (iii) Adela anatikisa chupa ya dawa ya kikohozi kabla ya kunywa, hii ina maana kuwa Adela .......................
   (a) hakuelewa na hakutenda kulingana na masharti ya daktari.
   (b) ameelewa na kutenda kulingana na maagizo ya daktari.
   (c) ataelewa na kutenda kulingana na maelekezo ya daktari.
   (d) alielewa na anatenda kulingana na maelekezo ya daktari.
   (e) anaelewa na kutenda kulingana na maelekezo ya daktari.

   (iv) Sentensi ipi inaeleza ukweli kuhusu ufahamu wa kusoma na kusikiliza?
   (a) Ufahamu wa kusoma unazingatia habari mwanzo hadi mwisho na ule wa kusikiliza unazingatia kusikiliza habari hadi mwisho.
   (b) Ufahamu wa kusoma unazingatia uchambuzi wa maana ya neno, sentensi na habari yote na ufahamu wa kusikiliza unazingatia kusikiliza kwa makini yale yanayosemwa na mtu mwingine.
   (c) Ufahamu wa kusoma unazingatia vitabu na makala na ufahamu wa kusikiliza unazingatia masikio na mdomo.
   (d) Ufahamu wa kusoma unamzingatia mwandishi na ufahamu wa kusikiliza unamzingatia msomaji.
   (e) Ufahamu wa kusoma unamzingatia mwalimu na ufahamu wa kusikiliza unamzingatia msikilizaji.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE
FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 112 05/09/2021 15:41

3. Jibu maswali yafuatayo:
   (a) Stadi ya kusoma ina umuhimu gani katika ufahamu?
   (b) Eleza umuhimu wa kuzingatia matamshi sahihi wakati wa kusoma kwa sauti.
   (c) Msomaji anawezaje kupata maana za msamiati uliotumiwa katika kifungu cha habari?
   (d) Kwa nini mtu anatakiwa asikilize habari kwa makini?

4. Chora picha ya kitu chochote unachokiona kwenye mazingira ya shule yako, kisha ielezee picha hiyo kwa maneno kati ya 50 na 70.

5. Oanisha maelezo yaliyopo katika orodha **A** na dhana zilizopo katika orodha **B** kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi.

| Orodha A | Orodha B |
|---|---|
| (i) Kuzingatia habari, kutambua mawazo makuu, kuelewa mtindo uliotumika na kuonesha uelewa wa jambo. | A. Kusoma kwa sauti |
| (ii) Aina za ufahamu | B. Kusoma kimyakimya |
| (iii) Msomaji hufumba kinywa na kupitisha macho kwenye maandishi harakaharaka. | C. Ufupisho |
| (iv) Kuimarisha ujuzi wa kutamka kwa kufuata kanuni na lafudhi ya Kiswahili. | D. Kusikiliza, kusoma, na kuona |
| (v) Kutokuondoa mawazo ya msingi katika habari. | E. Mambo makuu ya kuzingatia katika ufahamu |
| | F. Kupima ufahamu |
| | G. Kuchambua maandishi |

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE
FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 113 05/09/2021 15:41

# Faharasa

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Aghalabu** mara kwa mara, kwa kawaida, mara nyingi

**Baruapepe** ujumbe unaotumwa kwa njia ya elektroniki kupitia kompyuta au simu inayounganishwa kwenye mfumo wa mtandao wa intaneti

**Dhamira** nia ya kufanya jambo

**Faksi** mfumo wa kutuma matini kielektroniki kwa kutumia simu

**Falsafa** imani ya mtunzi kuhusu ukweli wa maisha

**Fanani** msanii katika fasihi simulizi, mtu anayesimulia hadithi, methali, vitendawili n.k.

**Fasili** maelezo ya maana ya neno

**Irabu** aina ya sauti ya lugha inayotamkwa bila kuwepo kizuizi chochote kwenye mkondohewa kutoka mapafuni kupitia kinywani na puani kwenda nje

**Kategoria** jumla ya vitu vya aina fulani vinavyoweza kuwekwa pamoja kwa mujibu wa sifa zinazofanana

**Kidahizo** neno kuu katika kamusi ambalo huingizwa kwa rangi iliyokoza na hutolewa fasili, namna ya kulitamka, aina ya neno pamoja na kuelezwa sifa zake za kisarufi na fasili yake

**Kiimbo** namna ya usemaji ambapo mawimbi ya sauti hupanda na kushuka wakati wa kuzungumza

**Kitomeo** kidahizo kinachoingizwa kwenye kamusi kikiwa na maelezo yake

**Kituo** alama ya uandishi inayotumika kama pumziko kubwa mwishoni mwa sentensi au ubeti

FOR ONLINE USE ONLY

| | |
|---|---|
| **Konsonanti** | sauti ambayo hutamkwa kwa kubana au kuzuia mkondohewa kutoka mapafuni kwenda nje kupitia ama chemba ya kinywa au chemba ya pua |
| **Lafudhi** | matamshi ya mzungumzaji yanayotokana na lugha yake ya mwanzo au lugha zinazomzunguka |
| **Lahaja** | tofauti katika matamshi, maumbo na matumizi ya maneno katika maeneo mbalimbali kwa lugha yenye asili moja |
| **Lufufu** | -engi, -ingi, lukuki |
| **Majigambo** | maneno ya kujisifia au kujikweza |
| **Maleba** | mavazi maalumu yanayovaliwa na wasanii wanapokuwa wanafanya maonesho mbalimbali ya lugha yenye asili moja. |
| **Mandhari** | mwonekano wa mahali unaojumuisha ardhi, miti, mito, milima au mabonde |
| **Maskani** | mahali anapoishi mtu |
| **Mathalani** | kiunganishi ambacho hutumika kulinganisha kitu kinachoongelewa na kingine; kwa mfano |
| **Mawimbi** | mtutumko wa sauti zinazosafiri katika hewa |
| **Misimu** | neno au maneno yanayozuka na kutumiwa na watu kwa muda fulani na baadaye kupotea |
| **Mizani** | idadi ya silabi katika mstari wa shairi au utenzi |
| **Mizungu** | matendo ya hekima yanayofunzwa kwa siri aghalabu kwa kundi la watu mahususi |
| **Mkabala** | utaratibu unaofuatwa kukabili jambo |



FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE
FOR ONLINE USE ONLY

KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 115 05/09/2021 15:41

| | |
|---|---|
| **Mkarara** | ni mstari wa mwisho katika ubeti wa wimbo au shairi unaoimbwa kwa pamoja |
| **Mkazo** | utamkaji wa nguvu zaidi katika sehemu ya neno |
| **Mshororo** | mstari mmojawapo ulio kwenye kila ubeti wa shairi au utenzi |
| **Muktadha** | mazingira yanayobainisha mahali jambo lilipofanyika |
| **Ngisha** | mawimbi madogo ya chini kwa chini baharini |
| **Njeo** | aina ya mofu inayopachikwa kwenye kitenzi kuonesha wakati |
| **Nyenzo** | vifaa vya kufanyia shughuli fulani |
| **Rashasha** | kalamu za rangi zinazotumika kuchorea au kuandikia zenye wino mzito wenye rangi mbalimbali |
| **Rejesta** | bahasha maalumu inayotumiwa kupostia vitu vya thamani |
| **Silabi** | sehemu ya neno inayoundwa na konsonanti na irabu au irabu peke yake na hutamkwa kwa pamoja kama fungu moja la sauti |
| **Takriri** | umbo la neno, silabi, au fungu la maneno linaloandikwa kwa kurudiarudia |
| **Tamathali** | usemi unaotumika kwa maana ambayo ni kinyume na maana ya kawaida ili kufunza jambo |
| **Tanbihi** | maelezo yanayotolewa sehemu ya mwisho au chini ya ukurasa au sura kwa ajili ya kutoa maelezo zaidi kuhusu hoja fulani iliyozungumziwa awali ndani ya ukurasa au sura hiyo |
| **Taswira** | picha ya mambo au vitu inayomjia au anayoiwaza mtu akilini mwake |

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE
FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 116 05/09/2021 15:41

| | |
|---|---|
| **Tathilitha** | shairi lenye mishororo mitatu kila ubeti |
| **Tathinia** | shairi lenye mishororo miwili kila ubeti |
| **Uakifishaji** | uwekaji wa alama za uandishi kama vile nukta, mkato, nuktamkato na kadhalika katika maandishi |
| **Ubeti** | kifungu cha maneno katika shairi au utenzi |
| **Umahiri** | uwezo wa kufanya jambo fulani kwa ubora zaidi |
| **Urari** | ulinganifu au usawa |
| **Vina** | Silabi za sauti za namna moja zinazotokea baada ya kila mizani kadhaa, hususani katikati na mwisho wa kila mstari wa ubeti wa shairi au utenzi |
| **Visawe** | maneno mawili au zaidi yanayokaribiana sana kimaana |

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE
FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 117 05/09/2021 15:41

# Bibliografia

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Baraza la Kiswahili la Taifa. (2016). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers (T) Ltd.

Kaduguda, R., Kiango, J. & Ipara, I. (2013). *Kiswahili Shule za Sekondari Kidato cha Kwanza.* Dar es Salaam: OUP.

Karama, S., & Saidi, M. (1983). *Maelezo ya Methali za Kiswahili*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers (T) Ltd.

Kiango, J. G. (2009). *Stadi za Lugha ya Kiswahili Utungaji II.* Dar es Salaam: TUKI.

Kihore, Y. M., Massamba, D. P. B., & Msanjila, Y. P. (2003). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA): Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D. P. B. (2009). *Stadi za Lugha ya Kiswahili: Ufahamu na Ufupisho I.* Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D. P. B. (2009). *Stadi za Lugha ya Kiswahili: Ufahamu na Ufupisho II.* Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D. P. B., Kihore, Y. M., & Hokororo, J. I. (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA): Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D. P. B., Kihore, Y. M., & Msanjila, Y. P. (2004). *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu (FOKISA): Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

Mbijima, R. J. (2020). *Uduni Wangu: Ngonjera za Watoto.* Dar es Salaam: Seromercy Publishing Company Limited.

FOR ONLINE USE ONLY

Mdee, J. M. (1996). *Sarufi ya Kiswahili Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: DUP.

Mohamed, M. A. (1986). *Sarufi Mpya*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Mulokozi, M. M. (mh.). (2002). *Tenzi Tatu za Kale.* Dar es Salaam: TUKI.

Nkwera, F. M. V. (1978). *Sarufi na Fasihi Sekondari na Vyuo.* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Saidi, M. (1976). *Fani Mbalimbali za Kiswahili 1.* Dar es Salaam: Longhorn Publishers (T) Ltd.

Taasisi ya Elimu Tanzania. (1996). *Kiswahili Kidato cha Kwanza*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Taasisi ya Elimu Tanzania. (1996). *Kiswahili Kidato cha Pili*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Taasisi ya Elimu Tanzania. (2019). *Kiswahili Shule za Sekondari Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tano na Sita, Fasihi*. Dar es Salaam: Taasisi ya Elimu Tanzania.

Taasisi ya Elimu Tanzania. (2019). *Kiswahili Shule za Sekondari Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tano na Sita, Lugha na Sarufi*. Dar es Salaam: Taasisi ya Elimu Tanzania.

Taasisi ya Elimu Tanzania. (2020). *Kiswahili Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Saba*. Dar es Salaam: Taasisi ya Elimu Tanzania.

Taasisi ya Ukuzaji Mitaala. (1988). *Kiswahili Sekondari*. Dar es Salaam: TUMI.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE
FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI_KIDATO CHA KWANZA_5 SEPTEMBER 2021.indd 119 05/09/2021 15:41

TUKI. (2005). *Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili I: Lugha ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

TUKI. (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.

Waihiga, G. (2010). *Sarufi Fafanuzi ya Kiswahili.* Nairobi: Longhorn Publishers (T) Ltd.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. (2005). *Muhtasari wa Kiswahili kwa Shule za Sekondari Kidato cha I-IV.* Dar es Salaam: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

FOR ONLINE USE ONLY

ISBN 978-9987-09-267-3

9 789987 092673